ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita - Tarehe 21 Juni, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani kuchangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 83

Kisiwa cha Mnemba kuliwa na Bahari

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Mnemba ni miongoni mwa Visiwa vidogo vidogo vilivyopo Unguja ambavyo vinatia fedha nyingi kutokana na Utalii. Lakini hivi sasa mazingira ya kisiwa hicho ni mabaya sana kwani upande wa mashariki wa kisiwa hicho chote kimeshaliwa na baharia na kupelekea baadhi ya majengo kuliwa na maji.

Je, serikali ina mpango gani wa kukiokoa kisiwa hicho na hali hiyo mbaya.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna hitilafu imetokezea kuhusu jibu alilokuja nalo Mhe. Waziri ni jibu la swali ambalo halimo katika orodha ya leo. Sasa wacha nitoe ufafanuzi kuwa jibu hilo halipo hivi sasa Waziri akae na swali hili tuliakhirishe litakuja ama baadae kama jibu lipo au pengine litafuata kwa maswali ya kesho.
Mhe. Waziri upumzike.

Nam. 25

Ulipaji wa Deni la Mecco

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Hassan Hamad Omar) – Aliuliza:

Kwa kuwa mradi wa ujenzi wa barabara ya Amani - Dunga, Mfenesini-Bumbwini pamoja na daraja la Mwera, Mwanakombo na kalavati ya Mkokotoni umekamilika, Kampuni ya MECCO ambayo imejenga barabara hizo inaidai Serikali kiasi kikubwa cha fedha kutokana na ujenzi huo.

(a) Je, kama jambo hili ni kweli, kucheleweshа kulipa pesa hizo wanazoidai Kampuni ya MECCO, si kucheleweshа ujenzi wa barabara ya Wete - Konde na Wete - Gando.

(b) Je, ni lini Kampuni hiyo ya MECCO watalipwa pesa zao na kupata nguvu ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Wete - Konde na Wete -Gando.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa njia hizi za Konde na Gando zimechelewa, MECCO kwa bahati mbaya anaidai Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa njia zilizojengwa Unguja na sio kwa fedha ambazo zinajengewa njia za Pemba. Sasa ni madai yake kwamba yeye mtaji wake ni mdogo kwa hivyo suala la kudai halihusiani na madai ya njia za Pemba. Ni yeye mwenyewe Mkandarasi kwamba mtaji wake ni mdogo na angeliiomba serikali iweze kumlipa fedha zake ambazo anaidai kwa njia ambazo zilijengwa Unguja ikiwemo barabara ya Amani – Dunga, Mfenesini – Bumbwini madaraja ya Mwera na Mwanakombo, na kalvati ya Mkokotoni. Kwa hivyo suala la kuchelewa kwa barabara Pemba halihusiani na madai ya mkandarasi, isipokuwa ni mkandarasi mwenyewe madai yake ni kwamba kwa sababu aliyompa *contract* yaani Mkandarasi ni yule yule Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na anayeidai ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa hivyo madai yake ni kwamba anataka alipwe ili aongeze mtaji wake ili aweze kuongeza kasi.

(b) Baadhi ya nyakati ilikuwa ikitokezea Mkandarasi kuchelewa kufika malengo kutokana na kutopatikana kwa maeneo ya ujenzi yaani inaitwa *obstruction* kutokana na kutolipwa kwa mapema fidia ya wale ambao wanaohusika na barabara ile nyumba zilizoko njiani. Hata hivyo ulipaji wa fidia kwa barabara zote sasa hivi umekamilika. Kwa hivyo tatizo hilo haliko tena.

Na kwa upande wa deni la serikali, serikali inafanya juhudi sasa hivi ili kuweza kumlipa mkandarasi ili barabara hizo ziweze kuendelea. Sisi tukishirikiana pamoja na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambapo ndipo deni lilipo tunajitahidi kuona kwamba analipwa mapema ili kazi iweze kuendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kutokidhi swali la msingi kama lilivyoulizwa na Mhe. Hassan miradi ya ujenzi wa barabara inatekelezwa kwa kufuata mipango. Sababu gani zilizopelekea mradi huo kukumbwa na deni kwa kushindwa kufanyika kwa muda muafaka.

Pili, barabara ile tayari ishapigwa *grader* na hivi sasa inaanza kuchimbuka mashimo. Wizara yako itachukua hatua gani angalau kusitiri mashimo yale kwa muda huu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nilisema kwamba madeni ambayo anadai Mkandarasi ni madeni yaliyotokana na barabara zilizojengwa Unguja. Sasa kwa wakati huo ndiko kulikokuwa na ucheleweshaji wa kulipwa Mkandarasi mpaka alipomaliza. Na hii ilitokana na baadhi ya nyakati kwamba yuko mkandarasi aliyeondoka baada ya kutofuata utaratibu na akachukua MECCO. Lakini kwa bahati mbaya deni lake halijalipwa. Kwa hivyo kama nilivyosema mwanzo kwamba kutokana na siku hizo zilizopo bado tuko katika harakati kubwa ya kulipa deni hilo kupitia Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili kuweza kuharakisha kulipa kwa sababu hali ya njia ikiachiwa itaweza kuleta matatizo kwa wananchi.

Ama sehemu zilizochimbuka kwa sababu kapewa Mkandarasi sisi kazi yetu ni kuangalia na kuzungumza na Mkandarasi ili aweze kurudi katika kazi yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hatua gani Wizara yako itachukua kwa muda huu angalau kuziba mashimo yale kwa dharura.

Mhe. Spika: Ninafikiri majibu ameshatoa kwamba atazungumza na Mkandarasi ili kurudia katika sehemu hizo zilizochimbuka au labda kama hukusikia.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ninashukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Kutokana na jibu la msingi Mhe. Waziri alilojibu, alisema kwamba mkandarasi anacheleweshwa na serikali kutokana na sababu ya kutopewa eneo la kufanyia kazi. Hali hiyo basi inapelekea kushindwa kwa serikali kumpa Mkandarasi eneo la kufanyia kazi kunapelekea Mkandarasi kuidai serikali fidia. Na kwa taarifa tulizonazo kwamba kila siku ya Mungu serikali hulazimika kumlipa milioni kumi. Naomba nimuulize Mhe. Waziri je, swali hili ni kweli.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza napenda nieleze kwamba ufadhili unaotoka isipokuwa ule wa MCC uliotolewa na Marekani unatoka kwa kulipia ujenzi wa barabara peke yake, hamna ulipaji wa fidia. Ni bahati nzuri tu kwa mradi ule MCC walikuwa na *component* mbili ulipaji fidia, ulitoka katika ufadhili ule na ujenzi wa barabara ulitoka katika ufadhili ule. Lakini hii mikopo inayotoka ADB, BADEA na kwengineko, wao wanatoa kwa ujenzi wa barabara tu, ulipaji fidia ni jukumu la serikali.

Na kama tujuavyo kwamba barabara zetu nyingi zinazojengwa zina nyumba nyingi sana njiani au karibu na njia yenyewe. Na kwa hivyo fedha zinakuwa ni nyingi za ulipaji fidia. Sasa kutokana na hali ilivyokwenda ni kweli kwamba serikali inachelewa kulipa fidia na sina hakika ni kiasi gani kama ulivyosema milioni kumi, lakini ni uhakika kwamba serikali inapata hasara wakati inapochelewa kutoa eneo la kujenga.

Lakini hata hivyo baada ya kuliona suala hilo Mhe. Spika, sisi sasa hivi tumechukua za dharura kwamba barabara yoyote watayopewa Mkandarasi italipwa fidia kwanza kabla hajapewa lile eneo au hajatia sahihi. Tumeanza na barabara ya Jendele/Cheju, kwa hivyo hivi sasa mkandarasi ana eneo safi kabisa la kujenga bararabara bila kizuwizi.][

. Na karibuni hivi tunatarajia kujenga njia ya Ole/Kengeja tunataka kuchukua mfumo huo huo kwamba akikabidhiwa tu mkandarasi iwe muda mchache anapewa eneo la kujenga barabara.

Kwa sababu ni sahihi kwamba inawezekana hata malipo ya fidia ya kupewa mkandasi yakaizidi ile fidia ya kupewa wananchi wakati wa ujenzi. Kwa hivyo ni suala ambalo tumeliona na Mhe. Spika, tunalishughulikia kikamilifu

ili kuipunguzia gharama serikali na kuwaondoshea wananchi kero za kutolipwa fidia mapema.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, tangu kumalizika njia ya Amani/Dunga na daraja zake hii ni bajeti inafika ya tatu. Sasa kama ndivyo ninamuuliza Mhe. Waziri kuna sababu gani ya msingi ikawa hamaliziwi pesa zake mkandarasi. Na kwa sababu mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, tulikwenda kuitembelea barabara ya Konde mara ya kwanza, na ya pili na ya tatu.

Mkandarasi alitueleza maana barabara ilikuwa inatiwa kifusi mpaka *layer* ya mwisho inaachwa inaharibika inaanza tena mara nyengine, inatiwa kifusi mpaka inafika *layer* ya mwisho kutiwa lami inaachwa inaharibika inaanzwa tena mwanzo. Sasa mkandarasi katueleza kama sababu ya kuchelewa ni kwa sababu ya kuwa anadai fedha zake nyingi zaidi milioni 300 au bilioni tano lakini bado hajalipwa fedha zake. Na akasema kama ni sababu moja inayosababisha kucheleweshe njia zile kwa sababu ya huo mtaji wake. Na kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kama mkandarasi mtaji wake ni mdogo. Je, haoni kama kuna haja ya serikali kufanya kila njia kumlipa fedha zake ili asipate sababu kucheleweshe kujenga barabara yetu. Na kwa sababu ana msingi wa kusababisha kucheleweshe kwa misingi hiyo ya kupata sababu hatuoni kama tutakuwa serikali inabeba lawama hiyo kwa sababu ya barabara ya Konde/Wete haimaliziki.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu la mwanzo kwamba barabara ya Konde na Gando haina deni kwa mkandarasi, isipokuwa ni mkandarasi mwenyewe anachukulia lile deni ambalo anaidai serikali kwa sababu ndio serikali ile ile iliyompa mkandarasi wa kujenga barabara ya Konde/Wete kwamba ndio sababu ya kucheleweshe kuijenga ile. Kwa hivyo na sisi baada ya kutokezea hali hiyo ya dharura na sisi vile vile tushafanya vikao vingi na mikakati ya kuweza kulipwa deni lake ili ziweze kuendelea.

Mkandarasi kama nilivyosema mwanzo anaidai serikali kwa barabara zilizomaliza katika sehemu ya Unguja. Lakini amechukua *advantage* hiyo kwa sababu aliyempa kazi ni yule yule ambaye anajenga barabara ya Konde na Wete/Gando.

Nam. 29

Umuhimu wa Mafunzo ya Ngazi mbali mbali kwa Walimu wa Skuli za Maandalizi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: (Kny. Mhe. Asha Abdu Haji) - Aliuliza:-

Elimu ya maandalizi ni muhimu sana katika kumuandaa mwanafunzi na masomo ya shule za msingi, kutokana na umuhimu huo, kuna haja ya kuanzishwa vyuo vitakavyotoa mafunzo ya ualimu na skuli za maandalizi kuanzia ngazi ya cheti, diploma, *degree* na kuendelea. Lakini kwa masikitiko makubwa mafunzo ya ualimu wa aina hiyo yapo kwa ngazi ya cheti pekee katika Visiwa vyetu vya Zanzibar.

(a) Je, wizara itahakikisha vipi kuwa mafunzo hayo yatapatikana katika ngazi tofauti.

(b) Je, zipo fursa za kimasomo za kujiendeleza kwa walimu ambao watamaliza ngazi ya cheti huko Tanzania Bara, au mwanafuzi akitaka kujiendeleza lazima aende nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 29 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kwamba elimu ya maandalizi ina umuhimu mkubwa katika kumuandaa mtoto kuanzia elimu ya msingi. Kutokana na umuhimu huo ipo haja ya kuanzisha mafunzo ya Ualimu wa maandalizi. Kwa hivi sasa, inaendesha mafunzo kazini (*in service training*) kwa walimu wa maandalizi katika vituo vya walimu vilivyoko Saateni, Unguja; na Chachani Pemba. Mafunzo hayo hayakidhi mahitaji yote ya ualimu wa maandalizi bali yanasaidia katika kuwapa walimu misingi ya awali ya ualimu wa maandalizi. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara yangu haijaanzisha mafunzo ya ualimu wa maandalizi katika vyuo vya ualimu kutokana na ukosefu wa walimu wa kutosha waliobobea katika fani hiyo. Hivi sasa yupo mwalimu mmoja tu mwenye shahada ya ualimu katika fani ya walimu wa maandalizi na walimu watatu wenye stashahada katika fani hiyo. Idadi hiyo ni ndogo kwa ajili ya kuanzisha mafunzo ya ualimu. Hata hivyo, Wizara inafanya maandalizi ya kuanzisha mafunzo hayo katika vyuo

vyake vya ualimu na pia kuendeleza Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuanza kufanya maandalizi ya kuanzisha mafunzo ya fani hiyo katika miaka ya hivi karibuni.

Vile vile, Taasisi ya Ualimu ya Zanzibar imeandaa mtaala utakaotumika katika kufundisha walimu watakaosoma mafunzo hayo ya ualimu wa maandalizi ya ngazi za Cheti. Pia. Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Ualimu cha Chuo Kikuu cha Agakhan kilichopo Dar-es-Salaam kimeandaa mafunzo ya miezi sita ya baadhi ya walimu wetu ambao baadae wanatarajiwa kuwa wakufunzi katika Vituo vya Walimu. Aidha walimu wawili hivi sasa wanachukua mafunzo ya stashahada ya ualimu wa maandalizi katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Walimu hao watakapohitimu kwa jumla yao mafunzo yao watakuwa wakufunzi katika vyuo vyetu vya ualimu na kuwa na uwezo wa kutoa mafunzo hayo.

b) Hivi sasa fursa ya kujiendeleza katika fani ya ualimu wa maandalizi zinapatikana hapa nchini. Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoa mafunzo katika fani ya ualimu wa maandalizi na Chuo cha binafsi kilichopo huko Tanga kinaendesha mafunzo ya stashahada katika fani hii. Hivyo, hakuna haja kwa wanaopenda kujiendeleza katika fani hii kutafuta masomo katika nchi za nje. Pia, Wizara yangu inafanya maandalizi na kutoa mafunzo ya fani hii kwa kuanzia na ngazi ya cheti katika Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Pemba kuanzia mwaka wa masomo wa 2014/2015.

Nam. 24

Ukosefu wa Madawa katika Vituo vya Afya

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny.Mhe. Hassan Hamad Omar) – Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga vituo mbali mbali vya Afya mjini na vijijini kwa ajili ya kuwasogezea wananchi huduma ya afya karibu ili kuwaondolea usumbufu. Kwa masikitiko makubwa sana kituo cha afya Kojani kimekosa dawa kwa muda mrefu na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hao.

(a) Je, Mhe.Waziri ni lini wananchi wa Kojani watarajie kupokea madawa na kuondokana na tatizo hili.

(b) Wizara yako imejipanga vipi katika kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika vituo vya Afya Vijijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza ningependa nitoe maelezo kidogo baadae nijibu. Kwa kawaida, Mhe. Spika, dawa za vituo vya afya zinaletwa nchini chini ya mfumo wa makasha (*Kits*) na huletwa kila baada ya miezi mitatu kutoka Bohari Kuu ya Tanzania MSD. Ingawa kwa sasa kuna vituo vichache ambavyo viko kwenye mradi wa majaribio vinapata dawa kwa utaratibu wa kuomba kile kinachohitajika (ZILS).

(a) Kituo cha afya Kojani ni moja ya kituo ambacho kinapata dawa katika mfumo wa makasha. Kwa mwaka huu *kits* zilipokelewa vituoni mwishoni mwa mwezi wa Februari baada kupita miezi 8. Tayari mwezi wa 5 vituo vimepata dawa kwa utaratibu wa makasha pia vimepokea dawa kikiwemo kituo cha Kojani.

(b) Wizara ina taratibu zake ambazo ni kituo kuripoti taarifa ya tatizo, mikutano ya viongozi wa afya wa Wilaya na Mikoa na pia uongozi wa Wizara kutembelea hospitali na vituo vya afya ili kubaini matatizo na changamoto na kuyapatia ufumbuzi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri mfuko wa fedha wa dunia *global fund* na shirika la kuhudumia watoto kwa muda mrefu walikuwa wakichangia huduma ya dawa kwa pamoja, lakini Oktoba na Disemba hadi mwaka jana wameshindwa kuchangia. Anaweza kulielezea Baraza hili ni sababu gani zilizopelekea kushindwa kuchangia.

Pili, alipokuwa akajibu swali la msingi alisema dawa husambazwa kwa makasha vijijini, lakini kuna kijiji cha Muyuni kuna baadhi ya dawa jana zimekosekana je anaweza kunambia kijiji cha Muyuni Mji Mkongwe au kijiji.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba ayachanganue haya masuala ni maswali ni mawili ambayo hayana uhusiano, analotaka lijibiwe ni lipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nilichouliza Mhe. Spika, mfuko wa fedha wa dunia *global fund* na Shirika la kuhudumia watoto kwa muda mrefu lilikuwa

likichangia mfuko wa dawa kwa pamoja. Lakini kuna taarifa mwaka jana Oktoba hadi Disemba wahisani hao hawakuchangia, anaweza kuliambia Baraza hili kwa nini hawakuchangia.

Pili, alipokuwa akijibu swali la msingi alisema dawa zinasambazwa kwa makasha vijijini lakini kituo cha Muyuni mpaka jana kuna baadhi ya dawa hazijapatikani, anaweza kunambia kijiji cha Muyuni ni Mji Mkongwe au kijiji.

Mhe. Spika: Ninafikiri Mheshimiwa muulizaji swali Mhe. Jaku anahusisha na suala hili kwa sababu ya masuala ya dawa na kwamba kulikuwa na wahisani walikuwa wanatoa dawa ambayo anasema kuanzia mwezi wa Oktoba mwaka jana wamesita kutoa msaada huo wa dawa. Inawezekana anahusisha na suala hili kwamba labda dawa hizo ndio zilikuwa zinasaidia kuondoa hayo matatizo ya usambazaji wa dawa vijijini ikiwa ni pamoja na Kojani. Ninafikiri kama majibu unayo ungelijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya : Mhe. Spika, *global fund* haichangii mfuko wa dawa kuna baadhi tu ya programu kama malaria, ukimwi, kifua kikuu hao ndio wanaofanya mradi na *global fund*, dawa hizo ambazo zinagawanywa vituoni hazina uhusiano na shirika hilo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri wa Afya, suali la nyongeza. Kwanza namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa majibu yake mazuri na tumeyafahamu, lakini kwa sababu Kojani ni kisiwa pamoja na utaratibu wa kutumia makasha lakini kwa sababu Kojani ni kisiwa na inapotokea dharura hulazimika watu kupata tabu sana kuvuka na kuja upande wa pili. Sasa pamoja na utaratibu huo mzuri lakini wameandaaje utaratibu mwengine zaidi kwa ajili ya kuwasaidia ndugu wa Kojani hasa kukiwa kunaweza kukatokea dharura na wakati ni kisiwa hawawezi kuvuka usiku, sasa kuna utaratibu upi walioupanga mzuri zaidi kuwasaidia ndugu zetu wa Kojani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli na Pemba visiwa ni vingi si Kojani tu peke yake, Wete vipo, Mkoani vipo na hapa Unguja vipo, lakini tatizo lililokuwa limejitokeza ni kwamba hao wanaoagiza dawa fedha zao walikuwa wanapeleka moja kwa moja *NSB* hawatupi sisi, kwa hiyo hatukuwa na mamlaka ya kuweza kuzichukua tukatafuta dawa pengine, na kwa kuwa huo ulikuwa ndio utaratibu wao kwa hiyo hatukuweza kuingilia. Lakini hata hivyo baada ya kubaini tatizo hilo sasa hivi tumeamua tutafute utaratibu mwengine ambao tutakuwa tunanunua dawa kwa mfumo mwengine na tutapata watu wengine tofauti na hao *NSB*. Kwa hiyo tutanunua dawa kwa jumla tutakuwa tunazigawanya hapa hapa katika bohari kuu ya kwetu kupeleka katika sehemu hizo. Kwa hiyo nafikiri tatizo hili baada ya

kubadilisha huo mfumo linaweza likaondoka. Kwa hiyo tutegemee mabadiliko mwaka huu wa fedha ujao.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza suali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Mhe. Naibu Waziri, pamoja na juhudi kubwa za wizara yako ya kusogeza huduma za afya vijijini, lakini bado kuna baadhi ya vijiji vina changamoto za huduma za afya na hadi wananchi kuamua kujijengea wenyewe kwa nguvu zao vituo katika vijiji, na kwa kuwa Mhe. Rais katika ziara zake za Mikoani alitoa agizo kwamba vile vituo ambavyo vimeanzishwa kwa nguvu zao wamaliziwe wananchi ili kuwapunguzia changamoto hizo. Je, Wizara yako ni vituo vingapi vilivyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambavyo mmevimaliza, na kama bado hakuna je, Wizara ina mpango wa kuvimalizia vituo hivyo ili kupunguza changamoto zinazowakabili wale wananchi ambao huduma za afya haziko karibu nao.

Mhe. Spika: suali liko moja kwa moja na suala mama haidhuru yote ina maana ya huduma za afya, lakini huku mna suali inayohusu dawa huko ni masuala ya ujenzi kumaliza vituo. Nikuombe basi Mhe. Salma suala hili ulitafutie utaratibu kuuliza kwenye suala la msingi.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe nikuombeni radhi tuendelee na lile suala la kwanza nimuombe tena Mhe. Abdi Mossi Kombo suali Na. 83 kama anataka lijibiwe.

Nam. 83

Kisiwa Cha Mnemba Kuliwa Na Bahari.

Mhe. Abdi Mossi Kombo - Aliuliza:-

Mnemba miongoni mwa Visiwa vidogo vidogo vilivyopo Unguja ambayo vinatia fedha nyingi kutokana na utalii. Lakini hivi sasa mazingira ya kisiwa hicho ni mabaya sana kwani upande wa mashariki wa kisiwa hicho chote kimeshaliwa na bahari na kupelekea baadhi ya majengo kuliwa na maji.

Je, serikali ina mpango gani wa kukiokoa kisiwa hicho na hali hiyo mbaya.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, na mimi naomba nimuombe radhi sana Mhe. Abdi Mossi Kombo, kwa kuja na suali lenye nambari ambavyo sivyo lilivyoandikwa na yeye mwenyewe, lakini nakuhakikishia Mhe. Spika, na Mhe. Abdi pamoja na

Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba hivi sasa tuna suali halisi kama ambavyo Mhe. Abdi amelileta ndani ya Baraza.

Kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 83 naomba nikubaliane naye kwamba kisiwa cha Mnemba ni miongoni mwa visiwa vidogo vidogo tulivyonavyo ambavyo hutuingizia fedha kutokana na shughuli za Utalii. Aidha, naomba nikiri juu ya hali mbaya ya kisiwa hicho. Hata hivyo, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa kisiwa cha Mnemba ni eneo moja tu ikilinganishwa na maeneo mbali mbali ya fukwe za visiwa vya Zanzibar pamoja na mafungu tuliyonayo baharini ambayo yanaendelea kuathiriwa na mmong'onyoko kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili pamoja na wananchi kwa ujumla kufuata miongozo ambayo wataalamu wetu wanaendelea kutoa ikiwa ni pamoja na kuacha shughuli zozote zinazosababishwa na sisi wenyewe katika kuchangia uharibifu wa mazingira, lakini vile vile kufuata ushauri wa kuhifadhi maeneo hayo.

Mhe. Spika**,** baada ya maelezo hayo, sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 83 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais hivi sasa haijawa na mpango maalum wa moja kwa moja wa kukiokoa kisiwa hicho kutokana na hali hiyo mbaya. Hii inatokana na kwamba suala lenyewe la mabadiliko ya tabia nchi ni jipya katika visiwa vyetu, hivi sasa ofisi yetu imo katika kuandaa mpango mkakati wa mabadiliko ya tabia nchi ambao utafuatiwa na kuandaa mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake mbali mbali ambazo zimejitokeza katika visiwa vyetu. Hata hivyo Kisiwa hicho ambacho hivi sasa kimekodishwa kwa muwekezeshaji, Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais inaendelea kufanya mazungumzo na muwekezaji wa Kisiwa hicho katika kuzungumzia juu ya jitihada za kuzuia mmong'onyoko unaendelea kwenye kisiwa hicho na Ofisi yangu ipo tayari kuendelea kutoa ushirikiano zaidi kadri ya hali inavyoendelea.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri suali dogo la nyongeza. Kwa vile kisiwa cha Mnemba kama ulivyosema katika suala lako mama ulisema kwamba ni kisiwa ambacho kinatia fedha nyingi katika Serikali. Je, Mhe. Waziri, Wizara yako haioni kwamba kuchelewa kukihifadhi kisiwa kile ili kuangamia na mmong'onyoko wa maji ya bahari, huoni kwamba Serikali itaingia hasara, ikiwa bado kisiwa kile hakijafanywa uhifadhi wa haraka haraka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana, Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu suali la nyongeza la Mhe. Abdi Mossi Kombo kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kisiwa hichi kwa muda mrefu kiko katika usimamizi wa muwekezaji, lakini hata hivyo Serikali inafanya mazungumzo ya karibu na wawekezaji hawa kuona hatua za awalimu ambazo zinaweza kuchukuliwa katika kuzuia mmong'onyoko huo, Serikali haijatulia na inafanya jitihada hizo. Hata hivyo, uzuiaji wa athari zinazoletwa na mabadiliko ya tabia nchi si kitu cha kuleta tija ya haraka kwa mara moja ikaweza kuonekana, ni jambo ambalo linachukua muda ili ionekane kwamba sasa tumeweza kuhifadhi fukwe hizi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize suali moja la nyongeza Mhe. Waziri, kwenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alivyokuwa akijibu suala hili la kupanda kwa maji alilihusisha zaidi na mabadiliko ya tabia nchi. Lakini Mhe. Waziri, atakubaliana na mimi kwamba uharibifu wa mazingira uliopo katika kisiwa cha Mnemba huwenda umesababishwa na ujenzi mbaya usiozingatia sheria ambapo wenye mahoteli wengi hasa katika maeneo ya juu wameisogelea sana bahari kinyume na taratibu za ujenzi. Lakini pili Wizara yako itasimamiaje kuona ujenzi wote uliokiuka utaratibu wa sheria au utaratibu wa mazingira unavunja mara moja ili kuepukana na matatizo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhsa yako napenda kujibu masuali mawili ya nyongeza ya Mhe. Salmin Awadh Salmin kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ninaomba nikubaliane naye kwamba athari za mabadiliko ya tabia nchi ni njia moja wapo tu ya kuharibu mazingira lakini zipo ambazo zinasababishwa na sisi wenyewe wanaadamu ikiwemo kwa miti lakini pia ujenzi holela ndani ya fukwe zetu, hilo haliepukiki kabisa. Katika kesi hii ya Mnemba kwa kweli kwa sasa hivi sina *data* halisi inayoonesha kama nao ujenzi umechangia katika suala hili, ni jambo ambalo naweza kumletea baadae kwamba nalo limechangia. Hata hivyo, kuhusu suala lake la pili kwamba kutaka Ofisi yetu kwamba wale wote ambao wamejenga katika fukwe basi waweze kubomolewa uwekezaji wao mara moja, Mhe. Spika, hilo ni suala la kisheria ndani ya Ofisi yangu, ndani ya Idara ya Mazingira hatuna sheria inayotuelekeza kufanya hivyo. Suala zima la usimamizi wa majenzi ya uwekezaji na maeneo ya kuishi wananchi lipo chini ya Wizara ya Ardhi na wao ndio wenye sheria ya kudhibiti hivyo. Hata hivyo suala hilo ni la

kisheria huwezi ukachukua hatua moja kwa moja, lakini hivi sasa tunaifanyia marekebisho sheria yetu ya mazingira ili kuona kwamba sisi wenyewe pia tunakuwa na nguvu ya kusimamia kwamba angalau hivi sasa basi isitokee uwekezaji ambao utakwenda kinyume na maagizo ambayo yanatolewa na wataalamu wetu wa mazingira na wataalamu wa ardhi vile vile.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri, swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri kajibu vizuri na namshukuru sana, lakini kwa kuwa yeye Wizara yake ndio mtunzaji wa mazingira na ndie msimamizi mkuu wa mazingira, na kwa kuwa watu wanapochafua mazingira yeye anastahiki kuingilia kati na kuangalia. Kwa kuwa kuna wawekezaji wanajenga mahoteli mpaka ndani ya kupita mita 30 zile walizowekewa na kwa kuwa Wizara ya Ardhi ndiyo yenye haki ya kuweza kutoa nafasi ya kuwa waende wakavunje.

Je, Wizara yake imejipanga vipi kusimamia hilo kuona kwamba Wizara ya Ardhi inawashirikisha wanapompa mjenzi wa hoteli muwekezaji wao watunzaji wa mazingira wakaenda wakaangalia na wakaweka masharti yao.
Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais: Ahsante kwa ruhusa yako napenda kujibu swali la nyongeza la Mhe. Subeit, kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Ofisi yetu kupitia Idara ya Mazingira ina jukumu la kuhakikisha kwamba mazingira hayachafuliwi na yanahifadhiwa. Lakini kwa ujumla suala la mazingira ni suala mtambuka Mhe. Spika. Na katika kesi hii ya ujenzi ambao usiozingatia sheria ya ardhi, ofisi yetu kubwa pahala pake ambapo walichoweza kufanya ni kupeleka *stop order* kuzuia ujenzi huo. Kwa sheria iliyopo sasa Idara ya Mazingira haiwezi kwenda zaidi ya hapo, baada ya kupiga *stop order* huwa tunaiandikia Wizara ya Ardhi, kitengo kinachohusika ili kuchukuliwa hatua inayofuata hapo. Lakini Mhe. Spika, kwa kuligundua hilo na kwa kugundua kwamba sheria yetu ya mazingira haina meno, naeleza tena kwamba karibuni tutawaletea sheria ya mazingira ili Idara ya Mazingira yenyewe iwe na uwezo na nguvu ya kusimamia masuala hayo na sio moja kwa moja kutegemea wadau wengine.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nimearifiwa kwamba kuna wageni, wageni hawa ni wageni wetu sisi wenyewe, timu ya mpira wa miguu na mpira wa Netball ya hapa Baraza la Wawakilishi. Wageni hawa kwanza walikuwa na shughuli moja muhimu sana hapo nje, naomba kwanza tutoe taarifa hiyo na baadae nitawatambulisha kwenu.

Waheshimiwa Wajumbe, ujumbe wa wageni wetu wa leo ni ujumbe wa wafadhili wetu wa michezo kutoka Kampuni ya *Grand Malt*, wamekuja hapa kwa ajili ya kutoa msaada wa vifaa vya michezo kwa timu zetu mbili za Baraza la Wawakilishi yaani mpira wa miguu pamoja na mpira wa mikono *Netball*. Tayari wameshakabidhi vifaa hivyo na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alivipokea vifaa hivyo hivi asubuhi na baadhi ya vifaa vilivyopokelewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni kama hivi ifuatavyo:-

Wafadhili wetu hawa au wahisani wetu wametoa seti mbili za jezi kwa mpira wa miguu, seti mbili za jezi kwa ajili ya mpira wa mikono, viatu kwa timu zote mbili, mipira kwa timu zote mbili pamoja na *track suit* tunategemea kwa timu zote mbili. Vifaa hivyo vinagharimu Sh. 9,500,000/=. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yenu kama alivyofanya hivyo kwa niaba yetu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuwashukuru sana ndugu zetu hawa wa *Grand Malt* kwa misaada mikubwa ambayo mara kwa mara wamekuwa wanatuletea pamoja na mara nyingi kudhamini michezo yetu ambayo tunacheza na timu nyengine. Na sasa niombe wageni wetu hawa ambao walikuja kutufariji hivi leo mapema asubuhi kwa kutuletea vifaa sasa wasimame ili kuwasalimia Waheshimiwa Wajumbe *(Makofi).*

Ndugu zetu wa *Grand Malt* karibuni sana na tunawashukuru sana kwa misaada yenu mikubwa mnayotupa kwa timu zetu za michezo hapa Baraza la Wawakilishi. Ahsante sana karibuni.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/14 - Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kofi hizo ziwe za kheri zijaalie mafanikio, zijaalie njia ya kupitisha bajeti vizuri.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kutoa maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais napenda kuchukua nafasi hii

kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini na ujasiri mkubwa wa kuiongoza nchi yetu. Sote tunakiri kuwa Dkt. Shein ameendelea kuchukua juhudi kubwa katika kutoa miongozo sahihi ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu kwa maslahi ya wananchi wote, na ni kiongozi anayejituma sana na kuwa mfano wa hekima, uvumilivu na uadilifu. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema na umri mrefu yeye na familia yake, amzidishie hekima na busara ili aendelee kuiongoza nchi yetu katika kipindi hiki cha mageuzi makubwa ya kiuchumi na uwajibikaji. Chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein tunaendelea kujivunia mafanikio makubwa katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mhe. Spika, vile vile, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Makamu wa Kwanza Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa juhudi zao kubwa wanazochukua katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuiongoza nchi yetu. Viongozi wetu hawa wameendelea kuwa mstari wa mbele wa kufuatilia utendaji katika Serikali na kuona matatizo ya wananchi yanapewa kipaumbele katika mipango ya maendeleo na kusimamia kwa karibu sana utekelezaji wake.

Mhe. Spika, unastahiki pongezi za pekee wewe mwenyewe binafsi kwa jinsi unavyoliendesha Baraza letu kwa umahiri na umakini mkubwa. Wewe ni hazina kwa nchi yetu kutokana na uzoefu wako mkubwa wa kuliendesha Baraza kwa mafanikio yaliyo wazi. Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu akuzidishie uwezo na hekima katika kutimiza majukumu yako haya ya Kitaifa. Naomba pia kuwapongeza Naibu Spika Mhe. Ali Abdalla Ali na Wenyeviti wetu wa Baraza Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalumu na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Spika katika kuliendesha Baraza letu hili.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa malengo na majukumu na kwa ushauri na maelekezo wanayoyatoa kwa Wizara wanazozisimamia. Aidha, natoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, Makamu Mwenyekiti Mhe. Saleh Nassor Juma na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na michango na ushauri walioutoa. Tunawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati hii waliomaliza muda wao kwa mashirikiano mazuri waliyotoa kwa Ofisi yetu katika kipindi chote walichotumikia Kamati hii.

Mhe. Spika, pia nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa kuipitisha Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Bajeti ya Serikali iliyopitishwa ndio itakayotuwezesha kuendesha kazi za Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014. Bajeti hiyo ya Serikali imezingatia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II).

HALI YA SIASA

Mhe. Spika, nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu na hivyo kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo. Amani na Utulivu huu tulionao ni matunda ya juhudi za viongozi wetu katika kujenga Zanzibar mpya ya umoja na maelewano. Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuiweka nchi yetu katika hali hii ya amani na utulivu. Pia tunatoa shukrani nyingi kwa viongozi wetu wote katika ngazi zote na wananchi wote kwa ujumla kwa kuendelea kuwa watulivu na kudumisha amani katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 27/3/2013 nchi yetu ilipata msiba mkubwa wa kuondokewa na Mbunge wetu wa Jimbo la Chambani Mheshimiwa Salum Hemed Khamis. Huu ni msiba wetu wote na tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahala pema peponi. Amin. Aidha, nachukua fursa hii kutoa mkono wa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, wananchi wa Jimbo la Chambani na uongozi mzima wa Chama Cha Wananchi (CUF) kutokana na msiba huo.

Mhe. Spika, kutokana na kifo cha Mbunge huyo wa Jimbo la Chambani, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliendesha Uchaguzi mdogo wa kumpata Mbunge mpya wa Jimbo hilo siku ya Jumapili tarehe 16/6/2013. Tunavishukuru vyama vyote vya siasa vilivyoshiriki katika uchaguzi huo na tunawapongeza wananchi wa Jimbo la Chambani kwa kushiriki katika uchaguzi huo mdogo kwa amani na utulivu mkubwa na kumpata kiongozi wao mpya. Mheshimiwa Spika, sasa uchaguzi umemalizika, hivyo hatuna budi kuendelea kushirikiana katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar itaendesha uchaguzi mdogo wa nafasi ya Diwani katika Wadi ya Ng'ombeni, Wilaya ya Mkoani tarehe 23 Juni, 2013. Tunawaomba wananchi wa Wadi hiyo kushirikiana na Tume kufanikisha uchaguzi huo kwa amani na utulivu ili tuendeleze umoja wetu tulionao katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeanza matayarisho ya kulipitia Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kuandikisha wapiga kura wapya na kuwaondoa wale wote ambao wamepoteza sifa ya kuwa wapiga kura kwa mujibu wa sheria. Aidha, katika uandikishaji huu, wananchi waliopoteza vitambulisho vyao vya kupiga kura wataweza kupatiwa vitambulisho vipya. Naomba kuwasihi viongozi wezangu wote na wananchi kwa ujumla tushirikiane vizuri na Tume ya Uchaguzi katika kuendesha zoezi hili. Huu ni wakati muhimu kwetu kuidhihirishia dunia kwamba Wazanzibari ni wamoja pamoja na kuwepo kwa tofauti za kiitikadi za kisiasa miongoni mwetu.

Mhe. Spika, pamoja na ukweli kwamba hali ya amani na utulivu katika nchi yetu inazidi kuimarika, bado wapo watu wachache miongoni mwetu ambao wamekuwa wakiendeleza vitendo vinavyoweza kuipeleka nchi yetu katika hali ya kuvunjika kwa amani, umoja na maelewano tuliyonayo. Watu hao wamekuwa wakiwahujumu wananchi wenzao kwa kuwamwagia tindikali na kuwahujumu viongozi wa dini. Serikali imesikitishwa na kuhuzunishwa sana na kitendo cha kumwagiwa tindikali Sheikh Fadhili Soraga kilichotokea tarehe 6/11/2012 na kumsababishia maumivu makali na athari kubwa katika mwili wake. Kitendo kama hiki kimetokea tena kwa Sheha wa Shehia ya Tomondo Mohamed Omar Said Kidevu tarehe 23/5/2013 na kujeruhiwa vibaya katika baadhi ya sehemu za mwili wake. Hivi ni vitendo vya kihalifu vinavyofanywa na watu wasio na huruma na ubinaadamu kwa wenzao.

Mhe. Spika, Aidha, matukio ya kupigwa risasi na kujeruhiwa vibaya Mchungaji Amrose Mkenda wa Kanisa Katoliki tarehe 25/12/2012 huko katika maeneo ya Tomondo na kuuawa kwa Padre Evaristus Gabriel Mushi kwa risasi katika eneo la Beit- el- Ras tarehe 17/2/2013 ni vitendo vya kuifedhehesha nchi yetu na kuihatarisha amani tuliyonayo. Serikali inatoa mkono wa pole kwa wote waliofikwa na mikasa hiyo na kuwaombea kwa Mungu awarudishie afya yao ili tuweze kuungana nao tena katika kuijenga nchi yetu. Tunawaomba ndugu na jamaa wa Marehemu Padre Evaristus Gabriel Mushina Waumini wote wa dini ya Kikiristo na wananchi kwa ujumla kuendelea kuwa wastahamilivu kutokana na machungu ya msiba huu. Serikali kwa mara nyengine tena inawasihi wananchi wote kutojiingiza katika vitendo vya uvunjifu wa amani na kujichukulia hatua mikononi mwao kwani haitamvumilia mtu yeyote atakaepatikana na makosa hayo.

MASUALA YA MUUNGANO

Mhe. Spika, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hivi sasa umetimiza miaka 49 tangu ulipoasisiwa tarehe 26 Aprili, 1964. Muungano wetu huu utatimiza nusu karne (miaka 50) ifikapo Aprili, 2014. Kipindi cha miaka 50 ni kipindi kirefu na nchi yetu ina kila sababu za kujivunia kutokana na

kuudumisha muungano huu kwa kipindi chote hicho. Yapo mafanikio mengi yanayotokana na muungano huu, ikiwa ni pamoja na kuwa na amani na utulivu katika nchi yetu. Tanzania ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika ambayo inasifika kwa amani na utulivu na imekuwa ni kivutio kikuu cha uwekezaji na Utalii. Aidha, Muungano huu umeweza kutoa fursa za kuwaunganisha wananchi wa pande mbili za Muungano. Kutokana na Muungano huu, wananchi wanayo nafasi kubwa ya kujiendeleza kiuchumi kwa kutumia rasilimali ziliopo na soko.

Mhe. Spika, pamoja na kuwepo na mafanikio makubwa, Muungano wetu unaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zilizopelekea kuwepo kwa manung'uniko ya wananchi wa pande zote mbili. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamati ya Pamoja inayoongozwa na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo. Tangu kuundwa kwa Kamati hii, jumla ya changamoto 13 ziliwasilishwa na kujadiliwa na kati ya hizo changamoto sita (6) zimeshapatiwa ufumbuzi (Kiambatanisho Nam. 1).

Mhe. Spika, kama sote tunavyoelewa nchi yetu imo katika kipindi muhimu cha matayarisho ya kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume ya Mabadiliko ya Katiba tayari imekamilisha Rasimu ya Awali ya Katiba hiyo mpya na kuzinduliwa rasmi tarehe 3/6/2013 huko Dar es Salaam. Hatua inayofuata hivi sasa ni kupitiwa rasimu hiyo na Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na Mabaraza mengine maalumu yanayoundwa kwa mujibu wa Muongozo wa Tume.

Mhe. Spika, hatua tuliyofikia hivi sasa katika mchakato wa kuandaa Katiba Mpya ni hatua muhimu sana na ni hatua inayohitaji utaalamu zaidi katika kujenga hoja za msingi ili kupata Katiba itakayokuwa na maslahi kwa nchi yetu. Huu si wakati wa kuhitilafiana na kulumbana bali ni wakati wa kuwa makini na kushikamana kwani tunafanya maamuzi yenye hatma ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mambo yanayogusa nchi na watu wake ndio msingi wa uhai wa taifa lolote duniani na Katiba ndio dira kuu ya kuongoza nchi, hivyo sisi viongozi wote tuna wajibu mkubwa wa kuonyesha njia na sio kupotosha umma kwa utashi wa kisiasa na maslahi binafsi. Aidha, huu si wakati wa kujitafutia umaarufu wa kisiasa, kudharauliana au kukebehiana bali ni wakati wa kushikamana na kusaidiana Mabaraza ya Katiba yaweze kutoa maoni mazuri ya kuboresha rasimu ya Katiba hii ili yakidhi matarajio ya wananchi.

Mhe. Spika, ikumbukwe kuwa tunafanya yote haya kwa manufaa ya watu wetu, hivyo maoni yetu yawezeshe wananchi kufanya shughuli zao za

kawaida za maisha bila ya bughudha na usumbufu katika upande wowote wa muungano wetu. Hatuna budi kupima tulikotoka, tulipo hivi sasa na tunakoelekea kwani kila siku "Majuto ni Mjukuu". Nawasihi Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba kujitokeza kutoa maoni yao yatakayokuwa na tija kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti na Makamu wake na Wajumbe wote wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kazi kubwa waliyoifanya kutupatia Rasimu ya Awali ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kazi kwetu wananchi kutoa maoni yetu kuhusu Rasimu hiyo kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

HALI YA UCHUMI NA MIPANGO YA SERIKALI YA KUIMARISHA UCHUMI

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati wa kuwasilisha hotuba yake ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 katika Baraza lako Tukufu, uchumi wa Zanzibar umekua kwa asilimia 7.0 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2011. Pato la Taifa kwa bei za miaka husika limefikia jumla ya Sh.1,354 bilioni kwa mwaka 2012 kutoka Shs. 1,198 bilioni kwa mwaka 2011. Kasi hiyo
ya ukuaji wa asilimia 7.0 ni ya juu katika kipindi cha miaka mitano
iliyopita.

Mhe. Spika, Mwaka 2012 Pato la kila mtu limeongezeka kufikia wastani wa Shilingi 1,003,000 (USD 638) kutoka wastani wa Shilingi 960,000 (USD 617) kwa mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Miongoni mwa mambo yaliyochangia ukuaji huo wa uchumi ni kama ifuatavyo:

i. Ongezeko la ukuaji raslimali kwa asilimia 41.3 kutoka thamani ya Shilingi 183.2 bilioni mwaka 2011 mpaka Shilingi 258.9 bilioni mwaka 2012. Ongezeko hili limesababishwa na uwekezaji mkubwa katika maeneo ya ujenzi wa nyumba za kuishi na biashara, zana za usafirishaji na ujenzi vijijini.

ii. Ukuaji mzuri wa sekta ya viwanda ambayo imekua kwa asilimia 9.2 mwaka 2012 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2011.

iii. Kuimarika kwa sekta ya huduma ambayo imekua kwa asilimia 8.7 mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.6 mwaka 2011.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wa Zanzibar kwamba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na kiongozi makini Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein inafanya kazi kubwa ya kuiletea nchi yetu maendeleo ya kiuchumi. Katika kufanikisha hayo serikali inaendelea kutekeleza sera na mipango na miradi ya maendeleo yenye tija na kuendeleza sekta za kilimo, uvuvi, mifugo, utalii na viwanda.

Mhe. Spika, katika kuendeleza juhudi za serikali za kuwaletea wananchi maendeleo na kupunguza tatizo la nishati ya umeme, nchi yetu imeshuhudia tukio muhimu la uzinduzi wa waya mpya wa umeme wenye uwezo wa kuchukua umeme wa MegaWatts 100 uliotandikwa kuanzia Ras Kiromoni hadi Fumba. Uzinduzi huo ulifanywa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, mnamo tarehe 10 Aprili 2013. Mradi huu umefadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Mradi wa Changamoto za Milenia (MCC). Aidha, Mhe. Rais, tarehe 11 Juni, 2013 alizindua kukamilika kwa Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya ndani ya Umeme katika Kituo Kikuu cha Umeme Mtoni, mradi ambao umefadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA. Mradi huu umegharimu jumla ya Shilingi Bilioni 57.

Mhe. Spika, kutokana na kuimarika kwa miundombinu hiyo ya umeme nchi yetu itaweza kuvutia wawekezaji wa ndani na kutoka nje kuwekeza nchini na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo ya jamii. Hivi sasa nchi yetu imeondokana kabisa na tatizo la mgao wa umeme ambao uliwaletea usumbufu mkubwa wananchi wetu katika harakati zao za kujiletea maendeleo.

Mhe. Spika, pamoja na hatua hii ya mafanikio, serikali inaendelea na juhudi za kutafuta nishati mbadala ili kuwa na vyanzo vya uhakika vya nishati na vyenye gharama nafuu vikiwemo matumizi ya nguvu za jua (*solar*), upepo, mawimbi ya bahari na *"bio gas"*.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA KUONGEZA FURSA ZA AJIRA

Mhe. Spika, masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kukuza ajira ni miongoni mwa mambo yanayopewa kipaumbele na serikali kwa kutekeleza mipango mbali mbali inayolenga kuwawezesha wananchi kiuchumi hususan wale wenye kipato cha chini ili waweze kumudu maisha yao ya kila siku.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuwainua wananchi kiuchumi, serikali imeendelea na hatua za kuwawezesha wananchi kwa kuwapatia taaluma ya

uzalishaji na masoko ya bidhaa zao na kuwapatia fursa za mikopo kupitia Mfuko wa Kujitegemea na Mfuko wa AK/JK. Vile vile serikali imeendelea na uhamasishaji wa uundwaji wa vyama vya ushirika na uanzishwaji wa vikundi vya wajasiriamali kwa lengo la kuwaweka wananchi pamoja na kutumia nguvu ya umoja huo kupata fursa ya mitaji, taaluma na masoko ya uhakika kwa bidhaa zao.

Mhe. Spika, suala la ajira kwa vijana linaendelea kutiliwa mkazo na serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa vijana wote ama wanaajiriwa au wanajiajiri wenyewe katika kazi za heshima (*Decent Work*). Kupitia Wzara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kazi Nje Nje yenye lengo la kuwapatia vijana mwamko wa kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea kuajiriwa.

SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

Mhe. Spika, katika kuimarisha sekta ya huduma za jamii, serikali inaendelea na juhudi zake za kuwapatia wananchi wa Zanzibar elimu, huduma za afya na maji safi na salama. Maji ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya viumbe vyote hapa duniani. Bila ya maji hakuna maisha, na bila maji safi na salama hakuna afya. Serikali inatambua kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka siku hadi siku na hivyo kufanya mahitaji ya maji nayo kuongezeka kwa kasi kubwa. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2012, hivi sasa Zanzibar ina jumla ya wakaazi 1,303,569 na kati ya hao, Mkoa wa Mjini Magharibi pekee una jumla ya wakaazi 593,678. Takwimu hizo za Sensa pia zinaonesha kuwa idadi ya watu hapa Zanzibar inaongezeka kwa kasi ya asilimia 2.8 kwa mwaka.

Mhe. Spika, iIi kwenda sambamba na ongezeko hilo la idadi ya watu na ukuaji wa miji, serikali inaendelea na mipango yake ya kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama nchini. Mipango hiyo ni pamoja na uhuishaji na upanuzi wa shughuli za maji mijini na vijijini, ubadilishaji wa mabomba chakavu na uwekaji wa mabomba mapya, uchimbaji wa visima zaidi ya 80, ununuzi pamoja na ufungaji wa mota, pampu na mita kwa wateja. Aidha, mipango hiyo inahusisha ujenzi wa matangi ya maji na sehemu ya kuweka mitambo ya kusukuma maji.

Mhe. Spika, serikali inawaomba wananchi kuthamini jitihada hizi zinazochukuliwa na serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji nchini kwa kuongeza ulinzi, upandaji miti na uhifadhi wa vyanzo na miundombinu ya maji.

Mhe. Spika, kufuatia ajali ya kuanguka kwa ukuta wa mnara wa tangi la maji hapo Machomanne Chake Chake Pemba, tarehe 2 Juni 2013 na kusababisha vifo vya watu watatu na kujeruhi watu wengine watatu, serikali inatoa mkono wa pole kwa wafiwa na kuwaombea Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema Peponi, Amin na kuwatakia majeruhi afya njema. Serikali imewatembelea waathirika hao na kutoa ubani wake.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Elimu, serikali inaendelea na mipango yake ya kuwapatia vijana wetu elimu bora kwa kujenga skuli mpya za kisasa kila wilaya, kujenga maabara na kuzipatia vifaa skuli hizo na kuwapatia wanafunzi wote wa Sekondari vitabu vya kusomea. Aidha, serikali inatilia mkazo zaidi suala la mafunzo ya walimu, uajiri na mgawanyo wa walimu hasa wa masomo ya sayansi kwa uwiano mzuri wa skuli za mijini na vijijini.

Aidha, kwa nia ya kujipatia madaktari wa kutosha nchini, katika mwaka huu wa fedha, serikali inakusudia kuanzisha mafunzo ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya serikali inaendelea na mipango yake ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya rufaa, kujenga hospitali kubwa na ya kisasa Mkoani Pemba, kuyafanyia ukarabati majengo ya zahanati na vituo vya afya kwa Unguja na Pemba na kuwa na mpango mzuri wa upatikanaji wa dawa wakati wote. Kwa upande wa wataalamu mipango ya kusomesha madaktari na wataalamu wengine wa sekta ya afya inaendelea.

MIGOGORO YA ARDHI

Mhe. Spika, suala la migogoro ya ardhi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu bado linaendelea kujitokeza na kuripotiwa katika ofisi yetu. Malalamiko hayo zaidi yanahusu uvamizi wa maeneo ya wazi na uuzaji kiholela wa mashamba na viwanja. Tabia ya wananchi na baadhi ya viongozi kuuza ardhi bila kufuata sheria na taratibu ziliopo ndio chanzo kikubwa cha migogoro hiyo. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili, serikali imewaelimisha Masheha wote Unguja na Pemba kuhusu Sheria ya Matumizi ya Ardhi nchini na kuwataka kujiepusha ama kuingia au kusababisha migogoro hiyo. Aidha, serikali imeanzisha Ofisi ya Mrajis wa Ardhi kwa ajili ya kusajili ardhi na kuwatambua wenye haki ya matumizi ya ardhi na mnamo tarehe 28/03/2013, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizindua rasmi zoezi la Usajili wa Ardhi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, juhudi zaidi zinazoendelea kuchukuliwa na serikali ni kutoa elimu kwa viongozi na wananchi kufuata taratibu za kusajili ardhi na kuwa na haki ya kuitumia. Zoezi hili limeanza katika maeneo ya Mji Mkongwe na

litaendelea kwenye shehia nyengine kwa utaratibu utakaopangwa. Natoa wito kwa viongozi na wananchi wote tufuate taratibu za kusajili maeneo yetu ya ardhi kama vile mashamba binafsi, mashamba ya eka tatu tatu na maeneo mengine ya wazi ili tupate haki ya kuweza kuyatumia kihalali na bila ya kubughudhiwa, hivyo kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

SENSA YA WATU NA MAKAAZI

Mhe. Spika, tarehe 27 Agosti 2012 wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walishiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi na zoezi hilo liliendelea kwa muda wa wiki mbili. Viongozi na wananchi walipata fursa ya kushiriki katika kutoa taarifa zilizohitajika. Pamoja na changamoto mbali mbali zilizojitokeza, zoezi hilo liliendeshwa vizuri na kwa mafanikio makubwa. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nawashukuru sana viongozi wote na wananchi kwa jumla kwa kushirikiana na serikali yao katika kufanikisha zoezi hili muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Sensa, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wabunge, Wajumbe wa Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya pamoja na Masheha kwa mashirikiano yao. Kwa namna ya pekee tunazishukuru na kuzipongeza Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliendesha zoezi hili kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Spika, matokeo ya awali ya sensa yalizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mnamo tarehe 31 Disemba, 2012 na yalionesha kwamba Watanzania tuko 44,928,923 ambapo Tanzania Bara ina wakaazi 43,625,354 na Zanzibar ina wakaazi 1,303,569. Kazi inayoendelea hivi sasa ni kuzichambua takwimu hizo ili kuweza kupata matokeo Kishehia, Kiwilaya na makundi mbalimbali ya kijamii.

Mhe. Spika, matokeo ya sensa yanaonesha kuwa tumekuwa tukiongezeka kwa kasi sana, ongezeko ambalo linaongeza mahitaji ya huduma za kiuchumi na kijamii na kulazimika kuzingatia ongezeko hilo katika mipango yetu ya maendeleo.

MASUALA MTAMBUKA, UKIMWI

Mhe. Spika, katika juhudi za kudhibiti UKIMWI nchini hasa maambukizo mapya, serikali kupitia Tume ya UKIMWI inatekeleza mipango mbali mbali ikiwemo kuongeza uwezo wa program za habari, utetezi na mawasiliano katika kuchochea mabadiliko ya tabia zinazochochea maambukizi mapya ya

virusi vya UKIMWI. Aidha, Tume ya UKIMWI imeendelea na program ya kutoa elimu ya UKIMWI inayohusu mpango wa kuimarisha uwezo wa jamii kupambana na UKIMWI *(Community Capacity Enhancement Program-CCE).*

Mhe. Spika, natoa wito kwa wananchi wote kujiepusha na mambo yote yanayoweza kusababisha maambukizi mapya ya UKIMWI na kuacha kuwanyanyapaa wale ambao wamepata maambukizi hayo. Pia ni vyema kwa kila mmoja wetu kuwa na tabia ya kuchunguza afya yake kila baada ya muda ili kujua kama yupo salama au ameambukizwa. Kama mtu ameambukizwa na kujua mapema atapata matibabu mapema na hivyo kuweza kurefusha umri wa maisha yake.

MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Spika, hali ya Watu wenye Ulemavu ni moja ya mkakati wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujenga usawa na kuheshimu haki za binadamu. Juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na serikali katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Watu Wenye Ulemavu *(United Nations Conventions of the Rights of Person with Disability)*, sambamba na utoaji wa mwamko kwa wananchi juu ya kuzingatia mahitaji maalum ya Watu wenye Ulemavu katika upatikanaji wa huduma mbalimbali. Serikali itaendelea na juhudi zake za kuwasaidia na kuwaendeleza Watu wenye Ulemavu kwa kuwapatia elimu, kuwajengea uwezo wa kujiajiri wenyewe na kuwapatia fursa ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Spika, utumiaji wa dawa za kulevya nchini ni hatari kwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu. Katika kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya nchini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Tume ya Taifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inaendelea kutoa taaluma kwa jamii kupitia vyombo vya habari (radio na TV) juu ya athari ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Vile vile taaluma hiyo inatolewa kwa wanafunzi na walimu wa skuli za serikali na binafsi kwa Unguja na Pemba. Aidha, serikali kupitia Tume imefanya ziara za kuonana na kujadiliana na Kamati za Ulinzi na Polisi Jamii kwa Shehia zilizoonekana kuathirika zaidi na biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika Mkoa wa Mjini Magharibi ili kupata njia bora zaidi za udhibiti wa dawa hizo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea na juhudi zake katika kupambana na uingizaji, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Natoa

wito kwa wananchi kuachana na tabia ya kuingiza na kutumia dawa za kulevya kwani kufanya hivyo ni kuliangamiza Taifa letu.

MASUALA YA MAZINGIRA

Mhe. Spika, ili tuweze kufanikiwa katika jitihada zetu za kukuza uchumi na kupunguza umaskini, suala la kutunza mazingira lina umuhimu mkubwa. Hali ya utunzaji wa mazingira katika visiwa vyetu si ya kuridhisha hasa katika udhibiti wa taka, uchimbaji mchanga na mawe, uharibifu wa matumbawe, uchafuzi wa fukwe, ukataji wa miti ovyo na ujenzi katika vianzio vya maji na njia kuu za umeme.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo kushajiisha upandaji miti, kufanya ukaguzi wa kimazingira na kuifanyia tathmini ya kimazingira miradi yote inayotekelezwa hapa nchini.

Mhe. Spika, natoa wito kwa jamii kuyatunza mazingira yetu pamoja na kushiriki kikamilifu katika programu mbali mbali zinazoandaliwa na serikali, Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo katika upandaji wa miti, utunzaji wa misitu ya asili, kutotupa taka ovyo, kutochimba mawe na mchanga pasi na kufuata taratibu zilizowekwa.

JINSIA NA WATOTO

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inazingatia uwiano bora wa kijinsia, serikali inaendelea kuchukua hatua mbali mbali ikiwemo uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango na Programu za Maendeleo. Aidha, serikali inachukua hatua za kuwajengea uwezo wanawake ili kuwawezesha kushiriki katika nafasi za utoaji wa maamuzi na utekelezaji wa miradi ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, watoto ni hazina kuu ya taifa, hivyo ili kuwa na taifa imara la kesho juhudi mbali mbali zinachukuliwa na serikali katika kuimarisha afya zao na kuwaendeleza kielimu. Vile vile serikali inachukua jitihada kubwa kuona haki za watoto zinalindwa na kuheshimiwa, miongoni mwa jitihada hizo ni kuanzisha Mahakama ya Watoto *(Juvenile Court)* ambayo tayari imeshaanza kazi. Pia serikali inaendelea kuimarisha vituo vya Mkono kwa Mkono ili kupambana na vitendo vyote vya udhalilishaji wa kijinsia nchini.

UTAWALA BORA

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa tayari imeanza matayarisho ya kuandaa Sheria ya Maadili ya Viongozi. Aidha, serikali imeshaandaa Rasimu ya Maadili ya Kitaifa ambayo yatapaswa kuzingatiwa na viongozi na wananchi wote katika nafasi zao za ngazi zote.

Mhe. Spika, serikali inaendelea kutoa mafunzo kwa watendaji kuhusu masuala ya kupambana na rushwa. Vile vile serikali inaendelea kuendesha midahalo ya Wanasheria kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, Jumuiya za Kiraia pamoja na Wataalamu na Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Zanzibar kwa lengo la kuitambua sheria ya rushwa na kusaidia kubainisha mianya ya rushwa nchini.

Mhe. Spika, Mfumo wa Mageuzi wa kiutendaji katika sekta ya umma unapitia katika mabadiliko makubwa ya utoaji wa huduma kwa kutumia mfumo wa mawasiliano na utunzaji wa taarifa kwa njia ya digitali. Kuzinduliwa rasmi kwa kituo kikuu cha serikali cha kuhifadhi taarifa za Kielektroniki hapo tarehe 5 Januari, 2013 ni hatua kubwa katika kuimarisha mawasiliano ya digitali katika taasisi za umma.

Kufuatia hatua hiyo, serikali imetayarisha rasimu ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao *(E-Government)* ambayo inatarajiwa kuwasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba ili kupata maoni yao hivi karibuni.

Mhe. Spika, sambamba na hatua hiyo, serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ili kuweza kutumia Mkonga wa Mawasiliano *(Optic fiber)* kwa kutoa huduma za kiserikali na za kibiashara. Hadi hivi sasa, serikali imeshafunga mkataba na kampuni ya Mawasiliano ya Simu, ZANTEL kuendesha matumizi ya mkonga huo.

MUELEKEO WA VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeweka muelekeo unaolenga kuchangia katika kufikiwa kwa dira na dhamira ya ofisi. Dira ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni kuwa na serikali yenye kutoa huduma bora kwa jamii na yenye muhimili mzuri wa uchumi na maendeleo endelevu, wakati dhamira yetu ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali katika sekta zote za SMZ na mambo ya Muungano kwa kufuata misingi ya Katiba, Sheria na Taratibu pamoja na kuhakikisha kufuata misingi ya haki za

binaadamu na ushirikishwaji. Hivyo, kwa mwaka 2013/2014 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais muelekeo wake ni kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- Kuwa na mfumo mzuri wa uratibu wa shughuli za serikali na masuala ya Muungano na utoaji wa taarifa za utekelezaji.

- Kuimarisha usimamizi na uratibu wa shughuli za utafiti nchini kwa kuzingatia mahitaji ya utekelezaji wa MKUZA II na mipango ya maendeleo.

- Kujenga uwezo wa kitaasisi katika sekta ya umma na sekta binafsi na jamii katika kukabiliana na maafa ili kupunguza wingi wa matukio ya maafa na athari zinazotokana na maafa hayo.

- Kuimarisha huduma za Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili ziwe bora, zenye ushindani kibiashara na kukidhi mahitaji ya serikali na jamii kwa jumla.

- Kuandaa sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar zenye hadhi na haiba na za aina ya pekee kulingana na umuhimu wa Mapinduzi kwa maendeleo ya taifa letu.

- Kuandaa mazingira mazuri ya kuendesha Kura ya Maoni ya kupitisha Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Kuandaa mazingira bora kwa ajili ya kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa 2015, ikiwemo kutoa elimu ya wapiga kura, kufanya mapitio ya majina, idadi na mipaka ya majimbo, kufanya mapitio ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kufanyia mapitio Sheria za Tume.

- Kuendesha mikutano ya Baraza la Wawakilishi na kusimamia kazi za Kamati za Kudumu za Baraza.

- Kujenga uwezo wa Watendaji na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2012/2013 NA MALENGO YALIYOPANGWA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na taasisi zake ilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 22,366,010,000.

Kati ya hizo Shilingi 17,214,186,000 kwa kazi za kawaida na Shilingi 5,151,824,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, ofisi iliingiziwa Shilingi 14,642,045,254 (sawa na asilimia 65). Kati ya hizo Shilingi 11,549,577,626 kwa kazi za kawaida (sawa na asilimia 67) na Shilingi 3,391,474,948 kwa kazi za maendeleo (sawa na asilimia 66). [Kiambatanisho Nam. 2A na 2B] kinajieleza.

Mhe. Spika, baada ya kutoa taarifa za jumla za utekelezaji wa kifedha kwa mwaka 2012/2013, sasa naomba kutoa taarifa za utekelezaji wa kila idara na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

OFISI YA FARAGHA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ina jukumu la kutoa huduma kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia Ofisi Kuu Zanzibar na ofisi zilizoko Pemba, Dar -es- Salaam na Dodoma.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/13, Ofisi ya Faragha iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 365,223,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2013, Ofisi ya Faragha iliingiziwa jumla ya Shilingi 270,634,098 sawa na asilimia 74.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho 2012/13 Ofisi ya Faragha imetekeleza mambo yafuatayo:

i Ofisi ya Faragha imeratibu vikao saba (7) vinavyohusiana na masuala ya Kisheria, Uchumi na migogoro ya kijamii.

ii. Ofisi imeratibu ziara 12 za ndani kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba na ziara mbili (2) kwa Tanzania Bara. Aidha, iliratibu ziara mbili (2) za nje ya nchi (Cuba na Umoja wa Falme za Kiarabu)

iii. Ofisi imetekeleza jumla ya ahadi 13 zilizohusu masuala mbali mbali ya kijamii.

iv. Wafanyakazi watatu wa Ofisi ya Faragha walilipiwa ada za masomo.

v. Ofisi imezifanyia matengenezo (service) gari tano zilizopo Unguja na mbili zilizopo Dar-es-Salaam.

vi. Ofisi imefanya matengenezo ya Makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ya Unguja pamoja na kufanya malipo ya huduma za maji na umeme kwa makaazi ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Faragha imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuimarisha kazi za Ofisi ya Faragha za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuzipatia ofisi zake zote nyenzo, vifaa na wafanyakazi wenye uwezo.

ii. Kusimamia utendaji wa Shughuli za Serikali kwa kufuatilia shughuli mbali mbali za utendaji katika mawizara.

iii. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuimarisha huduma za usafiri, ukarabati wa nyumba na upatikanaji wa vifaa mbali mbali.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Faragha iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 780,034,000 kati ya hizo Shilingi 521,741,000 ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 258,293,000 kwa ajili ya mishahara, posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*).

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kusimamia shughuli za uendeshaji na utawala pamoja na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/13 Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 866,184,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliingiziwa jumla ya Shilingi 659,123,270 sawa na
asilimia 76.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/13, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imetekeleza mambo yafuatayo:

i. Idara imeendelea kuwalipia ada na gharama za masomo wafanyakazi 65 (wanawake 31 na wanaume34)waliopo masomoni na kuwapatia wafanyakazi wote walioenda likizo stahiki zao. (Kiambatanisho Nam.3)

ii. Kujenga mazingira bora ya kazi kwa kununua vitendea kazi vikiwemo kompyuta saba (7), vifaa vya ofisi na samani.

iii. Kitengo cha Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali kimeboresha huduma za ghala na uwekaji wa kumbukumbu za ofisi na kusimamia shughuli za Bodi ya Zabuni.

iv. Idara imefanya uhakiki wa mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na kuandaa utaratibu wa tathmini ya utendaji kazi na upandaji vyeo kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

v. Idara imefanya semina ya siku tatu (3) kwa wafanyakazi 88 wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu Sheria za Utumishi wa Umma.

vi. Idara imeajiri wafanyakazi wapya 24 kwa mujibu wa mahitaji ya ofisi.

vii. Idara imewapatia wafanyakazi wa ofisi elimu ya msingi juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kujenga mazingira bora ya kazi kwa kununua vitendea kazi vya kisasa vikiwemo kompyuta saba (7), gari moja (1), vifaa vya ofisi na samani.

ii Kuendelea kuwalipia wafanyakazi 14 walioko masomoni ndani na nje ya nchi.

iii Kufanya warsha elekezi kuhusu sheria za utumishi pamoja na kuwapatia wafanyakazi elimu ya msingi juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI.

iv. Kutoa motisha kwa wafanyakazi kwa kuwapatia stahiki 27 zao ikiwemo malipo baada ya saa za kazi, sare kwa madereva, wahudumu na matarishi pamoja na kutoa zawadi kwa wafanyakazi bora.

v. Kuweka mfumo bora wa usimamizi na utoaji wa taarifa katika uwajibikaji kazini.

vi. Kuendelea kufanya uhakiki wa mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na kuandaa utaratibu wa tathmini ya utendaji

kazi na upandishaji vyeo kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 1,004,880,000. Kati ya hizo Sh. 378,081,000 ni kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 626,799,000 ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea na jukumu la kusimamia masuala ya mipango, bajeti, sera na utafiti. Pia idara hii ina jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kutayarisha ripoti za utekelezaji wa shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miezi mitatu, miezi sita, miezi tisa na mwaka mzima.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kutumia jumla ya Sh. 223,356,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Idara ilipatiwa jumla ya Sh.101,482,440 kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 45.

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 iliweza kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Idara imeendelea kulipa madeni ya ada na gharama za masomo kwa wafanyakazi wanne (4) waliomaliza masomo na kuwapatia stahiki zao wafanyakaz wawili (2) waliokwenda likizo.

ii. Idara imetoa mafunzo ya wiki moja kwa wafanyakazi11 wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya kuibua na kuandaa miradi ya maendeleo.

iii Idara imeandaa ripoti za utekelezaji kwa shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo kwa robo mwaka, nusu mwaka na miezi tisa. Pia imefanya vikao vya kupitia na kutathmini ripoti hizo.

iv. Jumla ya vibali 89 vya kufanya utafiti katika sekta za mazingira, historia, kilimo, maliasili, misitu na elimu vilitolewa. Aidha, Ofisi imeratibu vikao vinne; viwili vya

Kamati ya Taifa ya Utafiti na viwili kwa Kamati ya Wataalamu ya Kutafiti Rasilimali za Asili.

v. Idara kwa kushirikiana na *COSTECH* imetekeleza mambo yafuatayo:. Idara imeratibu Mafunzo ya kuibua vipaumbele vya utafiti ambayo Awamu ya Kwanza yalishirikisha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa 29 Rais, Tume ya Mipango na Ofisi ya Rais - Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Awamu ya Pili ilishirikisha maafisa utafiti wa Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Idara imeratibu uzinduzi wa Kongano *Cluster* tatu kwa Unguja na mbili kwa Pemba. Wanachama wa Kongano hizo walipatiwa Sh 8,000,000 kwa kila Kongano ili kuendeleza miradi yao.

Idara imeratibu semina ya siku moja iliyowashirikisha Makatibu Wakuu wa SMZ kuhusu majukumu ya *COSTECH*, masuala ya Kongano na umuhimu wa utafiti katika kuandaa mipango na sera za Kitaifa. . *COSTECH* imeendelea kulipa gharama za masomo ya muda mrefu kwa wanafunzi tisa (9) (wanaume 4 na wanawake 5) wa Zanzibar katika vyuo mbali mbali Tanzania Bara.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha mazingira ya kazi na uendeshaji wa Ofisi kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na kulipa maslahi ya wafanyakazi.
ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa miradi/program za maendeleo na Bajeti.
iii. Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera, mipango na miradi/program za maendeleo.
iv. Kutayarisha taarifa za utekelezaji za kazi za kawaida na miradi ya maendeleo na kuandaa mikutano ya kutathmini taarifa za utekelezaji.
v. Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuandaa mikutano na makongamano kuhusu masuala ya utafiti.
vi. Kuratibu vikao vya Kamati ya Taifa ya Utafiti na Kamati ya Wataalamu ya Kutafiti Rasilimali za Asili.
vii. Kwa kushirikiana na *COSTECH* kuvijengea uwezo vitengo vya utafiti vya Wizara za SMZ.
viii. Kuwapatia mafunzo ya kitaalamu wafanyakazi tisa (9) wa Idara kwa mujibu wa majukumu na kazi zao.

ix. Kuratibu utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI (*Global Fund*).

Mhe. Spika, Ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2013/2014 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 295,240,000 kwa matumizi ya Idara. Kati ya hizo Sh. 67,879,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa *ZSSF* na Sh. 227,361,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ina jukumu la kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za Muungano ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Uratibu ilipangiwa kutumia jumla ya Sh. 346,377,000 kwa 31 . Matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi, 2013, Idara iliingiziwa Sh. 199,640,550 sawa na asilimia 58. Aidha, Idara iliidhinishiwa Sh. 840,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa SMZ. Kati ya hizo Sh. 80,000,000 ni kwa Mradi wa TASAF na Sh. 760,000,000 kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Hadi kufikia Machi, 2013, Idara imeingiziwa Sh. 18,350,000 kwa mradi wa *TASAF*, sawa na asilimia 23 na Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo haukuingiziwa fedha katika kipindi cha miezi tisa (9).

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Idara imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Idara imeratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015 katika Wizara za SMZ na Mikoa yote ya Unguja na Pemba na kuandaa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha miaka miwili (Oktoba 2010 – Septemba 2012) na jumla ya nakala 3,500 zilichapishwa na kusambazwa.

ii. Idara imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kukusanya na kuandaa taarifa za utekelezaji Maafisa Viungo wa Wizara, Maafisa Mipango wa Mikoa pamoja na Waratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

iii. Idara imepokea na kuratibu jumlaya malalamiko 54 ya wananchi yaliyowasilishwa (Ardhi 7, Ajira 20, Masomo 11, Hali ngumu ya maisha 16). Kati ya hayo malalamiko 15 yamepatiwa ufumbuzi, malalamiko 39 yanaendelea

kushughulikiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ushirikiano na Wizara nyengine za Serikali.

iv. Idara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Viongozi 32 Wakuu wa Kitaifa zilizotolewa kwa ushirikiano na Wizara za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na taasisi nyengine za Serikali.

v. Idara imefuatilia mikutano minne (4) ya Baraza la Wawakilishi na mikutano minne (4) ya Bunge. Katika vikao hivyo hoja, ripoti na ushauri uliotolewa vimeratibiwa ipasavyo na kuwasilishwa Serikalini.

vi. Idara imeratibu vikao tisa (9) vya Kamati ya Taifa ya Sensa ya Watu na Makaazi iliyofanyika mwezi Agosti, 2012 na matokeo yake kutangazwa tarehe 31, Disemba 2012 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.vii. Idara imeratibu jumla ya vikao vinane (8) vya kujadili changamoto za Muungano. Kati ya hivyo, vikao vinne (4) vya Sekretarieti, vikao viwili (2) vya Makatibu Wakuu na Vikao viwili (2) vya Mawaziri.

viii. Idara imeratibu kikao kimoja (1) cha Kamati ya Pamoja ya Mambo ya Muungano baina ya Mheshimwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

ix. Idara imeratibu vikao tisa (9) vya kisekta kwa ushirikiano kati ya Wizara za SMZ na SMT kwa taasisi zisizo za Muungano.

x. Idara imeendelea kulipia ada na gharama nyengine za mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wanne (4) na mafunzo ya muda mfupi kwa mfanyakazi mmoja (1).

xi. Idara imesimamia utekelezaji wa miradi 39 ya maendeleo ya jamii –*TASAF* II. Pia, Idara imeandaa 33 na kuratibu warshaya siku mbili ya kujenga uelewe kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wa *TASAF* III iliyofanyika tarehe 22 – 23 Januari, 2013, Zanzibar (Kiambatanisho Nam. 4A na 4B).

xii. Idara imeratibu ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano kwa lengo la kuangalia utendaji wa Taasisi za Muungano na utekelezaji wa miradi ya Muungano iliopo Zanzibar. Taasisi zilizohusika na ziara hiyo ni Taasisi ya Sayansi ya Bahari, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Vitambulisho (*NIDA*) na Jeshi la Polisi. Miradi iliyotembelewa ni Mradi wa *TASAF* na Programu ya Kusaidi Huduma za Sekta ya Kilimo *Agricultural Services*

Support Programme–ASSP katika Wizara ya Kilimo na Maliasili.

xiii. Idara inaendelea na ukaguzi wa marejesho ya fedha za miradi midogo midogo ya wananchi na matayarisho ya Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

xiv. Idara imeimarisha Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Elimu (ICE) cha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kukipatia wataalamu wawili (2) wa masuala ya ICT.

xv. Idara imenunua vifaa vya kutendea kazi na imelipa stahiki kwa wafanyakazi waliokwenda likizo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha mazingira ya kazi na uendeshaji wa ofisi kwa kulipia stahiki za wafanyakazi na kununua vifaa vya kuendeshea kazi.

ii. Kuimarisha huduma za usafiri kwa kununua gari moja (1) kwa kazi za Idara.

iii Kuratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015.

iv. Kuwajengea uwezo wakitaalamu katika masuala ya uratibu wafanyakazi wa Idara, Maafisa viungo wa Wizara za SMZ na Maafisa mipango wa Wilaya na Mikoa.

v. Kuendelea kuwalipia ada za masomo wafanyakazi wanne (4) wanaoendelea na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.

vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za viongozi Wakuu wa Kitaifa.

vii. Kuratibu malalamiko ya wananchi yanayowasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

viii. Kuratibu vikao vya Baraza la Wawakilishi.

ix. Kuratibu utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na kufuatilia utekelezaji wa miradi iliyokwishapatiwa fedha.

x. Kuratibu vikao vya mashirikiano kati ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

xi. Kuratibu vikao vya Mawaziri, Makatibu Wakuu na Sekreterieti ya Kamati ya Pamoja ya Mambo ya Muungano.

xii. Kuratibu vikao vya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mhe. Waziri Mkuu chini ya uenyekiti wa Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujadili hoja za Muungano.

xiii. Kuratibu utekelezaji wa miradi ya Muungano inayotekelezwa Zanzibar pamoja na utekelezaji wa mradi wa TASAF.

xiv. Kuimarisha shughuli za Habari, Mawasilianao na Elimu. Mhe. Spika, Ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2013/2014 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 397,530,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Sh. 177,299,000 zitatumika kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Sh. 220,231,000 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa miradi ya maendeleo naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 840,000,000, kati ya hizo Sh. 760,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Sh. 80,000,000 ni mchango wa Serikali kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Jamii – *TASAF*.

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuratibu masuala ya maafa hapa Zanzibar, kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Kukabiliana na Maafa Nam. 2 ya mwaka 2003.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Kukabiliana na Maafa ilipangiwa kutumiajumla ya Sh. 210,674,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Idara imeingiziwajumla ya Sh. 124,811,070 ambazo ni sawa na asilimia 59. Aidha, Idara ilipangiwa kutumia Sh. 50,000,000 kwa kazi za maendeleo kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2013 Idara imeingiziwa jumla ya Sh. 20,000,000 sawa na asilimia 40. Aidha, Shirika la Mipango ya Maendeleo 36 la Umoja wa Mataifa *UNDP* liliahidi kutoa Sh. 624,000,000, na hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Shirika hilo limechangia jumla ya Sh.535, 160,000 sawa na asilimia 86. Aidha, *UNICEF* imechangia jumla ya Sh. 182,280,000.

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 iliweza kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

i. Idara imetayarisha Sheria mpya ya Kukabiliana na Maafa na inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014.
ii. Idara imetoa huduma wakati wa operesheni ya uokozi katika ajali ya kuzama kwa meli ya MV. Skagit mwezi Agosti mwaka 2012.
iii Idara imefanya matengenezo ya mitambo na redio za mawasiliano.
iv. Idara imetayarisha na kurusha vipindi 18 vya kukabiliana na maafa kwa lengo la kuelimisha jamii kupitia *ZBC* Radio.
v. Kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Idara iliandaa na kufanya jaribio la mezani la kukabiliana na maafa kwa lengo la kupima uwezo wa taasisi husika katika kukabiliana na maafa na kuzifanyia majaribio utekelezaji wa Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa *Emergency Preparedness and Response Plan*–

EPRP na Mkakati wa Mawasiliano wakati wa Maafa *Disaster Communication Strategy–DCS*.

vi. Kufanya tathmini kwa shehia 60 za Wilaya za Mjini, Magharibi na Kaskazini 'A' Unguja ili kujua hali, uwezo na mahitaji ya shehia 37 katika kukabiliana na maafa (Kiambatanisho Nam. 5A na 5B).

vii. Kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa shehia 14 kati ya shehia 60 zilizofanyiwa tathmini kwa Wilaya za Magharibi na Kaskazini 'A'. Mafunzo kama hayo tayari yameshatolewa katika Shehia 33 za Wilaya ya Wete na Micheweni katika mwaka wa fedha 2011/2012.

viii. Idara imeendelea kuwalipia gharama za mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wanne (4) na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wawili (2).

ix. Kununua vitendea kazi muhimu vya ofisi na kulipa maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i Kukamilisha Sheria mpya ya Kukabiliana na Maafa.

ii. Kununua vifaa mbali mbali vya kukabiliana na maafa, ikiwemo gari, vifaa vya mawasiliano, kompyuta na pikipiki.

iii. Kufanya matengenezo ya mitambo na redio za mawasiliano ziliopo kisiwani Pemba.

iv. Kutayarisha vipindi 48 vya kuelimisha jamii kuhusiana na masuala ya kukabiliana na maafa kupitia Radio na *TV*.

v. Kuendelea kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa na kuanzisha Kamati za Kukabiliana na Maafa kwa Shehia 50 (Unguja 30 na Pemba 20).

vi. Kuandaa majaribio ya kukabiliana na maafa *simulation exercises*.

vii. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi wanane (8) wa Idara.

viii. Kuandaa Jarida la kila robo mwaka la Tukabiliane na Maafa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

ix. Kukusanya taarifa zitakazotumika katika kuainisha maeneo hatarishkwa majanga mbalimbali (*Disaster Mapping and Profile*).

x. Kuendesha mikutano miwili (2) ya wadau wa maafa (*Disaster Sub national Platform)*.

Mhe. Spika, ili Idara ya Kukabiliana na Maafa iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 262,528,000 kwa matumizi ya Idara. Kati ya hizo Sh.101,557,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara,

posho za wafanyakazi na mchango wa ZSSF na Sh.160,971,000 kwa matumizi mengineyo.

Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 70,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo, ikiwa ni mchango wa Serikali. Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo *UNDP* limeahidi kutoa Dola za Kimarekani 300,000 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *UNICEF* limeahidi kutoa Dola za Kimarekani 130,000.

IDARAYA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe. Spika, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na shughuli za Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yanayosimamiwa na Idara hii ni pamoja na Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Pia, Idara inaratibu Hitma na Dua ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume (*Karume Day*).

Mhe. Spika, Katika kipindi cha 2012/2013, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ilipangiwa kutumia jumla ya Sh. 868,375,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara iliingiziwa Sh. 639,034,010 ikiwa ni sawa na asilimia 74.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Idara imeratibu kwa mafanikio maadhimisho ya Sherehe za kutimiza miaka 49 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
ii. Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu kwa mafanikio Sherehe za miaka 51 ya Uhuru wa Tanganyika na Sherehe za miaka 49 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zilizofanyika Kitaifa Dar es Salaam.
iii Idara imeratibu Hitma ya Maadhimisho ya Siku ya Karume (*Karume Day*) tarehe7 Aprili, 2013.
iv. Idara imeendelea na marekebisho ya Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa Nam.10 ya Mwaka 2002.
v. Idara imeshiriki katika uratibu wa Sala na Mabaraza ya Idd el Fitri na Idd el Hajj.
vi. Wafanyakazi wawili (2) wa Idara wamepatiwa mafunzo, mmoja (1) mafunzo ya muda mrefu na mmoja (1) mafunzo ya muda mfupi.
vii. Idara imenunua vifaa vya ofisi na vifaa vya sherehe kwa awamu ya kwanza ya kiwemo mashamiana 18.
viii. Idara imelipa stahiki kwa wafanyakazi wane (4)waliokwenda likizo.

ix. Idara imeendelea kukusanya taarifa na kumbukumbu za marehemu Mzee Abeid Amani Karume kwa ajili ya kuhifadhi na hatua za kufanikisha azma ya kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu za Mzee Abeid Amani Karume.

x. Idara kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania imeendelea na kulifanyia matengenezo kaburi la Marehemu Dkt. Omar Ali Juma.

Mhe. Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Taasisi mbalimbali na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha maadhimisho ya Sherehe za miaka 49 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Aidha nachukua nafasi hii pia kuipongeza kwa dhati Halmashauri ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa kazi nzuri ya kufanikisha sherehe hizo zilizofanyika tarehe 12 Januari 2013.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha mazingira ya kazi na uendeshaji wa ofisi, ikiwemo kununua vifaa vya sherehe, vifaa vya kufanyia kazi, na kulipa stahiki za wafanyakazi.

ii. Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wawili (2) na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi watatu (3).

iii Kuandaa na kusimamia maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na Sherehe za Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

iv. Kuandaa na kusimamia Dua ya kumuombea Marehemu Mzee Abeid Amani Karume (*Karume day*).

v. Kuendelea na kazi za kukusanya taarifa kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu za Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

vi. Kulienzi Kaburi la Marehemu Mzee Idris Abdulwakil kwa kulijengea uzio na kituo cha mapokezi.

Mhe. Spika, Ili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 2,189,103,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Sh. 65,452,000 kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na Sh. 2,123,651,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

IDARA YA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ina majukumu ya kuchapisha Miswada ya Sheria, Magazeti Rasmi na Nyaraka zote za Serikali,

pamoja na kuuza vifaa vya kuandikia kwa Taasisi zote za Serikali na watu binafsi.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya Sh. 512,555,000 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2013, Idara imeingiziwa jumla ya Sh.348, 695,378 sawa na asilimia 68 ya makadirio. Aidha, Idara katika mwaka huo wa fedha 2012/2013 iliidhinishiwa Sh. 3,032,400,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2013, Idara imeingiziwa Sh. 2,212,540,948 sawa na asilimia 73.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Idara imeendelea kulipia gharama za mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanane (8) katika ngazi ya Cheti na Diploma ya Uzamili.
ii. Idara imenunua vifaa vya uchapishaji vikiwemo karatasi, wino, madawa, "*plates*" na filamu.
iii. Idara imefanya upembuzi yakinifu *feasibility study* wa mahitaji ya vifaa vya kuandikia kwa Wizara na Taasisi za Serikali.
iv. Idara inaendelea na taratibu za kukamilisha Mpango Mkuu wa Biashara (*Business Plan*) kwa ajili ya Kiwanda na Bohari Kuu.
v. Idara imeendelea kuimarisha shughuli za upigaji chapa ikiwemo mpango wake wa kukihamisha Kiwanda cha Upigaji Chapa kutoka Saateni kwenda Maruhubi. Katika mpango huo jengo la Kiwanda lililopo Maruhubi limefanyiwa ukarabati mkubwa na mashine mpya za dijitali zimenunuliwa.
vi. Idara inaendelea kulipa stahiki na madeni ya wafanyakazi pamoja na kununua vitendea kazi vya ofisi.
vii. Idara imechangia jumla ya Sh. 118,827,200 katika Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 50 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha mazingira ya kazi na uendeshaji wa ofisi ikiwemo kununua vitendea kazi, kulipa stahiki za wafanyakazi na kununua gari kwa ajili ya usafiri wa wafanyakazi.
ii. Kuendelea kuwalipia gharama za masomo ya muda mrefu wafanyakazi wanane (8) waliopo masomoni.
iii. Kufunga mitambo ya dijitali ya uchapishaji na kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa mitambo hiyo.
iv. Kuchapisha Miswada yote ya Serikali itakayowasilishwa Baraza la Wawakilishi.

v. Kukamilisha na kutekeleza Mpango wa Biashara wa Kiwanda na Bohari Kuu *Business Plan* pamoja na Mkakati wa kupanua soko la huduma za Kiwanda *Marketing Strategy*.

Mhe. Spika, ili Idara iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 546,868,000. Kati ya hizo Sh. 282,022,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, posho na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *ZSSF* na Sh. 264,846,000 kwa matumizi mengineyo.

Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Sh. 2,500,000,000 kwa kazi za maendeleo. Kati y a h i z o Sh. 1,000,000,000 kuendelea na ukarabati wa jengo la kiwanda na Ofisi na Sh.1,500,000,000 kwa ununuzi wa mitambo mipya ya uchapishaji. Kwa upande wa mapato Idara imekadiriwa kuchangia jumla ya Sh. 500,000,000.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba ina jukumu la kuratibu shughuli za Idara zote zilizo chini ya Ofisi hii kwa upande wa Pemba. Hivyo, utekelezaji wa Ofisi hii ni kama ilivyokwishaelezwa katika Idara mbali mbali za Ofisi.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2012/2013, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 357,256,000 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2013, Ofisi iliingiziwa jumla ya Sh. 213,557,607 sawa na asilimia 60.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba itaendelea na kazi za uratibu wa kazi zote za Idara mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa upande wa Pemba. Ili kuweza kutekeleza kazi za uratibu wa shughuli hizo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 452,817,000. Kati ya fedha hizo, Sh. 199,417,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Sh. 253,400,000 kwa matumizi mengineyo.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Ibara ya 119 (1) na Sheria Nam 9, 1992 ya Tume ya Uchaguzi ili kuendeleza demokrasia kwa njia ya uchaguzi. Tume ina majukumu yafuatayo:-

i. Usimamizi mzima wa mienendo ya jumla katika Uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.
ii. Kukuza na kuratibu elimu ya wapiga kura.
iii. Kusimamia ukataji wa mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi Zanzibar.
iv. Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
v. Usimamizi wa Kura ya Maoni.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Sh. 1,084,000,000 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Tume iliingiziwa jumla ya Sh. 788,591,395kiasi hicho ni sawa na asilimia 73 ya makisio.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Tume imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Katika kuliendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Tume ilitoa elimu ya wapiga kura kupitia vyombo vya habari pamoja na mikutano ya wadau mbalimbali katika ngazi ya shehia (Kiambatanisho Nam. 6). Aidha, mitambo ya uandikishaji ya wapiga kura ilifanyiwa matengenezo.
ii. Matengenezo ya Majengo ya Ofisi za Tume za Wilaya ya Mjini na Kati, Makao Makuu ya Tume Unguja na Ghala la Tume lililoko Micheweni Pemba.
iii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) (wanawake wawili na wanaume wawili) na muda mfupi wafanyakazi watano (5) (wanawake wawili na wanaume watatu).
iv. Katika hatua za matayarisho ya kupitia mipaka, majina na idadi ya majimbo ya uchaguzi, Tume imewasiliana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Wadau wakuu wa Uchaguzi.
v. Kuifanyia mapitio Sheria ya Uchaguzi Nam. 11, 1984.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Tume ya Uchaguzi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuanza maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.
ii. Kupitia mipaka, majina na idadi ya majimbo ya uchaguzi ya Zanzibar.
iii. Kuendesha Kura ya Maoni 2014 kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

iv. Kuimarisha huduma za Ofisi ili kuweka mazingira bora ya utendaji kazi ikiwemo ununuzi wa samani na utoaji wa mafunzo kwa wafanyakazi.

Mhe. Spika, ili Tume ya Uchaguzi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh.987,000,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Sh. 514,000,000 kwa matumizi ya malipo ya mshahara na posho za wafanyakazi na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Sh. 473,000,000 zitatumika kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 4,694,000,000 kwa kazi za maendeleo.

OFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar limeundwa kwa maelekezo ya Kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na majukumu yake ya msingi yanatajwa kwenye kifungu cha 88 cha Katiba ambayo ni kama yafuatayo:-

i. Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo.
ii. Kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa Bajeti katika Baraza la Wawakilishi.
iii. Kuuliza maswali mbalimbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi.
iv. Kuidhinisha na kusimamia mipango ya maendeleo ya Serikali katika njia ile ile ambayo Bajeti ya Mwaka inaidhinishwa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Sh. 12,380,186,000 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Baraza liliingiziwa Sh. 8,204,007,808 sawa na asilimia 66. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo Baraza liliidhinishiwa matumizi ya Sh. 605,424,000 na hadi Machi, 2013 Baraza liliingiziwa Sh. 605,424,000 sawa na asilimia 100.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza liliweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Baraza limeweza kufanya mikutano yote minne ya kawaida, ambayo ni mkutano wa Nane (Julai 2012), Mkutano wa Tisa (Oktoba 2012), mkutano wa Kumi (Januari 2013) na mkutano wa Kumi na Moja (Aprili 2013).
ii. Jumla ya Miswada 16 ya Sheria ilijadiliwa na kupitishwa na Baraza (Kiambatanisho Nam. 7).

iii. Jumla ya Maswali ya Msingi 382 yaliulizwa na kujibiwa katika mikutano hiyo (kuanzia Julai 2012 hadi Juni 2013).

iv. Baraza liliendelea kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kupitia Kamati zake za Kudumu kama zilivyopangwa, na hatimae kuwasilisha ripoti zake kwenye Baraza katika Mkutano wa Kumi na Moja wa mwezi Aprili, 2013. Pia Kamati ziliendelea kufanya kazi zake hizo mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi wa Mei 2013 (Kiambatanisho Nam. 8).

v. Baraza la Wawakilishi liliunda Kamati Teule mbili (2) ambazo ni Kamati iliyopewa kazi ya kuchunguza madai ya kuwepo ukiukwaji wa majukumu ya Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na kuwasilisha Ripoti yake Barazani katika Mkutano wa Kumi (mwezi wa Januari 2013) na Kamati ya Kufuatilia migogoro ya ardhi ambayo bado inaendelea na kazi zake.

vi. Baraza lilipokea Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Baraza la Manispaa, Zanzibar ambayo iliwasilishwa kwenye Mkutano wa Tisa wa Baraza (Oktoba, 2012). Katika Mkutano huo Baraza lilipokea Taarifa ya Serikali juu ya Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza iliyoundwa tarehe 9 Agosti, 2011 kwa ajili ya kuchunguza mambo mbali mbali yaliyojitokeza kwenye Mkutano wa Nne wa Bajeti ya mwaka 2011/2012. Vile vile, Katika Mkutano wa Kumi (Januari, 2013) Baraza lilipokea Taarifa ya Serikali iliyohusu Ripoti ya Utendaji wa Baraza la Manispaa Zanzibar.

vii. Katika kujenga uwezo kwa Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza ili kuongeza ufanisi wa kutekeleza majukumu ya kazi zao, Baraza limewawezesha Wajumbe kuhudhuria ziara za kimafunzo nje ya Nchi kama ifuatavyo:-

- Wajumbe sita na Maafisa wawili walihudhuria mafunzo nchini Uganda.
- Wajumbe sita na Afisa mmoja walikwenda Zambia
- Wajumbe sita na Afisa mmoja walikwenda India
- Wajumbe saba na Maafisa watatu walikwenda Ghana

viii. Aidha, jumla ya wafanyakazi 26 wa Ofisi ya Baraza wameendelea kupata mafunzo ya fani mbali mbali katika viwango tofauti kuanzia Cheti, Diploma, Shahada ya Kwanza hadi Shahada ya Uzamivu (*PhD*.). Kwa kupitia

ufadhili wa Mradi wa Elimu ya Katiba na Mradi wa Kusaidia Vyombo vya Kutunga Sheria (*Legislature Support Project*), Waheshimiwa Wajumbe na wafanyakazi wamepata mafunzo kupitia semina mbali mbali zilizoendeshwa.

ix. Katika kuimarisha uhusiano wa Kimataifa, Baraza liliendelea kushiriki kwenye mikutano ya Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola, iliyofanyika Uganda na Nigeria na Mkutano wa Jumuiya ya Kamati ya PAC wa nchi za SADC uliofanyika nchini Uingereza.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2012/2013 lilipata bahati ya kutembelewa na wageni mbalimbali mashuhuri wa ndani na nje ya Tanzania. Miongoni mwao ni:-

i. Balozi wa DRC nchini Tanzania
ii. Balozi wa UAE nchini Tanzania
iii. Balozi wa Oman nchini Tanzania
iv. Naibu Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa
v. Balozi wa Norway nchini Tanzania
vi. Balozi wa Uingereza nchini Tanzania
vii. Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba
viii. Balozi wa Finland nchini Tanzania

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Baraza la Wawakilishi limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya mikutano ya Kawaida minne, pamoja na kuendelea na kazi za Kamati za Kudumu zilizopo na kazi ya Kamati Teule ambayo haijamaliza kazi zake.
ii. Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wa Baraza pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na ziara za mafunzo Wajumbe wa Baraza.
iii. Kuendeleza uhusiano wa kimataifa na wa kikanda baina ya Baraza na vyombo vyengine vya Kutunga Sheria na Jumuiya za Mabunge ya Jumuiya ya Madola.
iv. Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Shughuli za Baraza la Wawakilishi.
v. Kuendelea kuyafanyia matengenezo majengo ya Ofisi kwa Unguja na Pemba.
vi. Kununua vifaa na zana za kazi ili kuweza kutekeleza majukumu na uendeshaji wa Ofisi.

vii. Kuendelea kuweka mazingira bora ya Ofisi ili kutoa huduma bora kwa Wajumbe.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Baraza iweze kutekeleza malengo hayo kwa ufanisi, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 14,852,000,000 kwa matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo Sh. 7,911,951,000 ni kwa ajili ya mishahara, stahiki nyengine na mchango wa ZSSF kwa wajumbe na wafanyakazi wa Baraza na Sh. 6,940,049,000 kwa matumizi mengineyo.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Dola za Kimarekani 435,960 ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo.

UKUSANYAJI MAPATO

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 544,400,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

i.	Idara ya Mpiga chapa Mkuu wa Serikali	Sh.500,000,000
ii.	Idara ya Uendeshaji na Utumishi (Kodi ya ukumbi wa mikutano wa BLW wa zamani)	Sh. 38,400,000
iii.	Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa (Kodi ya milango ya duka na mashamiana)	Sh. 6,000,000
	Jumla	**Sh. 544,400,000**

Mhe. Spika, muhtasari wa makadirio ya fedha kwa kazi za kawaida na za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama unavyoonekana katika Kiambatanisho Nam. 9A na 9B.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, naomba kumshukuru kwa dhati Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa uongozi wake wa hekima na busara ambao siku zote umekuwa dira yetu katika kutekeleza majukumu ya ofisi hii ya kuwatumikia wananchi. Aidha, amekuwa mfano kwa maneno na vitendo katika kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunampongeza sana. Nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi zao katika kutekeleza majukumu waliyopangiwa.

Mhe. Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa mashirikiano, maelekezo, ushauri na michango ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa yaliyopelekea utayarishaji wa hotuba hii. Aidha, napenda kuwashukuru sana Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*) na nchi marafiki katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Ofisi yetu na ya nchi kwa jumla katika mwaka wa fedha 2012/2013. Miongoni mwao ni: AL-Yousef Foundation, Benki ya Dunia, Clinton Foundation, China, FAO, Finland, Norway Jumuia ya Afrika ya Mashariki, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI (Global Fund), Oman, UNAIDS, USAID, UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP, FAO, na WIPO. Vile vile, naishukuru sana Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wao wa karibu sana na Ofisi yetu. Pia nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali kama ZAYEDESA, Jumuia ya Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia Serikali katika kutoa huduma za jamii na kuiletea maendeleo nchi yetu.

Aidha, nawashukuru wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza hotuba yetu hii.

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia naomba sana nimshukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi

Aidha, shukrani za pekee ziwaendee familia yangu kwa msaada mkubwa sana wanaonipa katika kushirikiana kwenye kutekeleza majukumu ya Taifa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya
Sh. 21,768,000,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake (Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawakilishi) kwa matumizi ya kazi za kawaida na Sh. 13,105,036,000 kwa kazi za maendeleo (Kiambatanisho Nam. 8A na 8B).

Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

Kazi za Kawaida

i. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	Sh.5,929,000,000
ii. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar	Sh.987,000,000
iii. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	Sh.14,852,000,000
Jumla	**Sh. 21,768,000,000**

Kazi za Maendeleo

i.	Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa	Sh. 779,500,000
ii.	Mradi wa Ununuzi wa Mashine Mpya	Sh. 1,500,000,000
iii.	Mradi wa Ukarabati wa Majengo wa Kiwanda	Sh.1,000,000,000
iv.	Mradi wa TASAF III	Sh. 80,000,000
v.	Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (ZCDF)	Sh. 760,000,000
	Jumla ndogo	**Sh. 4,119,500,000**

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar

i.	Mapitio ya Mipaka ya Majimbo	Sh. 80,000,000
ii.	Kuendesha Kura ya Maoni (SMT)	Sh. 4,394,000,000
iii.	Kufanya Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu 2015	Sh. 220,000,000
iv.	Democratic Empowerment Project (DEP)	Sh.3,594,000,000
	Jumla ndogo (Tume)	**Sh. 8,288,000,000**

Ofisi ya Baraza la Wawakilishi

i.	Mradi wa Kuwezesha BLW (LSP)	**Sh. 697,536,000**

Jumla Kuu **Sh. 13,105,036,000**

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa niaba ya kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati, kwanza kwako wewe kwa kuweza kutupa nafasi hii ya kuweza kuwa watu wa mwanzo kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais.

Mhe. Spika, pongezi zetu nyengine vile vile tunaomba tuzipeleke maalum kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini vile vile na Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kutumia busara kubwa katika kutuongoza kwa uadilifu mkubwa pamoja na tofauti zao za kisiasa na tofauti zetu kisiasa, lakini wao wametuonesha mfano wa mashirikiano na sisi naomba wenzangu tuige

mifano yao ili kuwajenga na kuwaunganisha wananchi wetu bila ya kujali tofauti zao za kisiasa.

Mhe. Spika, na sisi kama kamati tunatoa mkono wa pole kwa familia na wananchi wa jimbo la Chambani, kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chambani Mhe Salum Hemed Khamis, tunamuomba M/Mungu amlaze mahali pema peponi Amin. Pia tunawaomba wananchi wa Chambani wawe na subra na kwa kuwa tayari wameshampata Mbunge mwengine ili waweze kushirikiana naye katika kuleta maendeleo.

Mhe. Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati pia napenda kumshukuru Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wa Ofisi hii kwa utendaji mzuri wa kazi zao ambao unaipelekea Kamati yetu kuweza kutekeleza majukumu ya kazi zake za kila siku kwa ufanisi mzuri. Hata hivyo, napenda kuishukuru Ofisi hii kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu bajeti ya wizara yao kwa mwaka 2013/2014 kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Spika, aidha nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwanza kwa kunichagua kwa mara nyengine tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, lakini pia kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa mda wote nilipokuwa nje ya nchi kwa kuichambua na kuijadili bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa ushirikiano wa pamoja na moyo wa dhati katika kutekeleza majukumu yao, pia shukurani maalum kwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati yangu Mhe Saleh Nassor Juma kwa uwezo aliounesha wa kuiongoza kamati yetu katika mazingira magumu ya ugeni wa kamati hiyo na kuweza kuwaongoza wajumbe wangu wa kamati hii ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Hivyo, namshukuru sana kwa hilo, sasa kwa ruhsa yako Mhe Spika, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:-

1.	Mhe Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Saleh Nassor Juma	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Mzee Ali	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5.	Mhe.Shadya Mohammed Suleiman	Mjumbe
6.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
7.	Mhe. Subeit Khamis Faki	Mjumbe
8.	Ndg.Rahma Kombo Mgeni	Katibu
9.	Ndg.Makame Salim Ali	Katibu

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba kutoa maoni ya Kamati kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa bajeti hii ya mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, pamoja na Mhe Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais napenda kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuikubali kwa pamoja na kuipitisha Bajeti kuu ya Serikali, lakini bado napenda kuijulisha Serikali kuwa watekeleze yale tunayoyapitisha na sio wachague wanayoyataka wao, kwani bado maamuzi ya Baraza lako tukufu kuhusu maslahi ya watumishi wa Baraza kama yalivyopitishwa na Tume ya Utumishi wa Baraza Serikali hamtaki kuyatekeleza jambo ambalo hata wewe mwenyewe Mhe Spika, huridhiki nalo japo kuwa unanyamaza kimya huku chombo chako hiki kinanyang'anywa mamlaka yake na baadhi ya watu Serikalini, kwa hiyo naomba suala hili Serikali iliangalie kwa makini katika Bajeti ya Baraza la Wawakilishi inapitia mikononi mwako, sitegemei hata wewe mwenyewe Mhe Waziri kuwa utakubali fungu unalolipitisha kwenye bajeti yako lisitekelezwe.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imepewa majukumu ya kusimamia idara nyeti ambazo ni muhimu ndani ya nchi yetu ikiwemo Tume ya Uchaguzi, Idara ya Upigaji Chapa, Idara ya Maafa, Baraza la Wawakilishi na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali lakini viel vile na Idara ya Kuratibu Shughuli za Muungano, ambazo zote zina majukumu makubwa ya kuhakikisha utekelezaji wa majukumu hayo unafanywa kiufanisi, kwa lengo la kukamilisha dhima iliyopewa na nchi kwa maendeleo ya nchi na wananchi wake.

IDARA YA MAAFA:

Mhe. Spika, Kwa upande wa Idara ya Maafa: Kamati yangu inathamini sana jitihada zinazochukuliwa na Serikali kupitia Idara hii kama tunavyojua ni Idara nyeti na muhimu ndani ya nchi yetu ambayo ni tegemezi kwa wananchi pindi yanapotokea maafa. Aidha, Kamati yetu inapongeza jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Ofisi ya Makamo wa Pili kupitia idara ya Maaafa kwa kutoa elimu kwa wananchi kupitia shehia mbali mbali Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, mbali na jitihada kubwa zinazochukuliwa na idara hiyo, kamati imeona ni vyema kwa Idara hii kuongezewa fedha katika fungu la maafa katika bajeti ya Serikali lakutosheleza, ili iweze kujiendesha vizuri na kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa vile hadi sasa Idara hii inakabiliwa na uhaba wa fedha za kuendeshea shughuli za maafa zinapotokezea, hali ambayo ni changamoto kubwa sana kwa nchi yetu, kwa vile suala la maafa si

kitu cha kukisiwa kwani hayajulikani yatakapotokezea yataathiri vipi. Ndio maana kamati yangu kila mara tunazidi kuishauri serikali yetu kuanzisha mfuko wa maafa ili kutoa nafasi kwa watu binafsi ,wafanya biashara, mashirika, na hata taasisi za kimataifa kuweza kuuchangia mfuko huo kama mataifa mengine yanavyofanya pamoja na wenzetu Tanzania Bara ambao wanao mfuko huo, na tuondokane na utaratibu uliopo hivi sasa wa kuwa yanapotokea maafa watu kukusanyika kwenye ofisi ya Makamo wa Pili na kutoa misaada, kwa hiyo waziri akija atusaidie Serikali imefikia wapi katika kuanzisha mfuko huo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, Vile vile Kamati inaona ni vyema Serikali ikaharakisha kuanzisha ujenzi wa jengo la Idara ya maafa ili kuwa na jengo litalokidhi mahitaji pamoja na kuwa na ghala la kuhifadhia vitu vyao kwa Unguja na Pemba.
Mhe. Spika, Kamati pia imeona kuna umuhimu mkubwa wa kuviwezesha vikosi vyetu ambavyo tunavitumia pindi maafa yanapotokezea kwa kuvipatia vifaa vya kutosha ambavyo vitawezesha kusaidia wakati majanga yanapotokea. Hii ni kuonekana mapungufu yaliyojitokeza katika maafa yaliyotokea ambapo tatizo kubwa kwa waokoaji lilikua pia kukosekana kwa vifaa vya kuokolea ambapo wangeweza kuvitumia na kusaidia ndugu na jamaa zetu waliopotea.

IDARA YA UPIGAJI CHAPA:

Mhe. Spika, Kwa upande wa Idara hii Kamati yangu inapenda kuipongeza Serikali kwa jitihada wanayoionesha ya kuwapatia jengo jengine la Ofisi ya Upigaji Chapa ambalo litakua faraja kwa watendaji wa idara hii, kwani miaka mingi waliteseka kwa kufanya kazi katika mazingira yasiyoridhisha. Hata hivyo, mbali na kupatiwa jengo ambalo liko njiani kuhamiwa lakini bado kamati imeona kuna haja ya Idara ya Upigaji Chapa kupatiwa vitendea kazi bora pamoja na kuboreshwa maslahi ya wafanyakazi wake kutokana na kazi ngumu wanayoifanya. Vile vile kuhakikisha mafundi wanapangiwa kazi kwa mujibu wa kada zao na pia kuwapa mafunzo ya kisasa ili kumudu vifaa vipya vitakavyokuja ambavyo tunategemea kuwa vitakuwa vya kisasa kabisa.

Mhe. Spika, naomba niungane na waziri katika hutuba yake kuzungumzia hali ya kisiasa. Mhe Spika, tunaungana na waziri kuwaomba wananchi kuendelea kuilinda na kuidumisha hali ya amani na utulivu iliyopo jambo ambalo ni msingi wa maendeleo yetu, pamoja na vitendo vichache vya uvunjifu wa amani vinavyotokezea bado tunaviomba vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea kufanya kazi ya kuwatafuta wanaojihusisha na vitendo hivyo ambavyo havitusaidii hasa kwa wakati huu, ambao hata viongozi wa kambi

mbili kubwa za kisiasa tayari wameshaondoa tofauti zao za kisiasa na wanafanya kazi kwa pamoja ndani ya Serikali na huu ndio uungwana.

Pia Waziri katika hutuba yake ametuelezea masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao mwakani unafikia umri wa miaka 50, kama alivyoeleza waziri Muungano bado ni muhimu kwetu kisiasa na kiuchumi, kwa hiyo kwa kuwa tumepata nafasi ya kujadili Katiba mpya hivi sasa nawaomba wananchi wote huu ndio wakati muhimu wa kusema wanataka watawaliwe vipi, kwani fursa hii tukiitumia vibaya na kuweka ushabiki wa mvutano wa kisiasa ambao hautamsaidia mtu yeyote au chama chochote unaweza kutupeleka pabaya, kwani katiba hii sio ya chama chochote na kwa msingi huo yeyote atakayechaguliwa kuongoza nchi hii hata ikitokezea mgombea binafsi ataongoza kwa katiba hii mpya tutakayoiamua, kwa hiyo pamoja na maslahi ya vyama vyetu, lakini ni muhimu kuijua na kuilinda misingi ya nchi yetu kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ameelezea hali ya uchumi na kusema kuwa pato la mwananchi limekua kutoka 960,000 (617.usd) kwa mwaka hadi 1,003,000 (638.usd), lakini bado kipato hiki ni kidogo sana kulingana na mahitaji ya kila siku. Kwa hiyo kama nilivyoshauri kwenye hutuba yangu ya kamati ya wenyeviti, mimi naishauri serikali wakati umefika kwa serikali yetu kuweka vipaumbele ambavyo vitachangia moja kwa moja pato la taifa pamoja na mapato ya ndani.

Mhe. Spika, kipaumbele cha mwanzo nnachoshauri ni kukamilisha *master plan*, na kuweka miundombinu kwenye maeneo huru ya kiuchumi, ili hao wawekezaji tunaowashawishi kuja basi watukute kuwa tumeshaandaa hayo maeneo ya uwekezaji.

Pili serikali ndani ya mwaka mmoja ujao kama wameshindwa kupata aidha mkopo au fedha kwa njia yeyote, basi watafute wawekezaji kwa njia ya *PPP* ambao wapo na wako tayari kuja kuwekeza kwenye ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri na hilo ndilo litakuwa lango kuu la uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa kwanza nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Waziri wa Fedha na Uchimi kwa taarifa yake aliyoitoa kabla sijaandaa hotuba hii, kwa kuona kwamba serikali tayari yale ambayo mambo tuliyoyapendekeza kuhusu ujenzi wa bandari ya Mpigaduri tayari serikali imeyafanyia kazi na tunawapongeza sana kwa hilo Mhe. Spika.

Tatu kuanza taratibu za utafiti wa rasilimali zote zilizopo hapa Zanzibar, ikiwemo ,gesi, mafuta na madini yaliopo Zanzibar.

Nne kutafuta wawekezaji wa ujenzi wa miradi wa nyumba za mikopo ya muda mrefu, ambapo pia wameshajitokeza na kuonesha nia ya kuwekeza katika miradi hiyo ya (*Real estates*). Kutokana na hali hiyo, wananchi watapata makaazi bora na ya kisasa pamoja na ajira kwa majengo ya biashara yatakayojengwa kupitia miradi hiyo.

Mhe. Spika, naamini vipaumbele hivi nilivyoshauri au tulivyoshauri kama kamati, kama kweli serikali inakusudia kuongeza pato la taifa na la mwananchi wa kawaida na kuinua hali ya maisha ya wananchi wetu itavipa umuhimu wa pekee, ili kuisaidia nchi kujikwamua katika hali ngumu iliyopo sasa.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe Makamo wa Pili wa Rais ni kiongozi wa jopo la mawaziri wanaoshiriki Vikao vya Kero za Muungano, bado kuna mapato mengi ambayo yaliyotajwa kwenye Katiba ya Muungano lakini hayaletwi Zanzibar, jambo ambalo linasababisha serikali kuendelea kuwakamua wananchi wakati kuna vianzio halali ambavyo kila siku tunapiga kelele, na hilo ni miongoni mwa mambo yanayochangia wananchi kuhisi kuwa muungano unawabana. Kwa hiyo, tunaomba sana Mhe. Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na jopo lake aweze kutusaidia katika kuainisha vianzio hivyo na fedha hizo ziweze kuingia serikalini. Mhe. Spika, ni wajibu wa serikali kuyashughulikia hayo na ndio matakwa ya wananchi waliotuchagua.

TUME YA UCHAGUZI

Mhe. Spika, kwa upande wa Tume ya Uchaguzi, kamati yangu imeridhishwa na jitihada zinazochukuliwa na Tume ya Uchaguzi, katika kuratibu masuala yake ikiwemo suala la kuendesha chaguzi mbali mbali za nchi. Vile vile kamati yangu inaitaka Tume ya Uchaguzi kuandaa utaratibu wa utoaji wa elimu ya uraia hasa katika kipindi hichi kilichobaki kabla ya kuanza Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na pia elimu ya upigaji kura na watu kujua haki zao, ili waweze kufanya maamuzi sahihi wakati shughuli za kijamii na za kitaifa zikiendelea.

Pia kamati inaishauri serikali kupitia Tume ya Uchaguzi kulipa umuhimu suala la kuliboresha Daftari la Kupigia Kura, ambapo hivi sasa tunashukuru kazi hiyo tume imeshaianza na tunawapongeza sana.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la watu katika nchi pamoja na kuweza kuwaondoa waliokosa sifa za kuwemo kwenye daftari, ili waweze kupatiwa fursa wenye sifa ambao wameshafikia umri wa kuandikishwa na kuepuka

kuwakosesha haki zao za msingi kama raia. Tunashukuru kwa kuwa kazi hiyo tayari inaendelea kwa ufanisi mkubwa.

Hata hivyo, kamati inashauri suala la ushirikishwaji kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa mambo yanayohusu Muungano Tume ipatiwe fursa hiyo, kwani itasaidia kuondoa baadhi ya kero zinazolalamikiwa na wananchi kuhusiana na chaguzi na mambo mengine. Lakini pia kamati inashauri kutolewa elimu kwa wananchi kuanzia sasa kuhusiana na kura ya maoni ili waweze kuitumia fursa yao kiukamilifu na kuachana na dhana potofu zilizopo kwa baadhi ya jamii.

Pamoja na hayo kamati yangu haijaridhishwa na kitendo cha Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano (*NEC*) kwa kuandaa na kuikamilisha Rasimu ya Kura ya Maoni ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania bila ya kushauriana tangu mwanzo Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*), matokeo yake inaweza kuwaletea kitu ambacho kimeshakamilika na kuwataka watoe maoni yao. Hili Mhe. Spika, sio jambo zuri katika kuweka mustakbali mzuri wa mahusiano yetu katika Muungano wetu.

Mhe. Spika, kwa kuwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar haikupata mashirikiano ya kutosha katika suala la utoaji maoni yanayohusu marekebisho ya Sheria ya Kura ya Maoni yanayohusu Katiba mpya, hata hivyo baada ya kudai wakaletewa dakika za mwisho kutoa mapendekezo yao. Lakini mbali na hilo tume pia imeeleza kwa mujibu wa sheria hiyo haitakuwa na fursa ya kutoa matokeo hata ya majimbo kwa hapa Zanzibar jambo ambalo hata wananchi wengi wanalilalamikia, ila wao wametakiwa kushiriki katika uendeshaji wa Kura ya Maoni na matokeo ya kura yakatangazwe moja kwa moja na *NEC*.

Hivyo, kamati inaitaka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kulifuatilia suala hili na kuhakikisha linatatuka, ili kuepuka mzozo usije kujitokeza baadaye na kuvuruga malengo ya kura ya maoni na tume kupewa ruhusa ya kutangaza kura kwenye vituo.

Vile vile, suala la uingizwaji wa fedha kwa upande wa Tume ya Uchaguzi kamati inaomba liwe kwa muda muafaka hasa kwa wakati huu, ili kuepuka kukwama kwa shughuli walizojipangia kuzitekeleza kwa wakati.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe. Spika, Idara hii ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kazi kubwa wanayofanya bado tunaitaka kuhakikisha inajenga jengo la kumbukumbu ya kuwaenzi viongozi wa kitaifa, kwani hakuna taifa lisilokuwa na historia. Leo ni aibu mtu akija kutaka aoneshwe kumbukumbu ya viongozi

na walioikomboa nchi yetu pamoja na vifaa vilivyotumika kukomboa nchi yetu hatuwezi kumuonesha, sijui tatizo ni nini wakati sheria tayari tumeshatunga. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka nikuambie katika ziara yetu ya China kimoja ya kitu tulichojifunza kuwa kila jambo wanalolifanya wanaweka kumbukumbu, hata viwanda vyao ambavyo vinazalisha mali vinaekewa makumbusho ambapo zaidi ya miaka 1,000 utakuta kumbukumbu ipo.

Vile vile sisi tulikiona mpaka sehemu ambayo aliyokuwa akilala mfalme wa mwanzo wa China zaidi ya miaka 800 iliyopita, isitoshe tumeweza kuoneshwa mpaka silaha za mwanzo zilizotumika katika Mapinduzi ya China pamoja na nguo, visu, mishare, mizinga na viatu vilivyotumika kwenye mapinduzi hayo.

Mhe Spika, waziri aje kutueleza kwa kua lile eneo la Mwera ambalo ni shamba la Marehemu mzee Karume, pahala ambapo ndipo palipotakiwa kujengwa jengo la kumbukumbu ya muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na kiongozi wa Zanzibar, lakini hadi leo suala hilo bado hakujawa na mipango madhubuti ya kujenga eneo hilo.

Pia mwakani tunaadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi, tumeshindwa kuendeleza ujenzi wa makaazi bora ya wananchi, ambayo aliyaanzisha muasisi wa Mapinduzi yetu ya Zanzibar. Jengine pia ni aibu kuwa hata maji yanatushinda kuwapatia hasa katika eneo la Mkoa wa Mjini Magharibi kama nilivyoeleza katika hotuba yangu na kwenye Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati nitakuja kueleza Mhe. Spika, hayo ndiyo yalikuwa matunda na Mapinduzi ya Zanzibar.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Spika, kamati haina budi kuipongeza Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo shughuli za uendeshaji wa vikao na kamati zake. Hata hivyo, kamati inasisitiza suala la kuanzishwa kwa Sheria ya Utawala wa Baraza, ili kulifanya Baraza kuwa huru katika kutekeleza majukumu yake kama Katiba inavyoelezea.

Pia tunakuomba sana Mhe Spika, wewe mwenyewe kwani tayari kuna mswada binafsi, ambao umeuzuia katika ofisi yako, na kwa kuwa tayari ule utafiti ulioagiza ufanyike tayari wenyeviti wako tumeshafanya kazi kubwa ya utafiti huo, na sasa naomba kikao kijacho uturuhusu kuuleta mswada huo ili na sisi tufanye kazi kama Mabunge ya Jumuia ya Madola yanavyofanya shughuli zao. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri katika utafiti huo hata na wewe mwenyewe Mhe Spika ulishiriki kikamilifu. Mhe Spika, leo tumeona choyo sana jinsi mabunge ya wenzetu yalivyokuwa huru kufanya kazi zao za kisimamia serikali tofauti na sisi tunasimamiwa na serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati inaitaka Wizara ya Fedha kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha uingizwaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa vikao na mambo mengine uwe kama ulivyopitishwa katika bajeti, ili kutuwezesha kuisimamia vyema serikali na si kucheleweshwa, kwani ucheleweshaji wa fedha hizo unapelekea kukwamisha utendaji wa shughuli zetu za Baraza. Mhe. Spika, tunamshukuru Mhe. Waziri katika hotuba yake ameeleza kwamba katika bajeti ya mwaka huu nadhani fungu letu limetekelezwa kikamilifu na tunakushukuruni sana kwa hilo. *(Makofi)*

Pia Mhe Spika, tunaiagiza Ofisi ya Baraza kuendelea na ukarabati wa maeneo muhimu ndani ya Baraza letu ikiwemo vyoo na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa upande wa miradi ya *TASAF*, kamati inapongeza jitihada za serikali wanazozifanya katika kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kwa kuwapatia miradi inayowasaidia kuweza kupambana na umaskini. Hata hivyo, kamati imebaini kukwama kwa miradi mingi ya *TASAF* na kufa njiani kunatokana na ukosefu wa soko na taaluma ya uendeshaji miradi.

Lakini kama nilivyoelezea katika hotuba yangu ya bajeti ya serikali, kwamba miongoni mwa sababu zilizopelekea miradi hiyo kufa, ni mipango mibovu ya serikali kushindwa kuwalinda wananchi wake hasa katika miradi inayotoa ajira kwa watu wake.

Kwa kweli serikali kuruhusu wafanyabiashara kuingiza kuku kutoka Brazil na kuuzwa kwa bei ya kutupwa hapa nchi imepunguza zaidi ya ajira 3,000, ajira ambayo wananchi wetu ilikuwa ikiwasaidia kuweza kujazia pengo la kipato chao, ili kuweza kusomesha watoto wao, kupata makazi yao na mahitaji mengine. Suala hili nitahitaji maelezo ya kutosha hasa kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha ambayo ndio watozaji wa kodi.

Lakini pia naomba serikali ifanye tathmini ni hasara gani walioipata wananchi. Aidha misaada au mikopo kupitia mifuko mbali mbali ambayo imekufa ni hasara kwa miradi ya ufugaji wa kuku baada ya kuruhusu uingizwaji kuku wa (*PEDUU*).

Mhe. Spika, serikali kama itashindwa kulinda ajira za ndani kwa wananchi wake, basi hizo jitihada zote za kuwawezesha wananchi kiuchumi zitakuwa ni

nyimbo tu. Kwa hiyo, ni lazima kuweka masharti maalum kwa wawekezaji wote wanaokuja kuwekeza Zanzibar na pia kuweka vikwazo maalum kwa uingizwaji wa bidhaa ambazo zinazalishwa hapa Zanzibar.

Vile vile kama nilivyoelezea kwenye Ripoti ya Kamati ya Wenyeviti kuwa ni lazima tubadilishe mitaala yetu, ili kuwaandaa wanafunzi kuweza kujiajiri wenyewe mara tu wanapomaliza masomo au kuja kushika nafasi za ajira kwa makampuni au viwanda vitakavyokuja kuwekeza hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, pia miradi mingi ya *TASAF* imekuwa ikikabiliwa na matatizo ya mara kwa mara na hatimaye kufa kabisa kutoka na kutopata ushirikiano endelevu wa uendeshaji miradi hiyo. Hali hii hutokea mara tu baada ya wahusika wa *TASAF* kukabidhi fedha za mradi kwa vikundi na kuwapatia elimu ya awali huwaacha wanakikundi kuundeleza miradi yao wenyewe, ambapo mara nyingi hujikuta wakipata hasara badala ya faida au kufa kabisa kwa mradi hiyo.

Hivyo, kamati inashauri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja wizara nyengine zinazohusika kwa namna moja au nyengine katika kuvisaidia vikundi vya miradi ya *TASAF* kielimu na kutowaacha mkono wanavikundi mara baada ya kukabidhiwa miradi, ili serikali iweze kufikia malengo iliyoyakusudia la kuwakwamua wananchi kiuchumi na badala yake isiwe kupoteza fedha ambazo zingefaa kutumika kwa mambo mengine ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, wizara ihakikishe inawapatia wananchi ushauri wa kuchagua miradi ambayo itakua na faida na si kupatiwa fedha za kuendeshea miradi, ambayo haitakuwa na faida kwao na kuishia kufa kwa mradi hiyo bila kupatikana mafanikio.

Mhe. Spika, kuhusu huduma za jamii, kwa kuwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ndio inayoratibu shughuli zote na kuripoti kwa chama kinachotawala, basi tunawaeleza kuwa bado Wawakilishi haturidhiki na utendaji wa Mamlaka ya Maji hapa Zanzibar hasa Mkoa wa Mjini Magharibi, kwani serikali imetumia fedha nyingi sana kuondoa tatizo la maji, lakini bado tatizo lipo.

Hata hiyo, hivi juzi Waziri wa Fedha ametuomba tuidhinishe nyingine karibu 55 bilioni, lakini imekuwa ni sawa kutia maji pakachani, kwani suala hili ni zito, linagusa maisha ya watu wengi na linaongeza kasi ya umasikini, kwani wananchi wanatumia pesa nyingi kununulia maji, kwa magari au madumu. Tunaitaka serikali kumaliza tatizo hili mara moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika masuala mtambuka, hasa yanayohusu watu wenye ulemavu tunaishukuru serikali kwa jitihada wanazozichukua kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu, lakini mkazo zaidi uwekwe katika kutafuta vifaa vya kusomea. Kwa mfano, kompyuta maalum kwa wasioona, fimbo za kutembelea na elimu ya ufundi kwa vijana wenye ulemavu, ili waweze kujitegemea, lakini bado serikali hawajatekeleza sera ya watu wenye ulemavu hasa katika kupewa upendeleo maalum kwa ajira kwa watu wenye ulemavu, labda waziri anayeshughulikia masuala ya utumishi wa umma kwenye hotuba yake ya bajeti aje atuelezee ni asilimia ngapi wameajiriwa serikalini kupitia ajira tuzilizozipitisha mwaka uliopita hapa Barazani mwaka uliopita.

Mhe. Spika, waziri ametueleza jitihada zinazochukuliwa na serikali kuhusu kuzuia kuingizwa na utumiaji wa dawa za kulevya hapa Zanzibar. Suala hili bado imekuwa nyimbo ya siku zote, kwani kama tutashindwa kupiga vita suala la rushwa basi dawa za kulevya zitaendelea kuletwa hapa nchini, kwani tumepitisha sheria nzuri hapa ya kumfilisi mali yake pamoja na kutaifisha hata nyumba inayotumika kuuza dawa ya kulevya, lakini tujiulize jee hakuna aliyekamatwa na dawa hizo hadi leo? Mhe. Spika, naiomba serikali iwajibike kisawa sawa vyenginevyo taifa litaangamia kwa kuwa na vijana wasiokuwa na akili kutokana na kutumia madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, masuala ya mazingira bado ni jambo sugu kwani hata miradi mikubwa ya serikali mingi yao haifanyiwi tathmini ya mazingira kabla ya ujenzi jambo ambalo limo ndani ya sheria. Sasa ikiwa taasisi za serikali zinakiuka sheria je, tutegemee nini kwa wananchi wetu hawa wa kawada? Kwa hivyo, na wao pia watavunja sheria. Kutokana na hali hiyo, tunaomba taasisi zilizokabidhiwa masuala ya kulinda mazingira zitekeleze wajibu wao kwa vitendo.

Mhe. Spika, suala utawala bora tunaomba serikali itekeleze kwa vitendo maamuzi ya Baraza lako tukufu, kwani tunapitisha maamuzi na maazimio mengi tena makubwa na serikali imekuwa na kigugumizi katika kuyatekeleza, jambo ambalo linawafanya wabadhirifu kuendelea kujiamini katika kutafuna mali za umma bila woga. Hivyo, hapa tunaitaka serikali kupitia kwako Mhe. Spika, itekeleze maamuzi halali yanayotolewa na Baraza lako tukufu, ili kuweza kuleta uadilifu ndani ya serikali yetu.

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunasikitishwa sana na Serikali yetu yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa kuenedelea kuwafumbia macho wahujumu wa uchumi wanaovujisha mapato ya kuendesha nchi badala yake wanakuja na mipango ya kuwakamua wananchi waliotafuniwa pesa zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hili kamati yangu itaendelea kuiambia serikali iache tabia ya kujificha kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa, badala yake kuwa serikali ya watu kulindana, jambo ambalo wananchi wamekuwa wakitulaumu sana na kutuona hatuna maana yeyote, kwani tumeshindwa kuilazimisha serikali kuwajibika katika kuwachukulia hatua wale wanaofanya ubadhirifu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuwa wewe ndiye uliyekabidhiwa dhima ya kusimamia shughuli zote za serikali, basi tuone utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa hasa kwa wale waliofanya hujuma ya fedha za umma katika mashirika mbali mbali ikiwemo Shirika la Umeme, kwani fedha hizo bado ni fedha za wananchi, ambazo zingeliweza kuondoa tatizo la madawati, madawa, maji, umeme na huduma nyingine muhimu kwa jamii.

Mhe. Spika, serikali ijue ina deni kubwa la Kamati za Baraza, kama vile Baraza la Manispaa, Shirika la Umeme, pamoja na ile ya mwanzo tumepoteza pesa nyingi za umma lakini hatujapata taarifa zinazoridhisha. Kutokana na hali hiyo, tunamuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, achukua hatua na tunaamini anaweza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naamini kama kutakuwa na makongamano ya kutathmini Mapinduzi ya Zanzibar, basi moja litakalotawala maoni ya wananchi ni kutoridhika kwao na jinsi waliopewa dhamana ya kuendeleza malengo ya mapinduzi kuiibia serikali, jambo ambalo angelikuwepo mwenyewe mzee Karume basi pasingelitosha, kwani hayo yalikuwa sio malengo yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati pia inamuomba sana Makamo wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, aache kuwafumbia macho, huhali na aanze kuchukua hatua mara moja kwa yeyote atakayefanya ubadhirifu wa mali ya umma. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, kamati yangu inashauri bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuongezwa katika fungu lake kutokana na majukumu makubwa, ambayo yanawakabili ya kuendesha na kuratibu shughuli zote za serikali, ambapo kwa sasa kutokana na bajeti walonayo tumeona sisi kama kamati inakuwa ni vigumu kuweza kutekeleza majukumu yao waliyokabidhiwa na wananchi.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza hotuba kwa niaba ya kamati sasa naomba nizungumze kidogo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura niweze kutoa maoni yangu binafsi. *(Makofi)*

Katika suala zima la mazingira, tunamuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, kutusaidia sana katika suala zima la mazingira. Kamati yangu Mhe. Spika inashughulika na masuala ya mazingira pamoja na kwamba wako katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, lakini Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais ni mratibu wa shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, bado tatizo la ujengaji wa mahoteli katika maeneo ya fukwe zetu ambao wanakiuka ile Sheria ya Ardhi ya kujenga mita 30 kutoka fukwe za bahari. *(Makofi)*

Kwa kweli suala hili tumeshasema sana na ujenzi bado unaendelea na taasisi zilizokabidhiwa majukumu zipo, sababu eti wanasema sheria. Mhe. Spika, mimi najiuliza swali moja, kama wewe umesema sababu sheria, mbona sheria zipo nyingi na Sheria ya Ardhi ipo kama Sheria ya Mazingira haiwezi kwenda kuwazuia wale, basi watumie Sheria ya Ardhi ambayo inawabana wawekezaji kujenga mpaka kwenye maeneo ya fukwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi sasa ninavyozungumza tayari kuna hoteli katika maeneo ya kusini na ujenzi ndio kwanza umeanza tayari wameshaiuka hiyo sheria ambayo tunaizungumza kila siku. Kwa hivyo, suala hili namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, aweze kumsimamia Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya mazingira kuhakikisha kwamba kufuatilia katika kila eneo ambayo anahisi mazingira yanaharibiwa.

Jambo jengine Mhe. Spika, naomba sana katika Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi. Mhe. Spika, tunaiomba sana serikali yetu iandae utaratibu miezi sita kabla ya sherehe za mapinduzi kuwe na programs maalum ambazo zitakuwa zinatoa elimu kwa wananchi wetu wa Zanzibar kujua historia na malengo ya mapinduzi yao. Vile vile kuangalia yale malengo kwa sababu malengo ya mapinduzi yaliandikwa pia tuwape wananchi fursa ya kuweka makongamano ya kutathmini je yale malengo ya mapinduzi waliyolenga viongozi wetu tumefikia asilimia ngapi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kimoja ambacho nimejifunza kwa wenzetu nchi ya China ni nchi ambayo ina watu wengi sana. Lakini katika nchi ambayo ina mipango madhubuti na mipango yao wanapanga kwa muda fulani. Kwa mfano, unapokabidhiwa jukumu kwa muda fulani na unapofika muda fulani kama halijakamilika hata mradi wowote wa serikali kama umekabidhiwa kuanzia mwaka fulani mpaka mwaka fulani kama haujakamilika, basi lazima kuwe kuna sababu ya msingi.

Mhe. Spika, kitu ambacho leo hakipendezi kwamba kuna miradi mingi ambayo inasimamiwa na serikali inakwama njiani ambayo bajeti yake inakuwa ndani ya mwaka mmoja na miradi inachukua zaidi ya miaka mitatu

au minne. Kwa kweli suala hili kwa malengo ya mapinduzi kuharakisha maendeleo hili linaturejesha nyuma sana.

Jengine Mhe. Spika, pamoja kwamba Mhe. Waziri wa Fedha kuhusu suala la makaazi. Jambo hili ni Sera ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu mwenyewe muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar mara tu baada ya mapinduzi aliweza kujenga nyumba bora za kisasa. Sasa serikali tumeacha kujenga nyumba na tunaachia wananchi wajenge wao wenyewe kutokana na hali ya kipato. Pato la taifa Mhe. Waziri ameshaeleza kwamba pato la mtu kwa mwaka ni shilingi 960,000 hivi ni mwananchi gani atayeweza kujenga nyumba ya kukaa.

Lakini sasa ni vyema tutumie Mifuko yetu ya Hifadhi na mimi nafikiri Mhe. Waziri wa Fedha kama alivyotwambia kwamba atakuja kutueleza lakini bado tuyatumie mashirika ya Kimataifa, ambayo yenye uwezo wa kifedha kuja kujenga Nyumba za Mikopo Nafuu za muda mrefu na kuweza kuondoa malalamiko ya wananchi. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nataka nizungumzie suala ambalo nimeliona jana. Mhe. Spika, nilikuwa nikiangalia taarifa ya habari *TBC*, nilimuona Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya nishati anatia saini mkataba wa kuanzisha Kiwanda cha Umeme wa kutumia gesi wa *megawatts* 400, ambacho kiwanda hicho kitajengwa katika eneo la Mtwara.

Mhe. Spika, naomba viongozi wetu kupitia kwako Mhe. Spika, watusaidie mpaka hivi sasa kwenye Katiba bado gesi ni suala la Muungano, pamoja na mapendekezo ya Zanzibar kuondoa suala la gesi na mafuta katika mambo ya Muungano, lakini mpaka hivi sasa bado halijaondolewa kwenye Katiba na linaendelea kutekelezwa.

Kwa hivyo, mimi nadhani kama kuna tafiti zinaendelea kufanyika, basi tafiti hizo zifanyike kwa pande zote mbili za Muungano, ili na Zanzibar kwa sababu kila tunapokwenda Mhe. Spika, maisha yanakimbia, umri unapotea lakini rasilimali bado inatusubiri. Kwa kweli fursa kama ile sasa kiwanda kile ambacho kinajengwa kitatoa *megawatts* 400, Zanzibar tunatumia *megawatts* 45 na hivi sasa tunaelekea 50. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nafikiri kama utafiti na Zanzibar ungekuwa unaanza, basi mimi naamini bado tunayo gesi ya kutosha hapa ambayo ya kuweza kuwekeza katika eneo zila la kiwanda cha umeme, ambao utaweza kupunguza makali ya maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, moja katika eneo ambalo hili pato la taifa pamoja na la mwananchi, nimeshaona Mhe. Spika kwamba muda unakaribia namalizia. Sasa katika eneo ambalo linaumiza sana kipato cha wananchi ni bili ya umeme Mhe. Spika na kama wenyewe Shirika la Umeme walivyotwambia kwamba hichi kiwango walichofikia hivi sasa bado wanategemea wataweza kuongeza tena.

Kutokana na hali hiyo, naomba Mhe. Spika viongozi wetu wanapokwenda kwenye vikao hivi hasa vya kushughulikia mambo ya Muungano, basi *at least* haya mambo mengine ya utafiti yanayofanyika na hapa kwa upande wetu wa Zanzibar yaweze kufanyika.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nataka nikushukuru wewe mwenyewe binafsi, wajumbe wa kamati yangu, Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wa wizara. Lakini kama alivyoeleza Mhe. Waziri na mimi nataka niwapongeze kwa dhati wake zangu kwa kuweza kunipa faraja pamoja na *support* katika kuwatumikia wananchi. Vile vile na kutumia muda mwingi kutokuwa karibu na familia kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.*)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, tunakushukuru sana kwa uwasilishaji wako huo, labda nimuulize swali tu, sasa wale wajane wamshukuru nani! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kuna tangazo moja dogo kwa Waheshimiwa Wajumbe wanawake, kwamba Mwenyekiti wa UWAWAZA anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe, kuwa yale mafunzo yao yatakuwa yanaendelea kwa wakati na pahala ambapo huwa wanafanyia shughuli hizo za mafunzo.

Baada ya tangazo hilo niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe hao wahudhurie mafunzo hayo.

Vile vile nakumbushwa kwamba ile khitma ya mwenzetu ya mama yetu mwenzetu Mhe. Amina Iddi Mabrouk itakuwa leo *Alaasiri* pale pale alipoondokea maiti kwa upande wa wanawake, na wakati wa *Isha* kwa upande wa wanaume Msikiti aliosaliwa maiti *Masjid Noor Muhammad*.

Baada ya hayo, Waheshimiwa Wajumbe, sasa niakhirishe kikao hichi hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe habari za jioni. Nimekuta hapa orodha ya watu wasiopungua 11 na wengine bado wangali wanaendelea. Tunachokiomba kila mjumbe ajitahidi kutumia dakika zake 20 bila ya kuzidisha. Lakini pia kila mjumbe ajitahidi yale ambayo mwenzake amekwisha kuyazungumza yeye aendelee kuyazungumza mengine. Kazi hii inatakiwa kufanyika baina ya leo na Jumatatu mpaka mchana ili jioni tuweze kufanya majumuisho. Ahsanteni.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hii. Lakini kwanza kabla ya sijachangia niweze kusema niliwahi kusema jambo ambalo kwa mujibu nilivyosomeshwa mimi na mwalimu wangu Mkuu; Mwanasheria, Katiba ya Zanzibar na naomba ninukuu kifungu hicho halafu baadae niweze kupata ridhaa ya kuweza kuchangia.

Kutokana na *paragraph* ya mwanzo inasema kuwa leo ni siku ambayo hotuba ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar ndio tunataka kupitisha. Lakini ndani ya Katiba hii kutakuwa na Makamo wa Pili na Makamo wa Kwanza. Sasa naomba nimuuliza Mhe. Waziri labda ni uchapaji tu imerukishwa au vipi hapa kwenye “u” badala kuwa “o”, naomba sana aniwekee vizuri *hansard*.

Mhe. Mwenyekiti, Kikatiba itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Katiba hii. Mimi naomba humu kuna Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar lakini kwenye kitabu inaeleza ni Makamo, hili suala nimelizungumza na naomba nilizungumze tena kwa sababu tunakwenda kwa mujibu wa sheria na tunaingia katika sehemu ya sheria. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hii uje unisahihishe kabla ya kutokuiunga mkono baadae lakini wache nichangie kwa jumla jumla halafu baadae tutakuja kusawazishana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kitabu chenyewe, kwenye ukurasa wa 7 suala linahusiana na mambo ya muungano. Naomba hapa niombe kuna suala niweze kulizungumza na ni suala ambalo huwa linasikitisha sana kwa Wazanzibari na ni wajibu wake mtu yeyote anayejisikia unyonge wajibu kusikitika. Wajibu wa kwanza kusikitika, wajibu wa pili kusema, kama hukusema unakuwa unatenda dhambi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa dakika 20 utatuonea tutekeleze Kanuni zetu dakika 30 katika kuchangia hilo, mheshimiwa utatuonea sana tunaomba kwa hilo utusamehe.

Mhe. Mwenyekiti, leo ameeleza hapa suala la gesi asilia na limo kwenye Katiba na sheria inasema wazi kuwa Katiba isikiukwe, isivunjwe lakini leo tangu wenzetu waanze kuchimba gesi asilia namuomba sana Mhe. Waziri atupe takwimu kwamba tumenufaika kwa kiasi gani kupata fedha za wenzetu waliochimba gesi asilia. Nimeangalia sana katika kitabu hichi naona sijaona maeneo ambayo yanaonyesha kwamba tumepata mafao hayo ya gesi asilia.

Lakini nataka nikwambieni wananchi wenzetu pamoja na Waheshimiwa katika rasimu hii inaonesha kwamba haya masuala yanataka kutolewa. Je, tukitolewa yale mafao yetu ya nyuma tutayapata au hatuyapati? Hapa nataka tuwe makini sana na ni lazima hapa tutulie kikweli kweli, tusing'ang'anie kwanza kwamba watoke wakati huko nyuma tayari wenzetu wameshachimba wana ma-*trilioni* ya fedha sasa hivi na hatujazipata.

Mimi naomba sana Mhe. Makamu wa Pili kuunda Tume si vibaya kuunda kijichumba chako kidogo cha kufuatilia haya mabakaa yaliyobakia. Tupeleke huko tukachukue pesa zetu za gesi asilia, wala usione tabu mheshimiwa ni haki yetu kwa mujibu wa Katiba wala watu wasifikiria ni maneno tu, ni maneno ya Katiba Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo naomba sana tuwe na tahadhari sana, tutaliondoa lakini mabaki yetu tupewe wenyewe tujenge nchi yetu ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria ya ndani ya Katiba yetu inavyoeleza. Kwa sababu bado sasa hivi halijapita hilo suala la kuendelea bado limo, wenzetu tayari wameshaendelea kuchimba. Mhe. Mwenyekiti, kasema leo tayari wenzetu wanatumia umeme wa *megawatt 4000,* sisi ndio kwanza hatujaanza kufanya shughuli hiyo. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili suala lazima lifikiriwe kwa undani kabisa na kuweza kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 12 hapa kuna sehemu ambayo pamoja na hatua ya mafanikio ya serikali inaendelea kufanya juhudi ya kutafuta nishati mbadala. Mimi juzi nimesema mbele ya Waziri lakini nashangaa sana lile suala la umeme takataka halikupewa kipa umbele na serikali na hii ndio Serikali Kuu na hapa ndio kunako msimamizi mkuu. Inavyoonesha hatulitaki lile, ndio maana yake. Jamani umeme mbadala ni *very expensive*, tusitafute kitu ambacho kilichokuwa ni ghali. Hizi tafiti zimeshafanyiwa muda mwingi sana tumefanya utafiti ukanda kule sehemu za Makunduchi na sehemu nyengine.

Tutasema kila siku lakini halitekelezeki, *simple case* taka taka zipo zinazagaa. Kampuni iliyokuwepo sasa hivi Sefrona iachie huru bado tunawaonea hawa tu. Naomba sana Mhe. Waziri tuone kitu ambacho kilichokuwa kipo karibu cha kuweza kutusaidia, hawa mpaka watakapokuja lini, wafanye *study*

wameshafanya *study* na wameshaona wana uwezo wa kupata *megawatt 60* mpaka 70 kwa taka tu tena tungojea nini, na wenzetu ndio wametia saini, hebu tutieni saini na sisi tuwaoneshe. Lakini tatizo Mhe. Mwenyekiti, wizara katika usimamizi wanakuwa wako *slow* sana. Hilo, Mhe. Mwenyekiti, tuseme ukweli utekelezaji unakuwa wa taratibu, mheshimiwa inaumiza sana.

Tunakwenda katika ukurasa wa 13 mfuko wa JK. Mfuko huo mpaka sasa hivi ni kweli tukubaliane tumefanya pupa, lakini hatukufanya pupa kwa sababu nia ilikuwa ni kuondoa umasikini kwa wananchi wetu upesi. Lakini mpaka leo hii imefikiwa wapi. Je, umezima moja kwa moja au utaendelea tena kuwaondolea umaskini wananchi wa Zanzibar kwa utaratibu ambao sasa hivi wa taaluma ambazo mtaweza kuwaondoshea bila ya pale mwanzo tulivyofanya mafamba. Naomba sana mfuko huo tueleweshwe sasa hivi ndani una kiasi gani, nataka nijue hivyo.

Ukurasa wa 15 naingia hapa sasa. Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya afya serikali inaendelea na mpango wa kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa. Mhe. Mwenyekiti hapa mimi sikubaliani napo. Nasema neno la Rufaa Hospitali ya Mnazi Mmoja futa kabisa. Nina ushahidi tosha wa kusema futa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wa Afya alizungumzia suala la *insulin*. Mhe. Mwenyekiti, naomba niisome *document* sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa siku zote jamani tukisema tuseme jambo kwa ushahidi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wangu Naibu Waziri anapenda sana kuripuka bila ya kutafiti. Mhe. Mwenyekiti, nina karatasi hizi na anibishe Mhe. Waziri mwenyewe yuko mbele yako hii hapa. Mkutano uliofanyika Wizara ya Afya Zanzibar tarehe 12 April, 2013 mwenyewe waziri alisimamia. Mkutano huu umeitishwa na Mheshimiwa mwenyewe Waziri wa Afya (Juma Duni) kwa kupata maoni ya kitaalamu kuhusu *insulin.* Amewataka wataalamu kuwaita waje ku-*present* kuhusu *insulin*, leo ni safi si safi.

Mhe. Mwenyekiti, cha kushangaza Mheshimiwa wangu Naibu Waziri juzi anakwenda kusema kuwa inakubalika nchi za Kiafrika, wataalamu na wao wamo humu. Naisoma sasa.

"Profesa Swai, Dokta Kaushik Rimaiya wameombwa kutoa maoni yao kwa kuanzia madokta hao walisema kuwa maelezo yao yameegemea kwenye udhibiti wa vyanzo vya kisayansi ambavyo vinapatikana kwenye vitabu vya *internent journal.* Kwa mujibu wa matibabu ya kisasa *insulin* aina ya *workhardt Limited* ya India ili itumike mambo mbali mbali yanahitaji yazingatiwe:

1. Utafiti wa kifamasia.

2. Utafiti unaoangalia usalama wa binafsi wa dawa yenyewe.

3. Usalama wa kinga, ichunguzwe kwa dawa hii sio au ilete saratani au kusababisha ulemavu, upungufu wa viungo kwa watoto tumboni kwa mama.

Lazima ifanyiwa japo utafiti mmoja ulinganishwe na dawa ya kizamani *Norvo*. Wakati huo *Norvo* ndiyo inayotumika, sasa mtashangaa hapa kwa nini *Norvo* ikataliwe iletwe hiyo ya India kwa sababu gani. Dawa hiyo ambayo ni mpya ya *Wockhardt* kwa usalama na ufanisi wake ili dawa ya zamani *insulin norvo* ibadilishwe katika matumizi na kutumika dawa mpya ya *Wockhardt* lazima ipatikane ridhaa ya dokta na mgonjwa.

Huyu ni mtaalamu sio Mshimba, huyu ni profesa. Tunaendelea Mheshimiwa nisikilize vizuri Mhe. Makamu wa Pili anasema kwamba,

"Wataalamu hawa wawili hawajaweza kupata popote ushahidi kuwa dawa za W*ockhardt* zinafanyiwa uchunguzi uliokamilika, taarifa ya uchunguzi imeambatanishwa kuwekwa kwenye mtandao huo.

Mwaka 2004 -2007 dawa hizi zilileta matatizo na kuondolewa katika soko na mpaka sasa hakuna uthibitisho kuwa dawa hizi zimekubalika na taasisi mbali mbali ikiwemo Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na *USA, FDA*, Bodi ya Chakula ya Madawa ya Kimarekani. Wataalamu hawa baada ya kuuliza, wametoa taarifa kuhusu *insulin* husika na kutumika Tanzania Bara katika soko binafsi na nchi nyengine za Ukanda wa Sahara, Afrika na Bara la India kwa ajili ya nchi yenyewe na Bodi ya Chakula na kwa kuwa uamuzi wa dawa hizi na ukizingatia uthibitisho uliopatikana. Profesa Swai Dokta bingwa wa Kisukari Mwenyekiti wa *Tanzania Diabetes Association* Dokta Kaushiki Rumaiya, Dokta bingwa wa kisukari, Makamo wa Rais wa *International Diabetes* Federation, mjumbe wa bodi ya *World Diabetes Foundation.*

Mhe. Mwenyekiti, kilio cha wagonjwa wa sukari ni hicho. Mhe. Makamo wa Pili kipindi kilichopita nilieleza suala la mashine ya uchunguzi wa *cancer* na nikaeleza vizuri na ukafanya utaratibu mmoja nimeupenda sana, ulipokwenda kutembea ukawa hukupata jibu zuri na mazingatio. Lakini katika hadithi hii Kamati wa Chama cha Wagonjwa wa Kisukari walikwenda kumuona Waziri na wakafanya taaluma nzuri aliwaita wataalamu na mwisho wa habari wataalamu wakasema basi tutakuja kumuona dokta wenu ili kubadilishana mawazo na kuweza kuliamua suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, dawa inauzwa kinyemela. Dawa sasa hivi zinauzwa, tunawataka wapiga kura wetu, leo tunakwenda kuwauzia dawa inaletwa hapa kwa utafiti wa binadamu sio wanyama. Tunawapeleka wapi Mhe. Makamu wa Pili inasikitisha sana. Mhe. Mwenyekiti, katika *hansard* Mhe. Naibu Waziri wa Afya anasema sisi tunapotoa *tender* kila tunachokitaka madhali tunahakika kuwa hiki hakina tatizo, kwa hiyo hicho ndicho tutakacho kinunua. Hiyo ndiyo *hansard* ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Anasema hapa mwenyewe kama maneno hayo atanipinga na ajipinge mwenyewe. Mheshimiwa tena hiyo lazima kuna *somethings* itakuwa kwenye *tender*, hiyo kuna watu wana 10%, haiwezekani wanunue dawa hii ifanywe mfano kwa mwananchi kwenye mwili wake. Mhe. Makamu wa Rais chukua hatua uwaokoe Wazanzibari wasendelee kufa. Waite Mheshimiwa Chama cha Wagonjwa wa Kisukari, awaite madaktari wenyewe wahusika, awaite wenyewe Chama cha Wagonjwa wa Kisukari, ili waamue hili suala, msimlazimishe mgonjwa lazima atumie hizo, wakati zipo dawa ambazo wanatumia mbona hazikuleta matatizo, kwa nini. Mpaka leo mashine ya *cancer* zile pale tunapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Wallahi Laadhimu nimelipa shilingi 60,000/- kwenda kuchunguza kinyama kupelekwa Dar-es-Salaam, mashine tunazo, kumbe nasikia 10% ametoa *ten thousand dollars* mtu kapewa, kuidhinisha *tender* ile mtu akachukue machakara yale, yale machakara eti. Bajeti ya Wizara ya Afya sipitishi nasema mbele ya Makamu wa Pili sipitishi. Leo nimekwenda Hospitali pale katika wodi ya Wazazi, kitanda kimoja watu watatu, mtu anarudi kwenda kuzaa anawekwa na mwenzake, mpaka chini ukitoka nje wodi inanuka mavi. Halafu leo niseme Rufaa hii! jamani tunakwenda *International hospital* tunaona, Rufaa zilivyo, tunazijua Rufaa zetu, sioni katika maposho, sioni katika utendaji kwanza na kwenda kwenye hivi vifaa tu kuona hali halisi.

Kuna siku moja mgonjwa nilikuwa nipo pale anatoka *operation*, nikasema kwa nini huyu mzee karudishwa *operation*, anaumwa *pressure* au ana kitu gani. Kaambiwa nguo za kufunikwa mgonjwa zimekwisha, mgonjwa kashindwa kufanyiwa upasuaji kwa nguo na ndio sheria kwamba ilivyo, inauma sana. Halafu tukisema sisi tunadharaulika, tunaona kwamba aah! basi si porojo. Sio porojo wenyewe wananchi wanasikio huko, kinachowaokoa kitu gani namna ya kuielekeza serikali, nasema tena Mheshimiwa siipitishi Wizara ya Afya, nisipopewa ripoti kamili na ripoti hii waliyoikanusha na Dokta huyo Swai aitwe, Dokta Kariuki aitwe tuone. Allahi Makamu wa Pili kukifanyika jambo hili *Allahuma Amina* Mwenyezi Mungu atakuzidishia baraka, utaona huko mbele, kama nasema porojo au nasema vipi, utakuja kuona.

Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa ukurasa wa migogoro ya ardhi. Daah! Mhe. Mwenyekiti, juzi nimesema pale migogoro ya ardhi isaidieni wizara yenu. Lakini vile vile namshukuru sana Mheshimiwa mwenyewe kaja leo imekuwa vizuri sana na Mwenyezi Mungu amjaalie ampe umri umrefu, anajitahidi kwa kiasi kikubwa sana. Leo nimezungumza na Mhe. Mohammed Aboud amesema na waheshimiwa, tumo kweli tunaoiba ardhi. Waheshimiwa wengine tumo tunauza hiyo, tumo kweli hatukatai, kwa nini tukatae. Tusile dhambi lakini siku ya ardhi mimi nitakutajia wewe huwajua mimi nitakutajia. Waheshimiwa Wawakilishi, Mawaziri, tunaiba ardhi, ukweli tuseme kwa nini tukatae, piga kofi sawa sawa. Lakini siku ya Wizara ya Ardhi nitawasema mmoja baada ya mmoja kama wataninunia toa ripoti, hakuna tatizo lolote.

Mhe. Mwenyekiti, bado kauli ya Mhe. Makamu wa Pili ikubalike, watendaji Mawaziri, muungeni mkono mumsaidie lile suala limalizike. Mheshimiwa anajitahidi na sasa hivi mahakimu wameshaongezwa kwenye Mahakama ya Ardhi haitosaidia zaidi tusiongeze tena matatizo, amefuta vya kufuta Mhe. Waziri na anaendelea kufuta, inshalla Mwenyezi Mungu amjaalie mkono wake uwe mwepesi afute haraka haraka ili nchi yetu tupate wananchi waipende serikali yao kwa utendaji wao mzuri chini ya mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti ya kitabu hichi waziri nasema kuwa askari wangu jamii bado hajawatendea haki. Sijaona ripoti ya kuonesha kwamba kuna sehemu ambayo itawainua humu askari wangu jamii. Hilo Mheshimiwa hujanitendea haki hata kidogo. Imeelezwa tu kuwa mashirikiano mazuri katika usakaji wa madawa ya kulevya wakiwemo polisi jamii. Umenisaidia nini hapa. Mimi nimefikiria utasema kuwa mara hii polisi jamii nimewatengea fungu la shilingi milioni mia moja kama wenzetu, wameseka milioni 100 za mbwa kichaa, milioni mia moja mimba za paka kuuliwa. Waheshimiwa hawa polisi jamii wanaokoa mambo lakini hawana fungu. Lakini kutoa mimba paka zina fungu, mbwa kichaa zina fungu, hawa je, binadamu wanaotulinda sisi. Naomba sana Mheshimiwa lazima tuwalinde.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwamba tulipiga kelele sana tulisema kwa kweli mratibu tubadilishe mazingira sasa hivi visakina kwa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili havifai. Visakina vibovu lakini mpaka leo havijaletwa, nataka nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho aniambie ameshapata visakina vitano, vizuri, vipya viko kwenye *escort*. Naomba sana Mheshimiwa njoo unijibu suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kuhusu habari ya Kamati. Kamati teule zimesemwa hapa za Baraza la Manispaa, Kamati Teule za wizara, yote

yamesemwa Mheshimiwa. Lakini pamoja na hayo katika mtu aliyekuwa mbaya sana na akisamehewa basi inakuwa ni dhambi kubwa za mtu mwizi. Mheshimiwa mpaka leo hawajatiwa pingu hawa. Mheshimiwa katika masuala ya umeme imegundulikana kuna watu wezi. Lakini tukisema hivyo Mheshimiwa upande mwengine niseme kuwa hali sasa hivi ya mazingira ya kuwa zile kelele kidogo inaonyesha wizi kidogo umepungua, lakini haupungui kwa sababu watu bado wapo unajua wana mbinu gani za kuiba. Mhe. Mwenyekiti, watie pungu hawa, wapelekwe kwenye vyombo vya sheria, Mwanasheria unaye watie pingu wanaoiba fedha. Anayeiba Mheshimiwa msimuache kabisa kwa sababu anauwa fedha za umma, anawatia umasikini wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, msiponiambia, mnambie kuwa Manispaa kuna maeneo mengine yamesafishwa lakini kuna maeneo mengine bado kabisa hayajasafishwa. Tunaomba Mheshimiwa tujibiwe wanasema Mkurugenzi kajiondoa mwenyewe, sasa sijui kama ndio utaratibu mtakuja kueleza hapa. Lakini wengine wamekubalika wameondoshwa wengine bado hawajaondoshwa, tunaomba waondoshwe haraka haraka.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia na Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi haishirikishwi ipasavyo, kule tume ya wenzetu kule Bara, ukweli tuuseme ndio huo, ukiwaambia katika haya mambo ya uandaaji wa rasimu wala hawajui maskini ya Mungu, hawajashirikishwa mpala leo hii. Mimi naomba sana na wao katika wajumbe wa Tume na wao wamo kwa mujibu wa Katiba yetu na wao wanastahiki lakini wanakuwa wanawekwa nyuma na kwa nini iwe hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho nampa taarifa Mhe. Waziri wangu ambaye kwa kupitia yeye ndiye anayeratibu mambo yote ya Serikali Kuu hapa nimepata fununu, *yaimu shaka* kama kweli uongo Mheshimiwa Waziri Muhusika atakuja kunambia, hivi sasa vikosini kuna watu wanachangishwa fedha shilingi elfu saba kwa kila mmoja kusaidia timu ishinde. Hili suala mimi sikubaliani nalo. Kikosi cha KMKM kinawambia watoe fedha za ziada baada ya zile elfu moja moja na elfu mbili mbili, zinakwenda wapi siwezi kujua. Lakini sasa hivi wameambiwa watoe shilingi elfu saba na elfu kumi na elfu kumi na tano.

Mhe. Waziri muhusika kama huna habari basi kazuie mara moja ili suala lisitendeke, kwa sababu wenyewe wameshanuna, wameshahamaki, watetee katika fungu lao kuna milioni 30 za michezo, wakapeleke katika kusaidia timu, tunakubaliana nalo. Na zile za nyuma elfu moja moja, elfu mbili mbili kataa sasa, futa kabisa ili tuweke mustakbala mzuri. Mheshimiwa hakuna

sheria nimechungulia sheria hakuna sheria inayolazimisha askari lazima atoe pesa za *sports*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima siiungi mkono hotuba hii kwanza mpaka nitakaporekebishiwa hili suala la Makamo na kwenda kwenye Makamu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Bakar Makame: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa Audhu billahi minashetwani rrajim, Bissmillahi Rahmani Rahim. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuipongeza Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais akiwemo yeye mwenyewe pamoja na watendaji wake wote ambao ndio wanaomsaidia kuandika hotuba hii bajeti ya Baraza la Wawakilishi.

Pili Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikaanza na hivyo, mimi kawaida yangu la kweli nitalisema kweli na la uwongo silisemi. Kwa hivyo kwanza naingia kwenye Katiba ambayo Katiba tuliirekebisha 2010 kifungu cha 9(3) kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na imani kubwa sana na Serikali ya Umoja wa Kimataifa kwamba tuwe wamoja, tushikamane, tuelewane, tukubaliane kwa mustakbali wa nchi yetu. Lakini nimeingiwa na mashaka kati yetu. Serikali ya Umoja wa Kitaifa lakini kila mtu na chama chake. Mimi nilikwenda kwenye ukimbizaji wa mwenge, ukimbizaji ule wa mwenge ulikuwa ni historia, uliwashwa mwenge kule kwa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambapo amezaliwa. Lakini nimesikitishwa sana Mhe. Mwenyekiti, upande mwengine hakuhudhuria mwananchi hata mmoja.

Sasa nitamuomba Makamu wa Pili wa Rais hapa anithibitishie hawakupata mualiko wa mwenge kwa sababu tetesi tetesi tu ni kwamba watu wanaabudu moto, moto huuabudu ila utauabudu wewe mwenyewe kama hukumtii Mwenyezi Mungu, hapo moto utaupata na ni moto wa Mwenyezi Mungu. Mhe. Mwenyekiti, nimesikitishwa sana hata yule Mbunge na Mwakilishi wa jimbo lile hakuwepo. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha, nakuomba Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwa Waziri wako uje unieleze watu hawa hawakualikwa?

Huko nyuma huu mwenge ulikuwa kwenye chama lakini tumeuweka mfumo wa vyama vingi tukauchukua serikalini na miongoni mwetu sote tulikuwa tunashiriki kuukimbiza huu mwenge Mhe. Mwenyekiti, leo ndio utakuwa ndio moto. Moto utaupata kama hukumtii Mwenyezi Mungu (SW), hilo moja nilisema niliseme maana mimi ndio tabia yangu.

La pili nimesikitishwa katika rasimu ya Katiba. Rasimu ya Katiba niseme kwamba sisi baadhi ya viongozi tumewachemsha wananchi wetu na tunawachemsha kwa minstaarafu ya kwamba ni mimi. Mimi nasema Mwenyekiti, rasimu ya Katiba tuwaachie wenyewe wananchi. tusiwapotoshe wananchi, mimi nasema la kweli nitalisema. Mimi nimesikitishwa sana na Katibu Mkuu wa CUF jinsi alivyofanya mengine wametujengea uhalali mbaya sisi viongozi wa ngazi ya juu katika Chama chetu, mmoja mimi. Mimi ni Makamo Mwenyekiti wa akinamama Tanzania wa UWT Tanzania ambaye ninatokana na Chama cha Mapinduzi. Nimepangiwa ziara sijui ziara zile ni za nini, kumbe naitwa kwenda kusutwa, nilipokwenda kwenye ziara ninaambiwa wewe tumekuchagua juzi Makamo Mwenyekiti tumekutuma sisi kwamba tunataka serikali mbili kwenye rasimu ya Katiba na maneno mengi, mimi sikufurahiwa. Mimi nasema msimamo wangu ni serikali mbili. Msimamo wangu ni serikali mbili nawaambia wanawake wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi kwamba msimamo ni serikali mbili na muungano utaendelea. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hili nilizungumze na nimelizungumza kwa udhati kabisa kwa roho kunjufu kwa sababu mimi la kweli nalisema kweli na la uongo silizungumzi. Lakini kubwa zaidi Makamo wa Pili Rais, hebu nifahamishe Makamo wa Pili kuna nini huku juu viongozi nyinyi watu watatu. Baina ya Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, tumepitisha Katiba hii ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lakini inasikitishwa Rais wetu wa Zanzibar ananangwa na mtu ambaye yuko chini yake si vyema. Sasa nyinyi wakubwa ikiwa hamuelewani mnatuongoza vipi sisi wadogo huku.

Ninakuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na kila mtu ananisikia leo hapa. Kaeni kitako muwe wamoja msituyumbishe sisi wananchi. Hili nalisema kwa nia safi kabisa kwa sababu linajitokeza. Mimi ninamsifu sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na yote hajanyanyua mdomo wake kujibu, anatumia uungwana na kwa sababu anajua kwamba wana vikao wanakaa. Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Mwenyekiti sasa nichangie moja kwa moja kwenye kitabu hiki.

Mlhe. Mwenyekiti, nakuja ukurasa wa 46 namba V ya kirumi, Idara inaendelea kuimarisha shughuli za upigaji chapa ikiwemo mipango yake ya kukihamishia kiwanda cha upigaji chapa kutoka Saateni kwenda Maruhubi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nakuomba sana kwamba utafanya jambo la busara kama kiwanda hiki kitamalizika kabla ya mwisho wa mwaka, nakusudia 2013 imalizike, 2014 tuwe na kiwanda chetu cha Upigaji Chapa. Kwa nini nikasema hayo, kiwanda hiki ni cha zamani, kiwanda ni misukosuko mingi imepata, kiwanda hiki tokea mimi Naibu

Waziri huko nyuma ilikuwa kishafikwa na misuko suko lakini bado hakijapata ufumbuzi wa maana kuhakikisha kwamba tunajitegemea kwa kiwanda cha upigaji chapa.

Mhe. Mwenyekiti niende ukurasa wa 52 mimi nachangia kidogo kidogo tu maana yake niliyokuwa nayo nishayatoa rohoni, sasa haya mengine nachangia kidogo kidogo. Ukurasa huu wa 52 unazungumzia Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti huko nyuma tulikuwa sera za mawizara zote zinapita Baraza la Wawakilishi. Sasa naomba tena Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba sera zote turudishe tena tutie kwenye kanuni kwamba sera zote za mawizara zipitishwe hapa Baraza la Wawakilishi. Kwa nini nikazungumza hivyo, kwa sababu sera ndio dira ya utekelezaji, ndio dira ya mafanikio lakini tatizo linalojitokeza sasa hivi tunaletewa tu humu hata sera hatuijui imekaa vipi. Naomba sana ili tuweze kurudisha tena sera za mawizara zipitie Baraza la Wawakilishi.

Nikiondoka hapo nije kwenye Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi. Mimi sielewi naomba Waziri atakapokuja anielimishe vizuri kuhusu mafao ya watumishi wetu wa Baraza la Wawakilishi, hapa kidogo nitakuwa mgumu, mafao ya watumishi wetu wa Baraza la Wawakilishi, naomba aje anieleze vizuri Mhe. Waziri, maana yake hili suala lina *hang* hajulikani mwenyewe nani sasa aje anieleze mwenyewe nani kwa watumishi wetu hawa wa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu ni watu ambao wanafanya kazi hawana wakati, sisi tukitoka hapa tunakwenda kwetu tunalala miguu juu wao wanaendelea na kazi hawa watu na si kweli Mhe. Mwenyekiti kila Wizara ina mfumo wake kwa wafanyakazi wake. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kupitia kwa Waziri wako aje anifafanulie na kama halijatengenea nitakuwa mgumu kwa suala hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti nikiongezea baadhi ya mambo mimi niseme waheshimiwa wenzangu tuwe wakweli baadhi yetu tusisikume tu mambo. Kuna waheshimiwa humu wanafuatilia majambo kwa *evidence,* kwa sababu na sisi tuna jukumu na tuna dhima kwa wananchi wetu.

Mhe. Makamo wa Pili juzi hapa liliulizwa swali kuhusu Manispaa, ingekuwa si vibaya ningesema tutoke sasa hivi twende Saateni, tubadilike Mhe. Makamo tunasafiri tunaona mambo mbali mbali tubadilike Manisapaa Saateni si pakuwekwa vile ni mchafukoge. Mabanda yamejengwa hayakujengwa kwa *design,* mabanda yamejengwa hayakujengwa kwa ufasaha, maana yake ni vurugu mechi wanasema wenyewe. Namuomba sana Mhe. Waziri muhusika aende na ninamuomba Mkurugenzi aliyeteuliwa, imani yangu kubwa sana Mkurugenzi aliyeteuliwa safari hii asingoje kuzungumzwa kwenye Baraza la Wawakilishi, ninamuombea dua afanye kazi zake kwa ufasaha na ufanisi.

Aende akaangalie kabla bajeti ya Waziri haijasomwa ili tuende sambasamba na mambo yetu katika usafi wa mazingira.

Mimi nilifikiria nitachukua saa nyingi lakini nilijipanga kwa mambo hayo pamoja na kwamba nitakuwa mgumu Mhe. Mwenyekiti kwa baadhi ya mambo lakini yale niliyoyazungumza mwanzo naomba nije nipewe ufafanuzi mzuri. Siungi mkono kwanza mpaka nije nipewe mambo yangu matatu niliyoyazungumza rasimu, kuhusu viongozi wetu watatu na suala la mwenge nipate ufafanuzi mzuri hatuwezi kwenda namna hii Mhe. Mwenyekiti. Kama ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa basi kweli tufanye Umoja wa Kitaifa na ndio dhamira kubwa ya kuhakikisha kwamba Umoja huu wa Kitaifa utadumu lakini naona unayumba, kwa sababu mimi hawezi akanisemea CUF mambo yangu. Mambo yangu niseme mimi mwenyewe CCM, serikali ni ya Umoja wa Kitaifa lakini kila mtu ana chama chake lakini katika kujenga nchi lazima tuwe wa wamoja na ndio lengo na madhumuni ya kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Baada ya kuzungumza hayo nimezungumza kwa nia safi kabisa na nimezungumza kama kawaida yangu linalonikera nilitoe watu walisikie nisinun'gunike.

Baada ya kuzungumza hayo niseme kwamba kama nilivyosema sitounga mkono hoja kwanza nipate ufafanuzi, tena ufafanuzi wa kina. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii adhimu yenye heshima pamoja na wananchi wenzangu kutupa afya kwa kuweza kuwa uhai na uzima wa kufika siku hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, labda katika kusaidia mimi leo kwa sababu ninamshukuru Mwenyezi Mungu anasema usipowashukuru wenzako wananchi, wako, walimu, walokusomesha kwenye vyuo, skuli basi Mwenyezi Mungu hataki kushukuriwa kama hujawashukuru wenzako. Kwa hivyo naendelea kuwashukuru wenzangu wote nikiacha wazee wangu, walimu wangu wenzangu walionifikisha hapa nilipofika. Sina miujiza ya kufika hapa bila ya nguvu za wenzangu kwa kumtangulia Mwenyezi Mungu mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, kawaida yangu mimi huwa ninakuja moja kwa moja na Wazanzibari wote na Watanzania kwa sababu suala langu siku zote ninazungumza maslahi ya nchi na suala hasa la muungano na hasa kwa sababu waziri muhusika, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo inagusa masuala ya muungano.

Mhe. Mwenyekiti, viongozi wetu wawili waasisi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Hayati Baba wa Taifa Mwalim Nyerere, waliunganisha muungano wetu huu ulikuwa wa maslahi ya wananchi wa Bara na Zanzibar na ni Muungano wetu huu ulikuwa wa kuaminiana (*trust)* hiyo kubwa tu zaidi kila mmoja aliamini hivyo na mwenzake aliamini hivyo. Zanzibar tunaposema Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambapo tunategemea kutimia miaka 50, maana ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwaletea maisha bora wananchi, maji, barabara, umeme Afya Maendeleo, Majumba bora ndio maana ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sote miaka 50 tuliyokuwepo hakuna mkamilifu na sote humu tunabadilika lakini tukiingia ni wale wale. Sasa tunasema kufanya kosa si kosa kurejea kosa ni kosa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunapoanza kurejea historia za kila zilizopita tutakuwa hazishi kwa Zanzibar yetu hii tunayokwenda nayo kwa sababu kila mmoja ukimnyooshea kidole mwenzako mmoja, vitatu vimekuelekea. Ukinionesha mimi sita mimi nina kumi. Sasa mimi ninafikiri Mwenyekiti, ningeliomba watendaji Wazanzibari pamoja na sisi viongozi ambao tunaowakilisha wananchi wa Unguja na Pemba katika Baraza lako tukufu hili kwamba tuyasahau tusongeni mbele kwa kuijenga Zanzibar. Lakini kusema kwa sababu kwamba awamu hii imefanya kosa, awamu hii imekosa hivi. hatutomaliza hapo tutapofika. Kwa hivyo ninakuja suala zima la rasimu hii ya Katiba yetu ambayo iliyokuwepo sasa hivi. Nasema sitini sio 70,70 sio 80, 80 sio 90, 90 sio 2000, 2000 sio 2015. Mabadiliko *it is change* wazungu wanasema "*man propose God dispose"* Unachopanga wewe siku nyengine Mwenyezi Mungu na yeye analipangua.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, suala la muungano mimi ningeliomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa dhati kabisa kwamba tukae tuone kwanza nia ipo hilo la kwanza. La pili tuwe wakweli pande zote mbili kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, muungano wetu huu ni muungano uliokuwa wa kuaminiana, wa kupendana, wa kushikamana, wa busara, wa hekma na usikivu. Ninao ushahidi mkubwa tunaokwenda, kuna wakati sio Zanzibar tulikuwa na hali yetu ya uchumi nzuri ambao ulikuwa wa Afrika Mashariki nzima Zanzibar ndio ilikuwa na *reserve* ya pesa, mabuku yapo rekodi ipo lakini tulikuwa tunawasaidia na wenzetu Bara walikuwa hohe hahe.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 1977 kwa bahati mbaya Nduli Iddi Amin aliingilia ardhi yetu ya Tanzania. Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema uwezo tunao, nia tunayo tutamuondosha. Lakini aliposema yale aliona kwamba na nguvu za Zanzibar zipo ndani ya muungano. Zanzibar tukatumia raslimali zetu zote na reserve kwa kuweza kushikamana bila ya kuumbuana, bila kusutana, haitoshi hapo awamu ya tatu, wenzetu kama walivyokuwa hoi sisi tulikuwa tunaringa na madola sio shilingi, akaja mjumbe akataka msaada ule

ule wa kushikamana wa kupendana na ule ule wa kuridhiana *trust*, bwana nenda kwa mwenzangu angalau anisaidie mamilioni ya dola. Mimi huku hohe hahe na alimtumza Mzanzibari alikuwa Waziri wake huko Bara basi kama Zanzibar akapewa suala lile lile la udugu. Vitu vyote vipo hivi Mwenyekiti, najua zamani nilikuwa nazungumza mitaani naambiwa Raza anaropokwa, lakini ninashukuru leo rekodi zangu zitaendelea kuwepo katika *hansard.*

Lakini vile vile mheshimiwa nasema kama sio viongozi wetu watendaji wangelikuwa wakweli hapa tusingelifika leo tukagombana na kuona hali hii tuliyofika. Hakuna mtu asiyetaka umoja, hakuna mtu asiyetaka muungano, hakuna mtu asiyetaka mashirikiano, ndio nilipokuwa nasema nchi mbili huru zimeungana ya Tanganyika na Zanzibar tukaita Tanzania. Hapo kuna muungano sasa hili jina la muungano, ina maana kuna mwenzako ukaunganisha. Ninakuja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, awamu ya tano nataka niisaidie Ofisi ya Makamo wa Pili tunaita Fungu Baraka kisiwa hicho kidogo au Fungu Kizimkazi. Mhe. Mwenyekiti, awamu ya tano tulikwenda kusimamisha bendera yetu ya Zanzibar. Kwa bahati nzuri Idara ya Uvuvi Zanzibar wasajili, kuna nchi tano ikiwemo ya Marekani tuliwapa kibali kule, kuna historia nzuri ya ndege. Mimi ningeliomba siku moja Wawakilishi tungelikwenda mkaona ile hadhi iliyokuwepo pale, kuna ndege, kuna uvuvi basi walipewa wale kwamba ni *sports* kwenda kuvua.

Mhe. Mwenyekiti, walipokwenda na tuliwapa kibali wenzetu Idara ya Uvuvi wa Bara waliwatia ndani wale wakasema hivi hao kisiwa chetu kimo ndani ya ardhi ya Zanzibar, Bara wanasema ni chao na wakawatia ndani wale ikabidi tuingilie kati Idara ya Uvuvi Zanzibar, hicho kisiwa chetu siku nyengine alhamdullih huenda Mwenyezi Mungu akatujaalia kuna *gas* na mafuta humo wakawakamata wakawatia ndani, wakaambiwa bwana hili ni letu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwaambia wenzangu wa Zanzibar tusikimbie kwenye urasimu kabla ya mali zetu hatujajua ziko wapi na tunalipataje. Tusiingie kwenye urasimu, kuna vitu ambavyo tunavyovidai tunaviona vipo kwa ajili ya *generation* ni vyao kwa ajili ya watoto wetu sisi tukakimbia tu kwenye urasimu bila kufanya utafiti hali nzima ya Zanzibar, uchumi wetu na *assets* zetu tulizokuwanazo.

Lakini tukiwacha hayo Mhe. Mwenyekiti, kuna Tume hii ya Fedha ya Pamoja, tume hii Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Wazanzibari tuna mabilioni ya pesa katika suala zima la mkusanyo wa pande zote mbili hizi. Tume hii ya Fedha miaka nenda rudi inapigwa dane dane inazungushwa tu na nina hakika humu kuna mambo mengi. Sasa ninachotaka kusema kwa sababu hii Tume inakwenda tu *cabinet* inakaa. Mhe. Mwenyekiti, hofu yangu

tunapokwenda kwenye rasimu kama hatujajua namna tunavyodaiana tutakuja kumdai nani humu ndani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, haya mambo yanataka watu tukae tutizame, nimezungumza vile vile suala la mkopo, juzi hii mpya nyengine siku ya Jumatano, taarifa ya habari ya ITV usiku saa 5.30 Serikali ya Tanzania imekopa bilioni 77.7, katika bilioni hizo bilioni 52 ni *fly over* ya Dar es Salaam na bilioni 25.2 ni mkopo wa kibajeti. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mkopo huu ni wa Tanzania ambao wametukopesha ndugu zetu Wajapan kwa miaka 30 deni hili tunakwenda kulipa baada ya miaka 10 na deni hili *percent* yake ni 0. Mhe. Mwenyekiti ningeliomba mbali na kusema kwenye suala la ITV hata gazeti langu ninaweza nikasema gazeti langu la uhuru la Chama cha Mapinduzi ndio lilokuwa limeripoti, magazeti yote lakini ningelichukua magazeti mengine Mhe. Mwenyekiti, tungelikuwa tunatafsiri mengine tena. Utaambiwa aah! si unajua hawa si wenzetu lakini nimechukua gazeti la uhuru.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachosema mimi hapa mkopo huu Tanzania imekopa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapokopa inaambiwa ilipe, *fly over* hii ni bilioni 52 inasema imekopa muungano, muungano upi? serikali ipi ya muungano? Maana yake imekopa Serikali ya Muungano ipi. Maana yake Mhe. Mwenyekiti, hili si suala la muungano. *Fly over* bilioni 52.5 si suala la muungano inakuwaje useme serikali ya muungano italipa. Sasa mimi nataka wenzangu tusaidiane katika kufanya maslahi ya nchi twende mbele, tutafute mambo ambayo yatatusaidia na kwa nini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapokopa huko isilipe muungano na hii wanapokopa si jambo la muungano.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri lengo letu zuri lakini ninachotaka kusema kwamba katika yote hayo tusipotizama mantiki ya kushikamana ya kuendelea. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema juzi kulikuwa kuna viongozi wameondoka na sisi sote hapa tutakuja kuondoka, *we are all in transit*, sidhani hata mimi siku nyengine ni magharini ninaweza nikafika ni kazi yake Mwenyezi Mungu. Mimi nataka kusema kwamba tuwe na hisia ya kusonga mbele ya kuona kwamba nchi yetu hii inaendelea kwa ajili ya vijana wetu. Hii Mhe. Mwenyekiti, miaka 50 tulikuwa tunakwenda shakla baghla tu, hatuelewani. Sasa nasema rasimu imekuja tunachotaka tujue yenye maslahi yetu sisi Wazanzibari, vile vile haya mambo Mhe. Mwenyekiti, yaeleweke kuliko tu tunakimbilia kwenye rasimu, hiyo rasimu ina mambo saba yatakuja kuzaliwa kumi na moja mengine. Tujue tunachotaka nini, je, tumeridhika? Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mbali na haya hapa karibuni nilitaka kusema kwamba hakuna suala la kukaa pamoja, kulikuwa na matokeo ambayo mimi na wenzangu sote tunalaani, matokeo yote ya kihuni ambayo sio sifa kwa binadamu ikiwa Muislamu ikiwa si Muislamu hakuna Kur-an inayosema umdhuru mwenzako, tunasema tunalaani matendo yote ambayo sio mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati hivi karibuni pale nyumbani kwangu Padri alipigwa risasi sawa, Waziri wa Muungano katoka na helikopta kaja hapa bila ya shaka imemgusa kimadhehebu, kaja anasema Zanzibar kuna ugaidi hee! jamani, lakini mimi kama mfanyabiashara na kiongozi kwa sababu nimekuwa katika sehemu nyingi ikabidi nianze kutembelea sehemu za mabalozi ninazozijua, wakaniambia bwana yule kakusudia kuumiza uchumi wa Zanzibar, Zanzibar hakuna ugaidi kwa sababu Serikali ya Mapinduzi haijatoa kauli yake. Lakini kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu.

Arusha sasa matokeo yaliyotokea yote sikumsikia Waziri huyu kusema Arusha kuna ugaidi. Lakini Zanzibar kwa sababu kutaka kuumiza uchumi tuzidi kuumia, akasema Zanzibar kuna ugaidi. Kwa hivyo Mhe. Waziri, nakuomba kwa heshima na taadhima, Mhe. Waziri ni kaka yangu Mhe. Mwenyekiti na ninaomba Baraza lako tukufu lisema kwamba Zanzibar hakuna ugaidi ili tupate manusura sisi sote, si peke yangu kuna wengine wote walikuwa na uchungu hapa, iliposemwa Zanzibar kuna ugaidi, ilibidi tuhangaike usiku na mchana. Mimi pale kwa bahati ndege pale ndio nazisimamia karibu ndege tano zilisimama siku hiyo hazikuja zilikatisha safari. Sasa jamani katika mazingira tunayokwenda nayo lazima tukae pamoja tuheshimianeni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba katika mambo kama haya yaliyokuwepo ningeliomba viongozi tusisubsiri 2014, suala la OIC, Afrika Mashariki haya mambo yanaweza kutatuliwa muda huu tuliokuwa nao.
Mhe. Mwenyekiti, jengine nije kwenye utaratibu wa *diplomatic passport* kwa kweli ninataka kusema jamani, mimi leo ni Mwakilishi ninastahiki kuwa na *diplomatic passport*, nikimaliza muda wangu huu *u-diplomatic* sina tena. Sasa nilikuwa nikitaka kumtahadhirisha Mhe. Waziri, kuna watu ambao hawastahiki wao na watoto kuwa na *diplomatic passport.* Sasa hofu yangu moja hawa vijana na wazee wakaingia katika masuala ya madawa ya kulevya, ugaidi tutaharibu sifa ya Zanzibar. Kwa hivyo wito wangu ninaoutaka kuomba Mhe. Mwenyekiti, wale wote ambao wanafuatwa majumbani hawataki kutoa *passport* ule mtandao ukatishwe. Sasa mtu umemaliza muda wako au Razza kamaliza muda wake, sasa kwa nini tena ning'ang'anie *passport* kwa kitu gani, kama huna jambo jengine kwani hakuna *passport* nyengine, ziko *passport* eti unaweza kusafiria kokote duniani, kila kitu kinakwenda na utaratibu. Nataka nimuombe Mhe. Waziri, hili suala linaweza kuja kutuumiza sisi Zanzibar, kuna *passport* za *diplomatic* zimezagaa watu hawajazirejesha wanazitumia.

Mhe. Mwenyekiti, suala la muungano katika masuala ya Zanzibar nafikiri na Waziri huyu aambiwe kwamba bwana wewe ulichemsha, kwa sababu bila ya

kumwambia hivyo kwa sababu unaposema Waziri wa Muungano yeye kaja pale Waziri tunayemjua sisi wa upande wa Muungano ni Mhe. Mohammed Aboud, yeye ndiye aliyepaswa kusema jambo hili. Kwa hivyo ninalotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala zima la utendaji wa kazi, jamani ninaomba *cabinet* au tume hii inapokwenda kukutana na viongozi wenzetu, Mhe. Mwenyekiti, haya mambo yako wazi na yapo ambayo yanashikamana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kukuombeni Wazanzibari na viongozi hili suala la rasimu ya Katiba ni letu sisi sote ambalo Dkt. Shein kalirithi, Makamo wa Pili wa Rais kalirithi ndivyo kwetu sisi lipo mikononi mwa wananchi. Kwa hivyo mimi wito wangu kwamba nione jambo hili sasa tunaondokana nalo lakini vile vile tujue kwamba nchi huru ya Zanzibar imeungana na nchi huru ya Tanganyika.

Mhe. Mwenyekiti, labda kwa kumalizia tu nilisema namna gani tulivyokuwa tumeshikamana na utaratibu mzima wa hii tume ya fedha pamoja na mambo mengine niliyokuwa nakumbushia na hili fungu Mhe. Waziri, kama hatujalifanyia kazi tutakuwa tunalo tena. Kwa hivyo mimi ninachotaka kusisitiza tu kwamba hizi *assets* zetu tulizokuwa nazo tuzione, hesabu zetu tuzione ili tuone kwamba Zanzibar tuna kitu gani kwa sababu tunapokwenda huko mbele tusije tukadaiana pakawa hakuna makumbusho hakuna hesabu tunaingia katika mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kusema suala hili la pamoja na Zanzibar, suala la mazingira, uchimbaji wa mchanga. Mimi ninaona hili jambo si kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nitamchukua Waziri sasa hivi tutakwenda Mwanakwerekwe pale mpaka makaburi ya wananchi waliozikwa mbele ya haki wanachimbuwe sasa hivi, ukenda utakuta kule gari za ng'ombe, pale kuna Sheha, kuna Diwani, kuna viongozi wote tena jioni na mchana, sasa mimi nafikiri tusimtafute mchawi *are we serious*, tena yanafanyika mchana. Sasa mimi nafikiri haya mambo kama watu wazima tutafute namna ya kuweza kuyakabili. Sasa mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti utaratibu sheria tukitumia hiyo, namkumbuka baba Komandoo alikuwa anasisitiza siku zote kuhusu sheria *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niko tayari kuwasaidia wenzangu kwa kuipenda nchi yangu Tume ya Pamoja hii ya Fedha ya Muungano, nataka nikuhakikishieni kwa uaminifu nilioupata katika nchi hii hapa nyote mliokuwepo, baba zangu, babu zangu, vijana wenzangu kuna wazee nawamkia shikamooni, lakini ninachosema nashukuru kwamba nchi imeniamini ninayafahamu mengi kwa siku moja ninaweza kukutajieni tatizo hilo na viongozi wote waliokuwepo madarakani, hebu niteni siku moja kwenye Kamati Kuu au kwenye Tume ;ya Pamoja ya Fedha, siku moja tu tutayamaliza, Mhe. Mwenyekiti, hapa nimezungumza bashraf tu, hapa sijazungumza chochote. Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii jioni hii ya leo kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi kabisa napenda niunge mkono kwa kipindi kikubwa hali ya kisiasa katika nchi yetu imekuwa ni nzuri pamoja na kuwa kunajitokeza na mambo ya hapa na pale lakini hali ya kisiasa katika nchi yetu ilikuwa ni nzuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wazee wanasema kwamba mjenga nchi ni mwananchi mwenyewe, mwananchi mwenyewe ndiye mjenga nchi, kwa hiyo utulivu uliopo kwa ajili ya wananchi wetu waliopo walioweza kutuliza, sasa na sisi viongozi wajibu wetu ni kuendelea kuituliza hiyo hali ya nchi ya kisiasa iliyopo. Kwa hiyo bado nahimiza kama tuendelee kuiweka nchi katika nchi ya amani.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine na mimi ninataka nizungumze kidogo kuhusu hali hii iliyopo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Mwenyekti, wananchi wetu wote walijenga imani sana kama Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa italeta maendeleo katika nchi yetu na italeta mshikamano katika nchi yetu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka nitoe masikitiko kidogo kwamba pamoja na Serikali ya Umoja wa Kitaifa tulionayo lakini bado kuna matatizo Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeshindwa kuyasimamia ili wananchi wa Zanzibar wakaona wanafaidi maendeleo yao ya nchi yao na Serikali yao ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, nategemeo yote ni kwamba yale matatizo madogo madogo na vikwazo vidogo vidogo vyote vitaongoka, lakini bado hali haijawa nzuri hata kidogo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tulikwenda Tume ya Uchaguzi, katika kamati yangu tulikwenda Tume ya Uchaguzi na tukazungumza na Tume ya Uchaguzi na bahati nzuri mimi niliwauliza masuala watu wa Tume ya Uchaguzi kwamba Waheshimiwa katika daftari mulipokuja kuboresha daftari la kudumu kulikuwa na watu ambao walipiga kura mwaka 1995, mwaka 2000 na mwaka 2005, lakini bahati nzuri mulipokuja kuboresha hili daftari watu hawa walikuwa na vitambulisho vyote vya kupigia kura, lakini kwa bahati mbaya baada ya kuwekwa kwa daftari la kudumu la wapiga kura, mtu atapiga kura sambamba na kitambulisho cha Uzanzibari Mkaazi, ikabidi watu wale haki zao zote pamoja na kuwa na vitambulisho vyote wakoseshwe haki yao ya kuandikishwa na wakose kupiga kura. Sasa nikawauliza watu wa Tume, hawa watu nyie mlipita mkazungumza na watu wa vyama, mukahakikisha waliokuwa na vielelezo hivi watapiga kura na wakaorodheshwa watu kwenye madaftari, vikachukuliwa vitambulisho vyao vile vikatobolewa kwa ajili ya

kuwa hawa wataingizwa kwenye daftari, lakini kinyume chake hawa watu kwa nini hawakuorodheshwa na hawakuandikishwa kuwa wapiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzai wa Tume ya Uchaguzi aliniambia Mheshimiwa ni kweli na hawa watu walikuwa 2800 lakini kati ya watu 2800 watu 800 waliandikishwa na kuingia kwenye daftari, lakini hawa watu 2000 sisi baada ya kuwa lazima wapite kwenye vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi tulimuandikia Mkurugenzi wa vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi ili aendeleze akamilishe kazi yake lakini kwa bahati mbaya hawa hawakuandikishwa, Unguja na Pemba. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninajiuliza wale 800 kwa nini waandikishwe na 2000 waachiliwe wasiandikishwe, au Wazanzibari kuna daraja la kwanza na daraja la pili. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nilitegemea kama baada ya Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa tutakwenda vizuri na tutakwenda sambamba, lakini bado hali haijawa nzuri tunakwenda vile vile kiujanja ujanja, hivi tunaelekea wapi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Raza kasema hapa sote kama viongozi tutakaa kwenye uongozi kwa muda wetu na muda ukifika tutarudi mbele ya Mwenyezi Mungu, jamani kuna watu wanawadhulumu haki zao tujue tutakwenda jibu kwa Mwenyezi Mungu, tunapita katika ulimwengu na tunakwenda kuhojiwa. Waheshimiwa sisi kama viongozi tutakwenda kuhojiwa katika uongozi wetu, tuache jamani kuwadhulumu watu nafasi zao au haki zao. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini kama kuna sheria tunaiona sheria hii inambana mwananchi wakati tunasema sisi kwamba nchi hii mwenye mamlaka ni mwananchi mwenyewe, leo katika nchi hii ya Zanzibar kuna Wazanzibari halisi hawamo kwenye daftari la kupiga kura lakini kuna watu wanaokuja kutoka nje ya Zanzibar wamo kwenye daftari la kupiga kura, kwa nini tunawadhulumu haki zao kila siku tunakuja tukikaa hapa tukipiga kelele, kila siku mimi nalizungumza suala hili. Kuna watu sio Wazanzibari wamo kwenye daftari, wapiga kura wa Zanzibar lakini Wazanzibari halisi kuna mke kapewa kitambulisho kaandikishwa na ni mpiga kura mume hakupewa.

Mhe. Mwenyekiti, leo tumewachukua Masheha sasa hivi, ndio tunaowapa daftari na Masheha wanalosema wao ndio kweli ya mwisho, haiwezekani, Masheha wengine wanawadhulumu watu kwa sababu zao binafsi tu na wao ndio tuliowafanya kama ni wasema ukweli. Waheshimiwa nawaomba kama tunakwenda kweli na Serikali ya Umoja wa Kitaifa tuwachiane hadaa, hizi hadaa ziachwe, kwa nini tusiwe na nia safi tukamuachia Mwenyezi Mungu na kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka nilizungumze ni suala la muungano. Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu yeye ndie mwenye nguvu na analeta mabadiliko yeye. Waheshimiwa kila mwenye macho yake

haambiwi tazama, anaona mwenye bila ya kuambiwa tazama, hili Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hatuoni kama sisi ni watu wenye macho yetu, kwa kweli wenzetu wao wanapita njia za kiujanja ujanja kutufanyia ujanja. Kuna kero za muungano ambazo hii leo Mhe. Waziri katuambia kama kuna kero kama 13 zimeshatatuliwa. Hebu tuzitizame hizi kero za muungano zilizotatuliwa ndizo ambazo ndizo zile ambazo kuwa sisi Wazanzibari tunaweza tukaendesha uchumi wetu, tunatatuliwa kero za muungano zile ambazo kwa Wazanzibari hazitawasaidia, lakini zile ambazo Wazanzibari zitawasaidia zinakuwa ni vikwazo.

Mhe. Mwenyekiti, tulikaa hapa katika Baraza lako la Wawakilishi tukapitisha kwa kauli moja kwamba mafuta yatakuwa ni ya Zanzibar na yatatolewa katka suala la muungano, kwanini linakuwa ni kikwazo mpaka leo suala hili lisiweze kutolewa. Leo Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari walio wengi wamekaa kitako wameulizwa maoni na wametoa maoni, imekuja rasimu ya Katiba na juzi imetolewa. Lakini hebu tujiulizeni nchi mbili zilizoungana zilizokuwa ni huru Zanzibar na Tanganyika tumeungana nchi mbili huru, ikaja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo inakuja rasimu wanathubutu kusema kwamba wabunge wa Zanzibar wawe 20 Watanganyika 50 na zote nchi ambazo kuwa tumeungana, tukiwa kna Serikali ambapo tumetoa Serikali yetu na wao wametoa yao tumeungana tukiwa pamoja, leo wao wapate wabunge 50 sisi 20 kwa nini. Kwa mfano hii rasimu tu kwa nini waandike hivyo na wakati tumeungana nchi mbili, hakuna kuungana nchi mbili mkubwa na mdogo, mie nimetoa fedha zangu na wewe toa fedha zako sawa sawa, maana sisi tumetoa nchi yetu na wao wametoa yao tumeunganisha Serikali na Serikali tumeunganisha, leo wanatuambia sisi 20 wao 50, wapi na wapi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema katika wakati huu wa utandawazi Wazanzibari tusichezee shilingi katika shimo la choo, tumetoka miaka karibu 49 hii ya muungano, tunatafuta sehemu ya kutokea Wazanzibari kumiliki na sisi nchi yetu tukaenda, bado Mwenyezi Mungu leo katuletea mabadiliko haya ya Katiba nayasihi naomba mambo ya vyama tuyawekeni upande tutizame Uzanzibari tuende tupate mamlaka yetu ya Zanzibar tuongoze nchi yetu. Leo tukija tukikaa hapa tukisema mimi langu langu chambwi na mwenzangu ana chambi anavuta wallahi fursa hii tunayopata tutakuja kaa miaka 50 tuikumbuke.

Mhe. Mwenyekiti, muamba ngomba kila mtu anavutia upande wake, ile ngoma kama inaanza basi kila mtu anavutia upande wake apate chambi kubwa zaidi. Tusitegemee kwamba wenzetu watatuvutia sisi watuletee sie, watavuta chambi kwao. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba jana hapa nilimuuliza swali Mhe. Waziri wa Katiba, Mhe. Waziri, Wazanzibari wameshatoa maoni yao kauli ya Serikali ni ipi, yeye aliniambia kauli ya Serikali ilisema

itaheshimu maoni ya Wazanzibari. Waheshimiwa ninawaomba nawasihi maoni ya Wazanzibari yaheshimiwe, kama nilivyojibiwa jana waheshimiwe.

Mhge. Mwenyekiti, suala jengine ni kwamba tume hiyo hiyo ya uchaguzi mwenzangu kazungumza tumekwenda kwenye Tume ya Uchaguzi, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi anatuambia hakushirikishwa katika mipango hii ya kura ya maoni, walivyokuja kuulizia ni bajeti tu, wakatoa bajeti yao ikatengenezwa lakini baada yakuulizwa mambo ya bajeti yaliyobakia yote hawakushirikishwa kwa nini na wakati haya mambo ni ya nchi mbili, tume ya muungano na tume ya Zanzibar zikae pamoja warasimu mambo ya kura maoni, lakini kwa nini watengeneze kura ya maoni wapange upande mmoja upande mmoja usishirikishwe. Naomba Waheshimiwa wenzetu wanafanya ujanja kidogo kidogo, waswahili wanasema ujiti na macho.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mhe. Ismail Jussa Landu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muunba wetu kwa kutujaalia uhai na uzima tukawa tunaendelea na shughuli zetu hapa katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. Nikushukuru na wewe Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.
Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba nikukumbushe kwamba kanuni ya 58 (6) inasema,

> "Kila Mjumbe anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiopungua dakika 20 katika mikutano ya kawaida na dakika 30 wakati wa mikutano ya bajeti, lakini Spika, akiona inafaa anaweze kumuongezea msemaji dakika si zaidi ya 10".

Kanuni imetulinda kutuongezea sio kutupunguzia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kulinda haki yangu hiyo naamini na wewe utailinnda maana ndio madhumuni ya kukuweka hapo kwenye kiti naomba sasa niendelee.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wametangulia kuchangia na wametoa michango mingi na mizito kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwanza niseme kutokana na hali halisi ilivyo muda hauruhusu kuhoji kifungu kimoja kimoja cha matumizi, lakini niseme tu kwa jumla kwa kumwambia Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwamba atakapokuja kufanya majumuisho ajiandae na yale maelezo ya kina vifungu mbali mbali ambavyo katuomba

tumuidhinishie hapa. Kwa sababu bado kuna vifungu vingi ambavyo sisi haturidhiki labda nikisema kwa jumla jumla tu nitoe mifano kwa sababu kama natoa mfano nikisema kimoja kimoja nitazitumia dakika zangu 30 kwa kuzungumza vifungu tu, lakini bado takriban katika Idara zote kuna maswali kuhusu mishahara viwango vinavyopisha baina ya miaka tofauti, posho maalum, viburudishaji, kwenye gharma za safari, viainisho vya mafuta, vinywaji, masuala kwa mfano kwenye ruzuku, huduma za utafiti na mambo ya ukimwi, kwa jumla kuna vifungu vingi tu ambapo Mhe. Waziri, tutataka maelezo. Kwa hivyo ningemuomba hili Mhe. Waziri, alichukulie kwamba nimezungumza kwa jumla lakini ajiandae kwa sababu utapokuja kusoma kwenye vifungu nitavisimamia vifungu hivi mbali mbali nitake maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini moja niseme kabisa, nilipokuwa nikiangalia ukurasa wa 66 wa buku hili la makadirio ya mapato na matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2013/14, katika bajeti ya Idara ya Huduma za Makamo wa Pili wa Rais, nilikuwa naangalia kwenye fungu la safari, nimeona kuna safari za ndani ikiwa zimetengewa milioni saba. Sasa nimeelewa kwamba labda zitakuwa ni za watendaji wake, kwa sababu mwaka jana suala hili nililiuliza nikaambiwa safari za viongozi hawa zinaratibiwa chini ya mfuko mkuu wa Serikali. Nilikuwa ninaomba hili si kwa Makamo wa Pili tu, tutapokuja kusema Serikali iwajibike kwa pamoja ikija hebu itusaidie takwimu au gharama za safari za viongozi wetu watatu hawa wakuu wa kitaifa, tusaidiwe tujue sisi ndio tunaozilinda na kuzipitisha kwa fedha za walipo kodi wa Zanzibar tujue, tumekaaje, hilo moja katika yale ambayo niliyosema nilitaka kutaja mahsusi na yale mengine nimesema kwa jumla nitakuja kuuliza kifungu kwa kifungu wakati wa kupitisha vifungu, lakini ichukuliwe hii kama nimetoa *notice* kwa madhumuni haya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nimpe indhari vile vile Mhe. Waziri, katika vifungu kabla sijenda kwenye maelezo. Katika kitabu chake cha bajeti ukurasa wa 59 katupa muhtasari wa fedha ambazo kaziomba katika Baraza hili kumuidhinishia, lakini bahati mbaya sana ni kwamba fedha hizo alizoziomba hazioani na mafungu yaliyomo ndani ya buku hili. Mhe. Mwenyekiti, nimfahamishe naomba nitoe mfano hasa ninalolizungumzia ni katika kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa katika kitabu kaomba mia saba sabini na tisa milioni laki tano, lakini nikenda katika buku hili la makadirio mradi huu umeombewa 340 milioni ambapo 70 milioni ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na 270 milioni ni fedha za wahisani, sasa kuna tofauti kubwa sana hapa baina ya buku la makadirio na hotuba yake.

La pili Mhe. Mwenyekiti, katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kataja mapitio ya mipaka ya majimbo 80 milioni, ukifungua ukurasa wa 474 ya buku hili huzioni hizo Mhe. Mwenyekiti, katika vifungu vya maendeleo. Kataja kuendesha kura ya maoni bilioni nne mia tatu tisini na nne milioni, katika buku la makadirio huzioni katuomba tumuidhinishie. Kataja kufanya maandalizi ya uchaguzi mkuu 2015, mia mbili ishirini milioni huzioni, fungu pekee nililoliona huku ni la *democratic* and *powerment project* ambalo ni bilioni tatu mia tatu tisini na nne milioni ndio nimelikuta katika kitabu na nalikuta katika vile vile katika kitabu cha makadirio. Kwa hivyo nampa indhari ajiandae pamoja na vile vifungu vya kawaida nilivyosema, nikiseme kimoja kimoja, aje na zile takwimu zake zote tutakapokuja kumsimamisha vile vifungu hapa aweze kutuelezea matumizi yale ambayo ameyaondoa.

Mhe. Mwenuyekiti, baada ya kuzungumzia hali ya uchumi wa fedha sasa nije katika mchango halisi wa maelezo hasa haya yamejikita juu ya mipango ya serikali katika ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni ofisi kubwa sana hasa kwa Baraza hili, kwa sababu inazidiwa na Ofisi ya Rais na inayo pengine sijui niseme sawa yake au imemzidi kidogo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini hao humu ndani hawawakilishwi ndio maana wanakuja mawaziri wao, lakini Ofisi ya Makamu wa Pili, Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe yumo humu ndani.

Sasa kwa mnasaba huo Mhe. Mwenyekiti, nadhani hapa ndio pahala petu pa kusema maneno haya ya kuiambia serikali, na mimi nataka nimpongeze sana mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame ambaye kazungumzia kwa undani na mimi sitochukua muda mrefu sana katika hilo juu ya suala la udhati wa huu mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Lakini mimi nasema Waswahili wanasema, “mtu huangalia alipojikwaa sio alipoangukia”. Na Waswahili hao hao wakasema kwamba, “Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu ni mchungu”.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wengine tulianza kuona dalili za kutokuwepo udhati mapema sana, yale mengine aliyozungumza mama yangu Mhe. Asha Bakari sitaki kuyaingilia ni hisia zake na maoni yake. Lakini kataja suala la sherehe hapa, sherehe sisi wenyewe tuliamua hasa hatwendi na kuanzia sasa mimi kama Ismail Jussa nasema nimeamua hasa siendi, kwa sababu hatuoni wengine inapokuwa shughuli ya Makamu wa Kwanza wa Rais wakija.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naangalia alikuwa anasafiri Rais wa Zanzibar au Makamu wa Pili nawaona mawaziri wa *CUF* wakioneshwa katika televisheni wanakwenda kuwapokea na kuwaaga viongozi wao, lakini mimi nimeshakwenda si mara moja, mbili wala tatu nilipokuwa Naibu Katibu

Mkuu wa Chama changu kwenda kumuaga Makamu wa Kwanza wa Rais, inafika humuoni waziri hata mmoja kutoka upande mwengine, inafika pahala hata Meya na Mkuu wa Mkoa pia hawaji wakati mwengine. Sasa yametokea haya hatukusema, limetokea la mwenge mnatugusa.

Mhe. Mwenyekiti, Mzee Aboud Jumbe alikuwa akisema ukipanda mbigili utakula mbigili. Kwa hivyo nasema kwa udhati wa moyo wangu lakini mimi sitaki kwenda huko Mhe. Mwenyekiti, langu mimi kubwa hasa ni kwamba mfumo huu kwanza ni chaguo la wananchi wa Zanzibar na unalindwa Kikatiba, na kama kuna watu wana choyo na kuona utaondoka huu hauondoki hivi hivi tu, lazima uridhiwe na wananchi wa Zanzibar wenyewe.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, tujiulize watu wana nia ya dhati? Baraza hili limepita liliunda kamati ya kusimamia Kura ya Maoni chini ya Mhe. Ali Mzee Ali, mzee wetu na katika wajumbe wake wengine watano bado wamo katika Baraza hili, yumo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yumo Mhe. Ali Abdalla Ali, yumo Mhe. Ali Mzee Ali; aliyekuwa hayumo Barazani sasa hivi ni Mhe. Zakiya Omar Juma. Hawa waliteuliwa ikiwa Kamati ya Baraza haikuwa Kamati ya Serikali, imekwenda kufanya ziara lakini ikajumuishwa na watu wa serikali wakiwemo Katibu Mkuu Kiongozi, Naibu Mwanasheria Mkuu, (Ndugu Nassor Said Mzee) na Katibu Mkuu wa Fedha Ndugu Khamis Mussa; kwenda kuangalia mfumo wa wenzetu, wakakuta mfumo huu ni wa aina ya peke yake tunaotaka kuuanzisha hata huko hauko, lakini wakapata mambo ya kujifunza.

Mhe. Mwenyekiti, waliandika ripoti imekuja hapa, tumesema Mama Asha Bakari katoa rekodi yake nzuri sana, kila wakati anasema tufanyieni semina tuelewe mfumo huu na wengine mara nyingi tumelisema hapa na tukaahidiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, si mara moja wala mbili mpaka leo hakuna semina. Lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, kama kweli watu wana nia na wameukubali mfumo huu juzi hapa tumefanyiwa semina na mashirikiano baina ya viongozi wa kisiasa na watendaji wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ninazo taarifa kwamba Baraza hili chini ya uongozi makini na huru wa dhati wenye moyo mweupe wa Mhe. Spika Mhe. Pandu Ameir Kificho kulikuwa na pendekezo la kuwemo na mada juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Katibu Mkuu Kiongozi kaikataa mada hiyo na watu wake serikalini. Huyu ndiye anayeongoza utendaji katika serikali.

Sasa kweli tunahitaji Serikali ya Umoja wa Kitaifa? Kwa nini akatae mada kwenda kuwafunza Wawakilishi? Tusifanye usanii wa kuitamka mdomoni

iwepo hapa kama tunaitaka kweli Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Haya yamekuja ndio yametufikisha hapa leo na nasema kama umepanda mbigili utavuna mbigili tu, ustahamilivu pia unakuwa na kikomo Mhe. Mwenyekiti. Hilo naomba niliache hapo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nilirejee kwa ufupi tu, nilichangia katika bajeti na hapa ndio pahala pake sasa hivi pana kiongozi mkubwa wa nchi, namwambia tena Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye kwa mujibu wa Katiba na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ndio washauri wakuu wa Rais, wamshauri Rais, serikali hii kubwa mno mzigo kwa wananchi walipa kodi wa Zanzibar. Kama kufanya majaribio, kama kuwa na mafanikio Mhe. Rais miaka mitatu inatosha afanye tathmini hatumuingilii ndani ya Katiba, lakini tuna wajibu wa kuwasemea walipa kodi wa Zanzibar kusema kama hii inabeba gharama kubwa tumwambie. Naomba hili litazamwe tena Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti naomba nizungumzie Idara ya Maafa ukurasa wa 41 wa kitabu cha hotuba. Mhe. Waziri kaelezea kazi zilizofanyika na mafanikio yake na huu mpango wa kuongezea nguvu shughuli nzima za kujiandaa na maafa. Kama nilivyosema kuna hitilafu ya fedha, lakini sitaki kulirejea kwa sababu nimeshalizungumza. Lakini nataka anambie hasa tumejiandaa hizo fedha zinakwenda kufanya kitu gani? Isiwe fedha zote kazi yake kujenga uwezo kwa masemina na mawarsha tu, vile vifaa hasa vya kufanyia kazi za uokozi na kujiandaa na maafa vikawa havipo.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha zilipotokea ajali mbili wengine tulikuwepo pale kwa sababu wengine wamo katika majimbo yetu tumekaa bandarini boti za polisi zinakuja pale mafuta hatuna, hata utaratibu wa Kamati ya Maafa haupo, hawapo kabisa wenyewe pale, mwisho wakagombana na mawaziri pale nasikia wanapigiana simu wanatukanana matusi ya nguoni kila mmoja anakwepa wajibu wake. Kwa hivyo, watwambie hii idara inafanya kazi gani na hizi fedha zilizoombewa mara hii hapa zimeandikwa shilingi 262,528,000 na huku zimeombewa 779,500,000, zilizoandikwa katika kitabu hiki, tuambiwe zinakwenda kufanya kazi gani, zinakwenda kununuliwa vifaa ama ndio masemina na warsha yatoke maposho halafu tena kazi kama kawaida *business as usually* kama tunavyoambiwa. Naomba tupate maelezo.

Jengine nakwenda haraka haraka leo kwa sababu muda hamna na nina mambo mengi ni Baraza la Wawakilishi. Mimi nataka nimpongeze na kuunga mkono hotuba aliyoitoa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi wa Kitaifa asubuhi, kwamba ni aibu kuwa mpaka leo mwaka wa tatu tunavutana na serikali tangu Baraza hili limeanza kwamba tunataka mamlaka ya Baraza la Wawakilishi yawepo kwa Baraza la Wawakilishi lenyewe, iwe chombo

huru, hii si idara ya serikali, huu ni muhimili wa dola katika mihimili mitatu. Panazungumzwa kupitishwa sheria tunapigana danadana tu, akija waziri katika hili anipe kauli ya kutosha nisije nikamzuilia bajeti yake anambie kwamba lini mswada ule utaletwa katika Baraza la Wawakilishi.

Kauli yake ya mwishoMhe. Mwenyekiti, aliyotupa katika kikao cha *briefing* alitwambia kwamba wameshakubaliana kuwa badala ya kuletwa hoja binafsi au mswada binafsi serikali itaupokea uje katika taratibu zake na sisi tukasema lengo ni jema la mashirikiano, tumewaachia mpaka leo mwaka wa fedha mwengine unamalizika na tukiendelea hivi Mhe. Mwenyekiti, na mwengine utamalizika. Tunataka kuambiwa utakuja lini mswada huu atupe tarehe hapa ya kuja mswada huo.Kwa sababu yale mengine ya kudharauliwa chombo hiki yatakuwa hayapo Mhe. Mwenyekiti, na hili nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ajiandae kweli kweli, kwa sababu hatuwezi kukubali chombo hiki kudharauliwa, ajiandae vizuri wala hatotushughulika kwa kunyanyua Katiba, tunataka hoja za msingi. Tutalinda hadhi yetu na haki yetu katika Baraza la Wawakilishi, kama mawaziri wamejisahau *backbenchers* tutalinda haki za Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hilo naomba niliachie hapo niende katika Idara ya Uratibu. Hapa Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo kadhaa, Idara hii inashughulikia mambo ya namna mbili. Kuna uratibu kwa masuala ya Muungano lakini pia kuna uratibu kwa masuala ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, yote ni sehemu ya idara hii. Mimi naomba nianze na ya Muungano.

La kwanza Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki ukurasa wa 17 Mhe. Waziri kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais katuzungumzia Sensa ya Makaazi na Watu. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nataka maelezo kwamba hizi takwimu zilizomo katika kitabu hiki tulichopewa ndizo. Mimi ninazo taarifa Mhe. Mwenyekiti, kwamba takwimu hizi nyengine za kupika na kulifanyika kikao cha wakubwa wazito, mmoja wa Jamhuri ya Muungano na mmoja wa Zanzibar pakatolewa maelekezo juu ya takwimu hizo. Lakini hayakuishia hapo tu, mpaka pakatengwa na fedha shilingi bilioni nne ili kwamba ziwekewe Masheha na Wenyeviti wa Vijijini na Mitaa kwa Tanzania Bara ili kutengeneza mambo. Sasa nimezidi kupata wasi wasi nikaona hayo labda yamekwisha, lakini katika kitabu hiki nikapata wasi wasi nilipokisoma ukurasa wa 17 kwamba kumezungumzwa humu kuwa, kazi inayoendelea hivi sasa ni kuzichambua takwimu hizo ili kuweza kupata matokeo kishehia, kiwilaya na makundi mbali mbali ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kazi inayofanywa kikompyuta chini ya dodoso hili hapa ninalo ilikuwa ukilitia ndani ya kompyuta dodoso hili linatoa takwimu hizo kwa pamoja, kompyuta inafanya kazi yake ya uchambuzi, haijafanya *memory*

kama wazee wetu enzi ya zamani. Kwa nini tuambiwe leo kuna kazi mpya ya kufanya uchambuzi, kuna nini hapo? Mhe. Waziri akija aje atupe maelezo katika hili.

La pili katika Muungano Mhe. Mwenyekiti, la Polisi, namuomba Mhe. Waziri alitazame sana suala hili. Polisi wako ndani ya Muungano lakini ndugu zetu hao wa Polisi wanasikitika. Polisi wa Zanzibar ni moja katika nchi mbili zinazoungana, Jamhuri ya Muungano na Zanzibar si mkoa. Zanzibar ina Kamishna wake wa Polisi lakini kinaonekana kiutawala au kimgao wa bajeti tuna tatizo kubwa sana la bajeti Zanzibar kuonekana kama vile mkoa tu, wakati huo wanahudumia viongozi watatu kwenye bega, tusiusahau ana Rais wa Zanzibar, ana Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais wakija viongozi wa Muungano hapa ndio wanaelemewa.

Imezungumzwa na Mhe. Makame Mshimba gari za kuongozea viongozi zimechoka taabani, tupeni angalau gari za kutembelea viongozi si idara ya Muungano hii. Huko nyuma alikuwa Kamishna wa *ZRB* namshukuru na kumpongeza sana Ndugu Moh'd Hashim Ismail alikuwa akiwatengea fedha, naambiwa ilikuwa kama shilingi 20,000,000/- kwa mwezi kuwasaidia Makao Makuu ya Jeshi la Polisi kufanya shughuli zao sasa hivi zimeondoka. Kwa hivyo wanapata tabu wanahangaika, sasa aje atwambie Mhe. Waziri mambo ya Muungano hapa kwa nini Jeshi la Polisi linadhalilishwa kiasi hiki kutoka Zanzibar halafu ndani ya Baraza tukipiga kelele tuonekane wabaya. Vile vile katika Uhamiaji kuna mapato yetu kutokana na *visa* tumeyazungumza sana, sitaki kurejea kwa maelezo marefu muda unapita na bado nina masuala mazito nataka nije nipewe maelezo.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna suala jengine hapa hili linahusu nafikiri zaidi Zanzibar na nataka akija anipe kauli. Mhe. Mwenyekiti, Katiba hii imetambua usawa wa Wazanzibari wote mbele ya sheria na imeweka misingi ya kumtambua nani Mzanzibari na kuna sheria ya kumtambua nani si Mzanzibari. Mimi wala sitokwenda alikokwenda Mhe. Subeit Khamis Faki, mimi nitazungumzia jamii maalum hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jamii ya Wazanzibari wenye asili ya Kingazija wanadhalilishwa sana, kwa nini tunawafanya kama watu wa daraja la tatu. Maana kama wanaambiwa daraja la pili hawa wamekuwa daraja la tatu sasa, wanapotaka kwenda kutafuta *passport* mpya zinazuiliwa wengine wanaambiwa ukiwa wewe raia athibitishe uraia wake.

Baada ya Mapinduzi kuliwekwa *decree* ikaweka wazi juu ya uhalali wa wananchi wetu waliozaliwa Zanzibar kwenye Mapinduzi na vizazi vyao vinavyoendelea baada ya pale je, ingeainisha wananchi wenye asili ya

Kingazija. Kama ni msingi wa kihistoria kwamba wao walikuwa raia wa Ufaransa au raia wa Uingereza huko Uingereza kwenyewe kuna raia wenye asili ya Ki-Comoro na wamekubaliwa kuwa raia na kama pana matatizo ya kikanuni acheni basi yarekebishwe, lakini kubagua watu jamii nzima kwa sababu ya asili yake Mhe. Mwenyekiti, si haki. Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri akija anisaidie na najua na wewe utaliunga mkono kwa sababu ukweli ni kuneemeshwa wewe Mwenyekiti. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nije katika suala jengine la Muungano vile vile ni suala alilozungumza Mhe. Mohammedraza mali za Zanzibar. Mimi nataka kuongezea nguvu pale alipomalizia yeye, tunataka maelezo juu ya *status* ya Fungu Mbarak, *Natham Island.* Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ya uhuru ya mwaka 1963 imetamka wazi wazi kwamba eneo la Zanzibar ni visiwa vya Unguja na Pemba na *Natham Island* imetajwa kwa jina. Sasa tunaambiwa maneno yanatutatanisha hapa kwamba kuna wenzetu wameshataka kuvingilia, hebu tupeni ukweli, toeni msimamo wa serikali katika chombo cha wananchi wa Zanzibar ndani ya wananchi wa Zanzibar na Baraza la Wawakilishi nini msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya *Natham Island,* nataka maelezo.

Lakini jengine ambalo nataka maelezo Mhe. Mwenyekiti, ni suala la kuna nyumba ambazo wakati wa utawala wa Awamu ya Tano ya Dr. Salmin Amour Juma Zanzibar ilinunua, moja ilikuwa ipo Afrika ya Kusini tena naambiwa iko katika eneo la nyumba ghali kabisa, daraja la juu. Wenzetu wanaimezea mate hii na yalikuwepo maneno panataka pafanywe mafahamiano eti watupe nyumba Dar es Salaam itumiwe kwa matumizi sijui ya kama kwa Mamamu wa Pili wa Rais au vipi, halafu eti wao wachukue nyumba iliyopo Pritoria. Hatuwezi kukubali hata siku moja ndani ya Baraza hili Mhe. Mwenyekiti. Nataka maelezo juu ya nyumba hii akija waziri pia aje anitajie na hizo nyengine alizokuwa anazijua yeye zilizokuwepo kwa wakati ule.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Uratibu wa SMZ Mhe. Mwenyekiti, naomba niende haraka haraka. La kwanza mimi napata wasi wasi kwamba kweli kunafanyika shughuli za uratibu wa serikali? Idara hii ninavyoona Mhe. Mwenyekiti, haifanyi. La kwanza hali inayoendelea humu ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa serikali mara nyingi Mhe. Asha Bakari anauliza hapa yuko anayeweka rikodi hizi? Mimi Mhe. Mwenyekiti sitaki kutanguliza maneno akifika waziri atakuja kuniambia hapa. Kuna mawaziri wametupa ahadi Baraza lililopita mwaka jana mpaka mwaka huu unamalizika hakuna kilichotekelezwa, tena kwa kauli nzuri tu na kututia tama. Kwa hivyo tunazo rikodi zao, kila waziri ikifika zamu yake nitakuja kumkumbusha hapa. Lakini mimi napata wasi wasi

mratibu wa shughuli hizi ni Idara ya Uratibu na katika kitabu chake Mhe. Waziri kasema hivyo kwamba moja katika majukumu yake ni hayo.

Lakini la pili, hata ahadi za viongozi wanapokuwa nje ya Baraza zinazotolewa wananchi wengi wanalalamika wanakwenda viongozi wanafanya ziara wanatoa ahadi. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe mara ngapi katembelea pande kadhaa katoa matamko halafu wananchi wanalalamika hakuna kinachotekelezwa, nini inafanya idara hii.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ukitaka kujua udhaifu wa hili ni hii bajeti matayarisho yake hakuna uwiano, kama kuna Idara ya Uratibu kweli vipi bajeti ya Serikali moja kila mmoja na *format* yake. Kuna wizara fungu la mishahara lote liko chini ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji, kuna wizara mishahara inaingia sehemu nyengine, vipi ndani ya serikali moja? Mafungu mengine ukitaka kuyafuata ukayafuate katika vifungu tofauti na mafungu mengine utayapata katika mafungu tofauti, kuna nini? Kuna uwiano hapo?. Lakini haijatosha hilo Mhe. Mwenyekiti, tunaendelea na juzi katika semina tuliyofanyiwa kule Kiwengwa katika Hoteli ya *Dream of Zanzibar*, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango anasutana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Maliasili mbele yetu Wawakilishi, anamwambia takwimu sizo na ndizo alizotuletea serikali moja hiyo, pana uratibu kweli hapo Mhe. Mwenyekiti.

Lakini hata hotuba za bajeti tukizipitia katika kamati wenzangu watakuwa wanakumbuka hawa na wewe Mhe. Mwenyekiti, unakumbuka kwa sababu ndio mwenyekiti wangu katika kamati yangu kwamba kumekuwa na hotuba ya waziri ya kila mwaka, ni zile zile kuna *cut and paste* wanabadilisha idadi tu ya fedha zinazoombwa lakini maelezo ndio yale yale, pana uratibu kweli wa serikali hapo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, sio hilo tu. Katika utendaji mzima wa serikali nilihoji na wewe ni shahidi wangu, katika kamati yetu kwamba vipi ndani ya miaka mitatu mizima na inavyoelekea itakuwa miaka mitano mizima shughuli ya serikali katika idara nzima ni kucheza na mswada tu, unaambiwa mwaka wa mwanzo tulipatiwa mswada ulikuwa katika kamati ya wataalamu ya wizara, mwaka wa pili wanakuja kuripoti kwamba mswada umekwenda katika kamati ya makatibu wakuu, mwaka wa tatu unaokuja mswada umekwenda katika Baraza la Mapinduzi. Nikauliza hapa na mwaka wa nne tutakujakuambiwa upo katika Baraza la Wawakilishi na mwaka wa tano Rais atasaini, sijui tutaambiwa nini. Basi miaka mitano mizima iwe idara inafanya kazi moja tu. Mhe. Mwenyekiti, naomba na hilo litizamwe.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho nataka kutolea mfano na hili naomba Mhe. Makamu wa Pili mwenyewe akija aje atwambie hapa, si la Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hili, mwenyewe aje atwambie, hivi katika yale maagizo anayotoa yeye na wenzake ikawa hayatekelezwi yakawa hayatekelezwi wamekasimiwa madaraka angalau ya kusimamia nidhamu hawa watendaji walioko chini yao au kila kitu kimesimamiwa huko juu?

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kuna maneno mengi Zanzibar ndogo hii, kuna wengine wanafanya masihara wanasema kuna makamu wa tatu wa Rais, kuna makamu wanne wa Rais wamedhibiti kila kitu hawana hata zile nafasi za utendaji, kwa maana ya mawaziri lakini wao ndio wanaosimamia kila kitu. Sasa hebu tuambie kwamba haya mamlaka kakasimiwa kama Mtendaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Katiba hii kakasimiwa kuwasimamia viongozi walioko chini yake, hebu tuambie ukweli na hili namuomba mwenyewe aje atwambie hasa ili tuone kama kuna udhaifu wa utendaji Barazani, hili alitolee maelekezo Baraza hili ndio msimamizi wa sheria ya umma na serikali.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, suala la Muungano. Katika hotuba hii ukurasa wa 7 mpaka wa 10 Mhe. Waziri kazungumzia suala la Muungano na utaratibu wa kuandaa Katiba mpya. Mimi Mhe. Mwenyekiti, sitaki kutangulia sana katika hilo, lakini nilikuwa nasema kuna mambo kwanza katika utaratibu, namtaka waziri awe makini na akija hapa aje anitosheleze wenzetu wa Tanganyika watwambie wanautaka Muungano au hawautaki?

Kwa sababu kutamka tu hapa si hoja, kama wanautaka Muungano kweli tuone Muungano unaozingatia misingi ya haki, heshima na usawa wa Tanganyika na Zanzibar. Wakati wa Komandoo Dr. Salmin Amour tunakumbuka alifanya mkutano mmoja pale Uwanja wa Malindi panapofanyika mikutano, akasema alikwenda Butiama akamwambia Mwalimu Nyerere wakati huo, akamwambia yeye ndiye Nyerere mimi ndio Karume mdogo. Sasa niambie unautaka Muungano au huutaki, hotuba zipo zinasema kila kitu. Ilikuja ile Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kuchoka dharau.

Sasa hapa wenzangu wamesema na mimi ninayo hapa, huu utaratibu wa kupata Katiba lazima uwekwe sawa ili tupate Katiba ambayo inayazingatia maslahi ya pande zote mbili. Leo Zanzibar imeingia katika historia siku zote tutawatangulia kwa kila jambo sisi wastaarabu, dola kongwe kuliko zote katika Afrika zinazokubali hasara Zanzibar. Ndio maana Waingereza wakasema, tarumbeta ikipulizwa Zanzibar wanademka walioko maziwa makuu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, leo sisi tumeasisi katika Jamhuri ya Muungano suala la kura ya maoni, sheria tumepitisha hapa katika Baraza hili hata kama si

mimi lakini wenzangu wamepitisha hiyo sheria. Leo imeandaliwa rasimu ya sheria Zanzibar imeletwa kama taarifa tu hapa halafu mnategemea sisi tukubali kuiridhia hapa. Katibu akituletea tuiridhie hii.

Lakini si hilo tu, tunazo taarifa Mhe. Mwenyekiti, kwamba palikuwa na mkakati hata wa kutaka kurekebisha sheria katika Katiba kulitoa Baraza la Wawakilishi, wajumbe wake wasiwe wajumbe, kama si kuingilia kati kwa wakati tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulisimamia yakawekwa mengine hapa tukaambiwa yanakuja tunayasubiri kwa hamu tuje tuyaone kuna nini. Lakini ninachotaka kusema kwamba lazima utaratibu wake uwekwe wazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme kwamba, wananchi wa Zanzibar wamepewa fursa adhimu sana ya kuamua khatma ya nchi yetu. Ni muhimu sana kuitumia vizuri.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie maneno yangu uniruhusu dakika tatu tu, nataka kumnukuu Mhe. Mohammed Seif Khatib katika kitabu chake cha 'Wasaka Tonge'. Hiki ni kitabu cha mashairi na kinatumika katika skuli zetu. Katika kitabu hiki katunga shairi nafikiri wasia mzuri kwa Wazanzibari sote na madamu kimetoka Chama cha Mapinduzi, kada wao mkubwa nadhani kitakuwa hakiwakeri kuwa labda kitawaudhi akina Mhe. Asha Bakari Makame na wenzake.

Mhe. Mwenyekiti, shairi lake linaloitwa 'kosa' anasema hivi:

> "Mmetufunga kamba za miguuni, za mikononi, za midomoni na kututosa baharini. Eti mnataka tuogolee, tubengelee, tujiokoe hadi tufike ufukweni. Kosa letu kubwa kudai haki yetu, miliki, mnahamaki na huku mnatukashifu. Msitunyanyase sisi watwana, watu wa maana, tumeungana, kwa heshima na taadhima. Sisi tuna kwetu, wenye asili, ilo kamili, na serikali iliyopatikana kwa damu!

Narejea, "Sisi tuna kwetu, wenye asili, ilo kamili, na serikali iliyopatikana kwa damu! Kuheshimiana kwa kupendana, kuelewana, kusikizana, hilo tutakubaliana". Ndio mkataba mheshimiwa huo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru na nasema nazuia kwanza shilingi juu ya hotuba hii mpaka nitapokinaishwa juu ya mambo niliyoyatolea hoja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa dhati kunipa fursa hii ya kuchangia jioni ya leo. Imani yangu Mhe. Mwenyekiti,

kama ilivyozingatia kanuni ya 58 (6) kwa Mhe. Ismail Jussa, ni imani yangu tutazingatia Wajumbe wote katika kutoa haki sawa humu ndani ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, baasa ya kusema hivyo kwa heshima kubwa sana nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa imani aliyonipa, elimu niliyoipata na niliyoyaona juzi kutoka China, naomba nianze kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa heshima kubwa nitoe pongezi za dhati kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa namna na jinsi wanavyosimamia kazi za kila siku kwa kuwaletea maendeleo na haki ya wananchi wa nchi hii. Imani yangu Mwenyezi Mungu atawasaidia katika hili na kuwapa nguvu na uwezo ili waendelee kufanya kazi zao kwa busara na hekma zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza lolote kuna jambo nilikuwa nataka nisaidie kuweka sawa katika Baraza lako, kwa sababu sheria zinatutaka kuzungumza mambo ya ukweli ambayo yanatokezea au yale ambayo tunazungumza katika Baraza hili. Sasa kiintarafu inawezekana mwanadamu akazungumza ulimi ukateleza, naomba niweke sawa wakati Mhe. Mohammedraza Hassannali alizungumza kwamba Waziri wa Muungano alishuka Zanzibar na kusema Zanzibar kuna ugaidi. Naomba *hansard* isomeke kuwa aliyefika sio Waziri wa Muungano ni Waziri wa Mambo ya Ndani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hilo naomba liwekwe sawa kidogo ili lisomeke vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuweka sawa hilo nataka niende katika suala zima la utawala bora na nitajaribu kwa muda kama wa dakika 30 nizungumzie haraka haraka nipate kuyazungumza yote.

Mhe. Mwenyekiti, linafahamika suala la utawala bora na kwa bahati Baraza linajitahidi sana katika kusisitiza suala hili, katika kuelekeza na kuyazungumza yale ambayo hayafuati utaratibu wa nchi hii. Mimi hapa nina ombi kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ajitahidi, pamoja na jitihada anazozifanya basi namuomba zaidi ajitahidi kuongeza jitihada hizo kwa wale ambao si waadilifu, si wakweli na si wajibikaji katika Serikali ya Zanzibar. Bado kuna watu hawaitendei haki, kuna watu si waaminifu na tunajaribu kuwalinda kila siku. Mimi nimuombe Mhe. Makamu wa Pili ajitahidi katika hili pale ambapo tunazungumza watu waliokuwa si waadilifu, wadokozi wa nchi hii basi hatua za kisheria zifanyike haraka. Tunaanza kupata matumaini kwa nchi yetu baada ya kuanzisha sheria ya rushwa, imani yangu kwamba kitengo cha rushwa kitaanza kufanya kazi kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo naomba niende haraka haraka katika suala zima la Muungano. Mimi Mhe. Mwenyekiti niombe sana, sote tuna uchungu wa nchi hii, sote tuna imani na nchi hii na serikali yetu nafikiri pia ina imani na nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe sana, zile fursa za kisheria ambazo zimeelezwa basi ni vyema tukazifanyia kazi ipasavyo.. Linakuja suala la maoni, linakuja na Baraza la Katiba lakini baadae kuna Wajumbe wa Katiba. Huu ni wakati muafaka Mhe. Mwenyekiti, kulifanyia kazi na kulivalia njuga suala hili, ikiteleza basi yale manung'uniko vile vilio tutakuja kulia tena baada ya kupitisha Katiba mpya.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi niombe sana na niombe katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kinachooneka mara nyingi inakuwa ni tatizo la elimu, watu wengi wanapata fursa ya kutoa mawazo katika masula ya kisheria na ndio hili pia linakuwa linatugonga. Baada ya kuangalia utaratibu wa kisheria tunakwenda kulumbana katika masuala ya kisiasa hatimae kile tunachokitaka tunakikosa.

Sasa ningeomba kabla ya kwenda kwenye Mabaraza ya Katiba na wale ambao wamepata fursa ya kwenda kuchangia katika Baraza ya Katiba wakapata elimu ya kutosha katika kwenda kutoa mawazo kwa maslahi ya Wazanzibari Mhe. Mwenyekiti, hili lilikuwa ombi langu.

Jengine kabla sijenda kwenye vifungu mimi leo nilikuwa nimeandaa vifungu vitupu kabisa kifungu baada ya kifungu na nimekuja kuchangia hotuba ya Makamo wa Pili na pia kitabu pamoja na vifungu. Lakini kwa kweli vimeanza kupita vingi baaada ya kwenda katika ile dhamira ya kuisaidia, kuielekeza na kuikosoa zile kasoro tunaanza kurudishana nyuma. Kwa kweli, hayatuletei mema wala hayajengi mustakabala wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, tunapoanza kunyosheana vidole kwamba Makamo wa Pili akija hawa hawendi, Makamo wa Kwanza akija hawa hawendi, huko hakutuletei hoja wala hakutujengei sifa. Sisi wengine Mhe. Mwenyekiti, hata hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa tulikuwa hatuna imani nayo kwa sababu inatuonesha udhaifu wa wenzetu na tukaanza kusema hao wanaanza kutubebesha magunia ya misumari hatuyawezi yatatuchoma. Matokeo yake ndio haya wengine tunaanza kunyosheana vidole hapa hata muda wa miaka mitano haujamaliza. Sasa hii ni hatari Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sana leo tusiwe kama mbwa wa Kichina. Mbwa wa kichina Mhe. Mwenyekiti, usiku anabweka asubuhi anapelekwa dukani kwenda kununuliwa nguo. Lazima tuwe na imani ndani ya nafsi yetu tukubaliane.

Mhe. Mwenyekiti, tukianza kusema haya kwa kweli hatufiki pahala kila mtu ana ushahidi katika sisi. Sisi wenyewe tunatunga sheria Mhe. Mwenyekiti,

hatuzitekelezi. Leo hapa wameunda tume sasa tume haifuati taratibu, watu wanavitambulisho vya tume, hawapigi kura hebu tujitizame sisi tuko wasafi. Mhe. Mwenyekiti, wengine humu Mawaziri kuna Maofisa wa Tume, mtu anakagua vitambulisho vya kupigia kura si haki yake, Waziri hii sio sheria. Sasa tukianza kuzungumza haya hatutafika mbali. Sisi wenyewe hatuko safi *CD* zipo Waheshimiwa Mawaziri wapo wanawahoji wananchi wakati wao si Maafisa wa Tume ya Uchaguzi, tuviachie vyombo vya sheria ambavyo tumevipa mamlaka tumevitungia sheria vifanye kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee hiyo ilikuwa ni dibaji ndogo tu ambayo sisi tukianza kuonesha imani kwa wenzetu ambapo leo sikufikiria kama Waheshimiwa wanaweza kuzungumza. Mimi nitatoa mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Ismail Jusa Ladhu anafiliwa na mama yake mimi niko Dar-es Salam nikamtumia *messege* Mheshimiwa wa *CUF* na nimepanda ndege kuja mazikoni, lakini hawa Waheshimiwa wenzake anaozungumza yeye wa *CUF* sikuwaona nilimuona Mhe. Salmin Awadh, Waheshimiwa watatu tu mazikoni.

Sasa tuna mapenzi lakini haya mapenzi hawa wenzetu wa *CUF* wanayarejesha nyuma na wanasababisha imani itutoke. Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi sitaki kuendelea hapo. Mimi naomba niendelee katika suala zima la migogoro ya ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mada Mhe. Mwenyekiti, ili nipate kuzungumza na wenzangu wapate kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, masuala ya migogoro wa ardhi ukurasa wa 16 kifungu cha 30 imezungumzwa suala la usajili wa ardhi, mashamba binafsi na shamba ya eka tatu tatu.

Kwanza niipongeze Serikali kwa mfumo ambao wameuanzisha hapo wa kuamua kusajili ardhi na waliokuwa na migogoro ya ardhi kuripoti ili zile ardhi zao wapate kupata hati miliki. Ni wazo zuri jambo la busara lakini nimuombe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais baadhi ya maeneo ambayo tayari yameshaendeshwa kwa utaratibu ambao waliodhi ile ardhi imekuwa wanawabughuzi wale watu ambao wameanza kufuata zile taratibu za kisheria kuwatisha na kuwabughuzi kwenye kutafuta haki zao za msingi.

Sasa nimuombe hili suala alielezee kwa upana kabisa watu wafahamu kwamba tayari Serikali imetoa mazingatio haya ya watu kwenda kujisajili katika masuala yao ya ardhi ili kujulikana nani hasa ni mmiliki wa ardhi ile ambayo ilikuwepo baada ya kuanza kunyosheana vidole na kuanza kusuguana katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kuchangia katika ukurasa wa 19 kifungu cha 47 Madawa ya kulevya. Mimi niombe kabisa kwa dhati Mhe. Mwenyekiti, kwamba tukiamua tunaweza na tukiwa tayari hakuna linalotushinda.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu sana tulikuwa tunapiga kelele suala la ng'ombe kuzurura barabarani kila anayekuja hapa ng'ombe wanazurura, gari za viongozi zinakumbana na ng'ombe njiani. Sasa Serikali ilifikia pahala ikaamua sifikirii kama leo tutamkuta ng'ombe anazurura katika barabara ndani ya Manispaa ya Zanzibar, kwa sababu Serikali baada ya kauli kubwa na Mhe. Rais kupiga kelele nyingi na kuanza kukaripia, ng'ombe wametoweka, kama wanatokezea basi bahati mbaya lakini sio wale ambao tumezoea tulipoamua tumeona, baada ya ng'ombe kukamatwa na watu wa kawaida ng'ombe anakamatwa na watu wenye silaha kwa kuhakikisha kwamba kwa wale ambao ni wakaida katika suala zima la kuwaondosha ng'ombe katika Manispaa ya Zanzibar.

Sasa niombe kabisa katika suala la madawa ya kulevya. Hebu Serikali iamuwe kabisa kwamba sasa hivi tumeanza kupambana na masula ya madawa ya kulevya. Juzi nilipokuwa nauliza swali la nyongeza la Mhe. Fatma Fereji juu ya suala zima la kujenga *Sober house*. Hebu tutafute sheria kali ya kuweza kudhibiti suala hili kadri inavyowezekana. Mimi nafikiri kama tulivyoamua katika maeneo mengine kupambana na masuala mazima ambayo ni kinyume na Serikali. Basi Serikali iamuwe kwa dhati kabisa kupambana na wale wote wanaotumia madawa ya kulevya wauzaji na waingizaji katika maeneo mbali mbali katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika muelekeo ukurasa wa 23 kifungu cha 58 kuimarisha huduma za kiwanda cha upigaji chapa. Niipongeze Serikali kwa jitihada ambazo zimeonesha kwa kuboresha kiwanda cha Maruhubi na kuweza kukihamisha katika maeneo ya Saateni katika ile kadhia iliyokuwa ikiwakuta kwa muda mrefu. Basi hapa naiomba sana Serikali pamoja na jitihada za kuboresha, pamoja na jitihada za kuweza kuwaweka wapigaji chapa katika hali ya kileo, bali naomba Serikali nayo na sisi tuwe tayari zile shughuli zote za Serikali ambazo zitahitaji kupigwa chapa basi tuelekee katika kiwanda chetu ili tuweze kukipa nguvu na ufanisi ili kiweze kujenga tija na kukipatia mafanikio yalikuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapa naomba nizungumzie katika Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya kitaifa ukurasa 42 kifungu cha 87 tumeleezea mengi. Mhe. Mwenyekiti, tumeeleza namna ya kuienzi hitma, kurekebisho ya sheria ya kuwaenzi viongozi wa Kitaifa Sheria Namba 10 ya kwaka 2002. Lakini bado mimi nakuwa napata masikitiko Mhe. Mwenyekiti, na suala la kuweka kumbukumbu za viongozi wetu wa kitaifa. Suala hili tunalipigia

kelele muda mrefu lakini kila siku tunapokuja tunaambiwa Serikali imejipanga, inajitayarisha kutafuta vitu vya waasisi kofia aliovuaa Mzee Karume, kisu alichokuwa akitumia hawa, kwa nchi za wenzetu ipo historia za viongozi zote zimewekwa katika makumbusho.

Sasa ni suala ambalo limechukua muda mrefu, mimi kumbukumbu zangu tangu wakati wa Serikali iliyopita basi pia suala hili lilizungumziwa namna ya kujenga nyumba ambayo itaweka kumbukumbu za viongozi waliopiita vizazi, historia, utamaduni wao pamoja na yale yote ambayo wameyafanya katika shughuli zao.

Sasa niombe kwa dhati kabisa Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri basi hili suala la kuweza kupata hiyo nyumba ya kuweza kufanya shughili za kumbukumbu. Kama haiwezekani basi tukaombe ile nyumba za Mzee Karume kule Mwera tuiboreshe na kuweka kumbukumbu zake ili watu ambao wakija katika nchi wakitaka historia za viongozi na wao wazipate na wengine tuwatafutie kwengine.

Lakini vyenginevyo kila siku tunajitayarisha tunatengeneza Mhe. Mwenyekiti, kauli ambazo kwa kweli sasa hivi zimepitwa na wakati kwa kuzingatia kwamba Serikali imepiga hatua na kubadilika katika nyanja mbali mbali. Sasa kama tumefika pahala pa kubadilika na hili naomba Mhe. Mwenyekiti lifanyiwe hima zaidi.

Nikitoka hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kunukuu vifungu. Swahiba wangu mwalimu wangu wa kazi Mhe. Ismail Jusa Ladhu pale alisema vifungu hivi vina mashaka na kama tukiamua kukichambua kimoja baada ya kimoja tutakesha ukiangalia kitabu na mabuku kuna mambo ambayo hayana muelekeo.

Sasa kuna viwili tu nitavizungumza na vyengine nitakapokuja kupitia katika kitabu kikubwa basi tutakuwa tunapitia kifungu baada ya kifungu ili kuonesha kasoro. Pia najiuliza Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Fedha mwaka jana wakati tunachangia bajeti alipoleta wazo la Serikali la kupitisha vifungu ili tupate fedha za kununua meli, nikamueleza mwakani tukijaaliwa yale ambayo tuliyapunguza basi tuendelee kupunguza tutafute pahala pengine pa kuweka ili tuwasaidie wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tuna mifuko ya JK na AK fedha zake ndogo. Mimi naomba kuna baadhi ya fedha tukiziondosha na kuziweka katika mfuko lile tatizo la ajira kwa vijana wetu tutawasaidia, tutapata mabilioni ya pesa tutakwenda kununua meli na tutapata mabilioni ya fedha na kuekeza katika sekta ya vijana kuweza kujiajiri, bado wananchi wana hali ngumu. Sasa kama kuna

maeneo tumejiekea zaidi sivyo kwa nini tusiwapeleke vijana wakaweza kujiajiri.

Mhe. Mwenyekiti, fungu namba 22.0 uimarishaji Ofisi Kuu Pemba 2012/2013 waliekewa laki sita na mwaka 2013/2014 milioni saba laki tisa na arubaini elfu, imezidi sukari au unga mimi sielewi, soda imepanda bei kwa sasa hii tofauti kubwa laki sita mpaka milioni saba laki tisa. Sasa kama kuna pesa kama hizi Mhe. Haroun Ali Suleiman Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ana umasikini wa fedha tumpelekeeni asaidie vijana. Tuache kujenga mazingira ambayo kwa kweli sio kama hayasaidii lakini hata ukiondosha sio tatizo kubwa kiasi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, safari za ndani Ofisi Kuu Pemba fungu 22. 03.00 gharama za safari 2012/2013 ilikuwa milioni mbili 2013/2014 ilikuwa ni milioni kumi laki tano sitini elfu safari za ndani. Najiuliza nini kilichoengezeka kwa thamani gani kwa sababu unapoongeza kitu uongeze kwa thamani iliyoongezeka kama safari za ndani zimeongezeka basi tujue dizeli imeongezeka kiasi gani na gharama yake itakuwa kiasi gani, lakini unapoangalia tofauti kidogo inakuwa napata mashaka.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zingatia muda.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, simalizi hata hili kwa kuheshimu muda wako. Fungu jengine Mhe.Mwenyekiti, hili limepungua tusipige kwenye kuongezeka tupige kelele pia katika suala la kupungua. fungu la 22. 04. 00, 2012/2013. Ofisi kuu Pemba ilipewa gharama za mafuta walitengewa milioni sitini laki nane, mwaka huu walitiliwa milioni arubanini na tisa laki nane na hamsini elfu gharama za mafuta wamepunguziwa mafuta yashuka. Sasa sizungumzii katika kuongeza nazungumzia pia katika suala la kupunguza, kwa sababu kuna maeneo ukipunguza katika suala la mafuta basi kuna hatari za kupunguza utendaji wa kazi katika maeneo. Sasa haya ni baadhi ya maeneo lakini kama utakaa maeneo ni mengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa huzuni kabisa na masikitiko. Masikitiko yangu yanakuja kwa baadhi ya Waheshimiwa wenzetu wanatupa mitihani. Mhe. Mwenyekiti, na mitihani wanayotupa pale wanapopangiwa hotuba zao wakasema baada ya kazi nzuri ya hotuba hii nampongeza mke wangu na wanangu nawatakia kila la kheri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi jana kwangu kulikuwa hakukaliki mwanangu akaniambia yule Mhe. Waziri wa Fedha Omar Yussuf mbona kasema mke na wanawe, mbona na wewe baba sijakusikia, nikamwambia basi kesho nitizame nitakusifu. Kwa hivyo, na mimi baada ya kumaliza namtakia kheri mke

wangu pamoja na wanangu watatu Mhe. Mwenyekiti. Mwanangu wa kwanza anaitwa Lukman Ali Salum , Abuubakar Ali Salum na watatu Hikman Ali Salum Mwenyezi Mungu awape afya njema wanisaidie mzee wao katika utendaji wa kazi na utumishi wa wananchi wa Jimbo la Kwahani.

Pia sitowasahau wananchi wa Jimbo la Kwahani nawaomba wawe na moyo na nguvu katika kusimamia haki na uadilifu. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Salum Ali kwa kibwagizo chako cha kumalizia. Sasa ni nafasi ya Mhe. Hamad Masoud Hamad baadae Mhe. Omar Ali Shehe akifuatiwa na Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia mswada huu ambao Mhe. Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ametuletea.

Awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuajilia kuwepo hapa leo ikiwa tunajadili mambo ya msingi ya wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wao.

Kwanza nimpe pole Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mhe. Mwenyekiti, hapa tunazungumza mambo ya kitaifa mambo ya nchi. Sio kwamba mambo ya kijamii na ya kibinafsi yasitajwe. Lakini sidhani kwamba ni vizuri kwenda mazikoni kwa mtu halafu ukasema ulikwenda ukawa hivi na hivi, hivyo ni kusimanga na si vizuri ninavyofikiria mimi na wengine kwa kweli hawakubali bora akusimange peke yako kuliko kwenye hadhara hii, ni watu wazima sisi lazima tuchukuliane.

Mhe. Mwenyekiti, tulipitisha mswada hapa wa kuanzisha Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC)*. Mimi katika kuchangia nilisema maneno wengine wakacheka lakini sikuwa nafanya mas-hara. Nilikuwa na madhumuni na maana halisi nilisema hivi, kama Shirika hili la Utangazaji Zanzibar litaanzishwa kwa jina la *ZBC* na kama kiongozi wa shirika hili saa hizi wakati huu tunajadili mswada atakuwa ni yule yule atakayekuwa baaada ya kuanzishwa na sheria ile tuliyoipitisha basi isiitwe *ZBC* iitwe *MBC* mkacheka sana hapa.

Sasa namtumia salamu Waziri wa Habari, Utamaduni na Utalii namwambia hivi akimbie kamba kabla ya ngo'mbe Mhe. Said Ali Mbarouk (MBM) Mwakilishi wa Gando. Akimbie kamba kabla ya ngo'mbe kama hawezi kuisafisha nyumba mwenyewe wakumsafishia nyumba yake anamjua amsaidie mapema.

Mhe. Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu tumechoka na manyago ya *ZBC*. Hapa sisi tunazungumza mambo ya msingi na asilimia kubwa Wazanzibari wanatusikiliza sasa hivi. Sasa wakati mwengine vipindi hivi hurudiwa lakini Waheshimiwa kuna manung'uniko makubwa kwamba mbona utangazaji saa nyengine unakuwa wa kubabaisha, anaekwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub anamungunya maneno hasikiki labda pengine maneno haya yanaonekana yanaudhi, hatuudhi mtu hapa sisi tumeletwa na watu wetu kuwazungumzia mambo yao wayasikie. Mtu humu akikosa nidhamu Baraza hili lina kanuni zake, wasituhukumu kwa kutubania watu wetu wasitusikie *ZBC* salamu za Waziri wenu mtazipata maana hampo hapa narudia tena Mhe. Waziri kimbia kamba kabla ya ngo'mbe, maana ngo'mbe wa safari hii ni kipole.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais ambaye hotuba yake imesomwa na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed kuna mambo chungu nzima.Mimi nazungumza kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wenzangu wamezungumza na mimi nazungumza nnayo haki hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka tulipofikia Serikali ya Umoja wa Kitaifa haikuwa rahisi, nyote mnajua hapa kila mtu alitoka jasho tulianza mchakato na ulikuwa mrefu pakafanywa *lobbing* ya hali ya juu, kila mtu akenda kwa watu wake akasema anavyotaka yeye, lakini hatimae watu wakapiga kura ya maoni. Tumefanya marekebisho ya Katiba hapa Mhe. Ismail Jusa Ladhu amesema hapa Serikali hii imepatikana kwa kura ya maoni na naomba ninukuu kifungu cha 80 (a) cha Katiba hii *page 111*.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu kinasema hivi kura ya maoni kwa mabadiliko ya baadhi ya vifungu vya Katiba kifungu cha 48 cha sheria Namba 9 ya mwaka 2010. Sheria inasema hivi:

(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 80 cha Katiba Baraza la Wawakilishi halitaweza kutoa mabadiliko ya Katiba kuhusiana na sharti lolote lililokuwemo katika kifungu chochote kilichoainishwa katika kifungu cha pili cha kifungu hiki mpaka kwanza mabadiliko hayo yakubaliwe na wananchi kwa kura ya maoni.

Kwa hivyo, kama kuna mtu ana mawazo anajidanganya kwamba labda kufanya varange Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa iondoke ifutwe iwe haipo anajidanganya, *process* ya kuifuta hii ni ile ile tulioingilia. Kwa hivyo, mna maana gani vyovyote tufanyavyo na yeyote afanyae ama kutaka kui-*sabotage* Serikali hii au kutaka kui-*promote* Serikali hii, mimi nasema tukubaliane na tueleweke kwamba Katiba hii tuliipitisha sisi Baraza si lazima kwamba wengine walikuwemo au hawakuwemo, nazungumzia Baraza la Wawakilishi Zanzibar ndio waliofanya Katiba hii hapa.

Mimi nijiulize swali halafu nitajijibu halafu vile vile na kuna wengne wanauliza swali kama hilo. Mimi kama kiongozi mwakilishi nikizungumza na watendaji, si wa Serikali iwe wowote wale au watu wangu kwa maana kwamba wapiga kura wangu, halafu nikawaambia katika kuulizwa maswali nikawaambia kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni juu tu huku chini msiruhusu. Mimi nasema nikiulizwa hivyo na nitajibu hivyo, mimi mwenyewe najijua kwamba ni mnafiki ni mzandiki si mkweli na sifai kuwa kiongozi.

Sasa namuuliza swali hilo hilo Mhe. Ismail Jusa Ladhu, Mhe. Asha Bakar Makame, Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na kila aliyekuweko humu. Lakini hili nataka nijibiwe na Makamu wa Pili wa Rais. Nasema ikitokea hivyo yeye atajibu vipi na atajisikia vipi kama jawabu ni hilo kama nililotoa mimi kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni juu tu huku chini usiruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, *spirit* ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa humu ndimo ilimoanzia na humu ndio mwao. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nimefungua ukumbi huu Mhe. Mwenyekiti, hatuwafanyii haki watu. Sisi tumetakiwa tuwe mfano wa kioo, hatuna *spirit* hiyo humu. Mhe. Mwenyekiti. Mimi nitatoa mfano kama kuna *spirit* kuna ile ari ya sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Baraza hili sasa kuna Mawaziri na *backbenchers*, mbona silifahamu hilo hakuna upinzani humu. Humu kuna kuambizana ukweli kutoa *data*, kuelezana, kufahamishana kushauriana ili Wazanzibari wapate manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna choyo kuna Spika, kuna Naibu Spika, Wenyeviti wawili Baraza hili. Hivyo kweli kama kuna *spirit* miongoni mwetu katika hili, humu ni vyama viwili tu basi na mmoja hana chama Mhe. Mwanasheria Mkuu . Lakini kama kweli kuna *spirit* katika Baraza hili Chama cha *CUF* ni wa kukosa hata nafasi moja ya Uenyekiti.

Kama hilo halitoshi mimi kwa kweli nilisikitika sana na bado nasikitika na bahati mbaya Mhe. Spika, hayupo. pengine hata angekuwepo ningesema hivi hivi ninavyosema leo. Ziliundwa kamati hapa hizi ambazo sasa hivi zinafanyakazi Mhe. Spika, ndiye anayepanga Wajumbe. Kuna Kamati ya Fedha Uchumi, Fedha, Kilimo na Biashara, orodha ya kwanza iliyotolewa Kamati hii ilikuwa na Wajumbe 7, 4 *CUF* na 3 CCM nisikilizeni vizuri maana yake wengine mmekaa kama hamnisikilizi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya muda alinijia Mjumbe mmoja wa CCM akanambia Kamati ile vipi nikamuuliza kamati gani? Mimi hata habari sina

wewe uko katika kamati fulani na hivi na hivi, mimi habari sina akanitajia Wajumbe. Kamati hii si mpaka lazima mpate Mwenyekiti, nikamwambia hayo siwezi kukwambia kwa sababu masuala ya Uenyekiti na Makamo Uenyekiti ni kwenye kura.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kabla ya siku ya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamo kama ilivyo kanuni Kamati ikabadilishwa *CUF* akatolewa mmoja na CCM akaingizwa wamekaa CCM 4 na *CUF* 3 aliyefanya hivi Spika, ndiye mwenye mamlaka nani anayeweka Wajumbe katika kamati au kuna mwengine niambiwe *just* kwa sababu CCM wao wengi ili wapate uenyekiti, maana yake nini hii, hakuna *spirit.* Kwani hapa mimi nikiwa mwenyekiti, akiwa mwenyekiti nani na nani majukumu ni yepi si yale yale au kwa sababu kuna shilingi 50,000/= na 100,000/=. *This is very very unfair* na mimi kwa kweli limenisikitisha na litaendelea kunisikitisha na nyinyi kama mko *genuine* katika hili, basi lazima linasikitisha. Ingefanywa mara ya kwanza hivyo hivyo mimi sina tatizo kwani ngapi zimefanywa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi *spirits* hiyo haikuwepo, kamati nyingi sana tumekubaliana baadhi ya wajumbe, jamani basi kama ni hivyo kwa sababu hata ukipiga kura uwenyekiti na umakamu watachukua walio wengi, nani hajui. Lakini wakikubaliana hapana. Mwenyekiti awe CCM na makamu awe CUF, Kamati ya Mawasiliano ikadinda, wote hao, *so what*, ndio maana yake nini. Kwa hivyo, hata hilo Baraza kuna watu hawaridhiki na *GNU* na kwa maana hiyo tusiwaoneshe watu kidole kwamba wana tongo, kumbe macho yetu sisi yameoza.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye *ZEC* (*Zanzibar Election Commission)*. Juzi Rais wa Zanzibar ameteuwa tume na makamishna wapya. Hata kama wengine ni wale wale lakini tunasema ni tume mpya.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kama kuna watu wanafuja, wanaharibu, wanakoroga au wanatengeneza ni Tume ya Uchaguzi, ni *secretariats,* makamishna wao ni *decision makers,* wanakaa wanafanya hivi *policy* na inakwisha habari yake, lakini watendaji ukisikia kura zimevuja itakuwa ni wao, zimechapishwa nyingi, wameteuwa watu ni wao. Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo haliturudhishi kabisa. Tangu tume hii ilipoundwa ni zaidi ya miaka 20 ni yeye mpaka hii leo, miaka 20 maana yake nini, ana uwezo eeh! kuliko wengine na kwa hivyo aendelee kuwepo hapo mpaka astaafu, ndio maana yake. *Secretariat* ya Tume ya Uchaguzi waheshimiwa iliopo pale saa hizi, hawa ni wafanyakazi wa serikali walikuwa wanafanyakazi mahali fulani huko wakahamishiwa pale. Tunaiomba Tume ya Uchaguzi na Kamishna wafanye mabadiliko *is too much.* Wao sasa hivi wanakuwa ndio *instution,* kuna jambo unalifanya mpaka linafanana na wewe

miaka 20 hapo hapo, unalipi jipya, una mawazo gani, wewe miaka 20 una mawazo gani mapya tuambie lakini bila shaka wako pale kwa madhumuni na maana fulani haiwezekani.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nasema hiyo tume huru si huru. Kuna siku hapa tukijaaliwa...

Mhe. Mwenyekiti: Zingatia muda.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Sawa. Kuna siku hapa tukijaaliwa tutatoa ushahidi kwamba sio huru. Mhe. Mwenyekiti, waziri atuambie hapa ni mabadiliko gani ya msingi ambayo yatafanywa katika Tume ya Uchaguzi kuhusu *secretariats* na hata watendaji wengine wa wilaya, ili wadau wa uchaguzi wote waridhike, hilo ndio la msingi. Sisemi aridhike CUF au Chadema au CCM, wadau wa uchaguzi waridhike lakini *secretariats* iliopo kwa kweli naweza kusema sisi wengine hatuna imani nayo hata chembe. Mhe. Waziri uje utuambie hapa kabisa. Nasema tume sio huru imeingiliwa mno na yote yanataka kuingiliwa lakini tume haionekani kuwa ni huru.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, Katiba hiyo hiyo ukurasa wa 8 wa Katiba ya Zanzibar, unasema;

Ukurasa wa 8, Kifungu cha 9(3)

"Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Umoja wa Kitaifa na utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia"

Ukurasa wa 5(7)(2)(d), kifungu cha 7,

"Haki ya kupiga kura kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka 18", hiyo ni 7(1) kuna 7(2).

7(2)(d) inasema;

"Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria".

Lakini hapa anakusudia kwamba;

> "miongoni mwa mambo ambayo Mzanzibari anatakiwa awe nayo au atashindwa kuandikishwa kuwa mpiga kura, ni kukosa kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura".

Mhe. Mwenyekiti, ni zaidi ya Wazanzibari 50,000 hawana vitambulisho vya *ID* na wana umri wa zaidi ya miaka 18 na wanasifa zote, lakini wanashindwa

kuthibitisha. Kwa sababu kuthibitisha sio kusema tu kwamba mimi naitwa Hamad Masoud, nina umri wa miaka 19 au 30, sijathibitisha bado. Sasa hivi kuthibitisha umri ni gharama, uwe na shs.35,000 nani hajui hilo. Usipokuwa na *ID* kwa mujibu wa sheria wewe ni mkosa, ukamatwe, ushtakiwe na ufungwe na utoe faini, ndio sheria. Wote hao zaidi ya 50 wanatakiwa saa hizi wawepo jela, mbona hajakamatwa mtu, kwa nini hakuna *enforcement* ya sheria hii, tunatunga sheria lakini hazisimamiwi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba waziri anayeshughulika na upigaji kura atuletee marekebisho ya kifungu hiki, kwa sababu kifungu hiki kuthibitisha umri sio kazi ndogo, lakini kama ni kusema mimi nina miaka 40 nikakubaliwa, sawa. Lakini si hivyo. Uwe na cheti cha kuzaliwa ndio maana yake na ndio maana Masheha wote *syndicate*, unakuwa na cheti, aah! hicho ni kidogo, hivyo ni cha Muungano, hicho ni *fake*, yaani maamuzi ni ya Sheha kwisha. Kwa hivyo, kuthibitisha umri kuwa zaidi ya watu 50,000 Wazanzibari wenye haki zao ni kazi kubwa, tusitunge sheria au Katiba ambayo haitekelezeki au utekelezaji wake ni mgumu, tutakuwa tunafanyakazi gani sisi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika tano za kumalizia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba waziri atakapokuja hapa atuambie ni lini ataleta marekebisho ya kifungu hiki kwenye Baraza hili, ili suala la kuthibitisha umri kwa Wazanzibari zaidi ya 50,000 liwe ni rahisi. Mimi sikatai kuthibitisha umri lakini lifanywe ni rahisi, akili zipo, vichwa vipo na hili linawezekana, tusiweke vitu ambavyo ni *unaffordable* haviwezekani. *Prohibitive* vinamzuwia mtu kupata haki yake. Mhe. Waziri hili nakuomba kwa heshima na taathima.

Daftari la kupigia kura, Tume ya Uchaguzi. hayo nasema ni 7(2)(d) ukurasa wa 7 katika Katiba yetu hii ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, daftari la wapiga kura lina manyago. Juzi katika ziara zetu kama wadau wa uchaguzi, tumewakuta wananchi wana stakabadhi walizopewa katika wilaya kwamba wao wameshapigwa picha, kwa hivyo bado kwenda kuchukua nini *ID*.

Mkurugenzi wa vitambulisho, namtaja kwa jina Mohamed Juma Ame katika mikutano mbali mbali tuliofanya, alisema kwamba kuanzia siku unayopigwa picha wilayani mpaka kukipata kitambulisho *ID* haizidi wiki mbili. Hawa wanavyo, wana zaidi ya mwezi mmoja na wengine wana zaidi ya miezi miwili.

Juzi walipokwenda kwa sababu zoezi la uandikishaji limeanza Kaskazini A wakaambiwa hamtapewa vitambulisho mpaka Disemba. Kwa hivyo, Mhe.

Waziri Tume ya Uchaguzi unayo wewe. Mwambieni Mkurugenzi wa Vitambulisho awape *ID* wiki mbili zimeshapita, wana miezi miwili au mitatu au vyenginevyo zoezi la uandikishaji Kaskazini A lisimame mpaka wapewe vitambulisho vyao Disemba. Asija akatuambia kwamba zoezi hili litarudi, uzoefu hauoneshi hivyo. Kwa sababu zoezi hili kwa sheria zote zaidi ya 300 litachukua mpaka mwaka 2014, kwa hivyo hawawezi kutuambia kwamba watarudia tena mwaka 2014 na 2015 watu waweze kujiandikisha.

Mhe. Mwenyekiti, nakuheshimu sana lakini la mwisho nakwenda kwenye karatasi hii hapa. Katika ukurasa wa 67 jadweli hili. Mhe. Mwenyekiti, kwenye jadweli ukurasa wa 61 kuna changamoto zilizokubaliwa na SMT na SMZ kujadiliwa ili kupata ufumbuzi, kila jina litaitwa, changamoto, matatizo, adha, balaa. Sasa mimi nasema kuna changamoto hapa kama alivyoziita 13. Changamoto zimepatiwa ufumbuzi, zinaendelea kujadiliwa, hazijapatiwa ufumbuzi. Sasa nazungumza zile ambazo hazijapatiwa ufumbuzi mpaka hii leo tunasoma bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ni ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, mpaka leo Wazanzibari mjue linajadiliwa halijapatikana ufumbuzi, ati kushiriki kwetu. La pili, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, nalo bado. Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki nayo bado. Mgawanyo wa mapato, yaani mgawanyo wa mapato yatokanayo na msaada kutoka nje bado. Mgawanyo wa mapato yatokanayo na faida ya Benki Kuu nayo bado linajadiliwa. Tume ya Pamoja ya Fedha nayo bado.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hali hii nataka serikali mbili tu; moja ya Zanzibar na moja ya Tanganyika. Miaka 50 ya Muungano tunatimiza keshokutwa, tunajadili sherehe za miaka 50 za keshokutwa mambo haya ya msingi kwa uchumi wa Zanzibar, kwa mustakabali wa Zanzibar na Wazanzibari wenyewe mpaka leo yanajadiliwa, miaka 50 na utachukua mingine 150 hayapati ufumbuzi haya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, hii siiungi mkono mpaka hapo waziri atakapokuja hapa akaniridhisha, pamoja na kuwaridhisha watu wa Ole. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuahirisha Baraza kuna tangazo hapa, kuhusu semina ya Mamlaka ya Bima nchini.

“Kwa heshima tunaomba uwakumbushe wajumbe kwamba ile semina inayohusu shughuli za Bima nchini kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,

ipo kama ilivyopangwa keshokutwa Jumapili na itafanyika katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi hapa Chukwani.”

Waheshimiwa tunaombwa kufuata wakati ili tuweze kwenda kwa mujibu wa taratibu ambazo ilikuwa tumejipangia.

Baada ya maelezo hayo sasa nachukua fursa hii kuwashukuru sana wajumbe, kwa namna tulivyoonesha mashirikiano hadi tulipofikia hapa. Kwa hivyo, tunaahirisha Baraza hili mpaka siku ya tarehe 24/06/2013 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 24/06/2013 Saa 3:00 za asubuhi)